BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	Mhe.	Zubeir Ali Maulid	-	SPIKA
2.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
5.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
6.	Mhe.	Issa Haji Ussi Gavu	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
7.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais
10.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
11.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**

34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 23 Mei, 2018

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Hati Mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2018/2019. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Mhe. Tatu Mohamed Ussi (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii):

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 209

Ukubwa wa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kwa kuwa uteuzi na upangaji wa Wizara kwa mujibu wa Katiba na Sheria ni jukumu la Mhe. Rais, hata hivyo kama Wawakilishi wa wananchi tunapaswa kushauri tu. Na kwa kuwa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni wizara kubwa sana inayobeba mambo muhimu ya huduma za wananchi na inaonekana majukumu hayo ni muhimu yakafanyika kwa ufanisi.

Je, serikali haioni haja ya kuigawa wizara hii na masuala ya Sheria na Katiba yakawa mbali na Utumishi wa Umma.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi) – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 209 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuwa jukumu la kuteua na upangaji wa Wizara kwa mujibu wa Katiba na Sheria ni la Mhe. Rais. Muundo wa Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na mambo mengine ulizingatia mahitaji na mwelekeo wa serikali aliyoiunda. Adha, muundo huo unatokana na matokeo ya tafiti mbali mbali zilizofanywa zinazohusiana na masuala ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hayo naamini bado azma hii muhimu na kuna haja ya kuendelea na mundo uliopo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naomba kuuliza swali la nyongeza na nimpongeze kwa majibu hayo, nieendelee tu kushauri kama swali la msingi linavyojieleza unaweza ukaupokea ushauri au ukaukataa si kosa, pamoja na maelezo ya Waziri ukweli unabaki pale pale wizara ina mambo mengi hii na yote muhimu kwa wananchi.

Je, imezingatia kigezo gani cha kuzalisha Wizara ya Vijana, Uamaduni, Sanaa na Michezo kutokana na iliyokuwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wakati Wizara ya Katiba na Sheria zimeundwa mambo mengi makubwa Katiba na Sheria kuna utumishi suala hilo mpaka hivi leo ukiangalia hii ni wizara kubwa na kuna baadhi ya wananchi kutokana na ukubwa huo bado kumekuwa na malalamiko.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo kama nimesikia vizuri. Tatizo Mhe. Mwenyekiti Mhe. Jaku Hashim Ayoub anaposema hasemi na *microphone* matokeo yake inakuwa tabu kusikia na anajuwa tunalo tatizo la *echo* lakini hata hivyo wacha nijaribu kumjibu kwa kadiri nilivyosikia.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote ushauri sio kitu cha lazima, ushauri unaweza kuupokea au ukaukataa na kuna ushauri mzuri na kuna ushauri ambao sio mzuri unaweza kusababisha matatizo makubwa. Kwa hiyo, ni lazima kuwa makini wakati unapopokea ushauri na kufanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, Mhe. Rais haingiliwi katika maamuzi yake ana nguvu zake za Kikatiba na hizo ndizo zinazompa kuunda serikali yake kuunda wizara zake kwa mujibu anavyoona inafaa na anafanya hivyo kwa mahitaji na kuitazama vizuri Ilani ya chama chake aliyokwenda kuitangaza kwa wananchi na ahadi mbali mbali alizozitowa kwa wananchi.

Kwa hivyo, anavyounda wizara anaangalia namna gani atatekeleza Ilani hiyo na ahadi alizotoa kwa wananchi na wakati huo huo anaangalia hali ya uwezo wake wa kiuchumi katika nchi. Kwa hiyo, hizi wizara haziundwi tu mwenyewe baada ya kutafakari anaunda na muongozo unaomfanya na ni yeye peke yake anayekuja halafu kuulizwa na wananchi kile ambacho ameahidi kwa hiyo tumpe nafasi Rais wetu kufanya maamuzi ya msingi kwa maendeleo yetu wananchi wote na Wajumbe wa Baraza hili tukufu na hilo katika kutekeleza hivyo ndio matokeo

mazuri mnaona kila baada ya muda unapofika wa Uchaguzi Mkuu, Chama cha Mapinduzi kinashinda kutokana na umakini wa Rais wetu. *(Makofi).*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwanza, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatowa na ni kweli mamlaka, madaraka yote juu ya suala hili kwa kweli ni yeye Mhe. Rais wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa tumeona kwamba miaka ya mbele miaka nenda miaka rudi katika serikali ya awamu iliyopita au ya wakati wa Mhe. Rais Amani Karume alikuwa ndiye Rais wa Zanzibar palifanyika mageuzi ambapo Waheshimiwa Manaibu Waziri wote katika serikali walipata maagizo kwamba waende kufanya kazi wabakie Pemba sasa katika mazingira ambayo tulokuwa nayo hivi sasa awamu hii, ni utaratibu upi ambao Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wanatumia ili kuhakikisha kwamba katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vinapata uwakilishi wa kisiasa sawa sawa kwa upande mmoja hasa katika mazingira ambayo tunakuwa tunakosa katika masuala ya usafiri baina ya Unguja na Pemba zipo ndege najuwa lakini ni uwakilishi upi wa kisiasa ambao unakuwepo mara nyingi maana yake Mawaziri tunakuta wako Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti naomba kurejea tena Waheshimiwa Wajumbe wanapouliza maswali ya nyongeza kusema sana na *microphone* ndipo unapowasikia vizuri ili na ule mjibu swala ajibu kwa umakini kama nimemfahamu vizuri Mhe. Simai Mohammed Said naomba kumjibu maswali yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wetu wa Zanzibar alipounda serikali yake ameunda kwa kuangalia uhalisia wa nchi yetu kwa kuiona Unguja na Pemba na ukilingalia Baraza lake la Mawaziri hivyo ndivyo alivyounda, ili uwakilishi wa kila eneo upatikane lakini vile vile, alipowaweka Waheshimiwa Manaibu Waziri nia na dhamira ni kumsaidia waziri katika utekelezaji wa majukumu yake na si mawaziri wala manaibu mawaziri sote kwa pamoja tunawajibika kutekeleza majukumu kwa wananchi katika visiwa vyote viwili. Kwa kweli, kama mutaona Mawaziri wanakwenda Pemba kufanya shughuli zao Manaibu Waziri wanakwenda Pemba kufanya shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, na juu ya hivyo serikali yetu imewaweka Maafisi Wadhamini kule Pemba kwa msingi kama lolote linalotokea la haraka linashughulikiwa na wanaleta taarifa. Lakini viongozi wetu wakuu hivi karibuni tu Mhe. Rais alikuwa Pemba akifanya ziara kuoanana na wananchi kujuwa mambo mbali mbali yanayoendelea katika kisiwa cha Pemba na cha Unguja kwa jumla wake. Makamu wa Pili wa Rais anafanya ziara za mara kwa mara kwenda huko kwa msingi huo huo na viongozi wote Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na wote walioko katika serikali wanafanya hivyo kwa nia ya kuhakikisha tunatowa fursa sawa kwa visiwa vyetu vyote viwili na kuhakikisha majukumu ya serikali yanatekelezwa kwa ukamilifu wake katika kila eneo la nchi yetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 50

Mazingira Hatarishi yanayoikabili Nyumba ya Daktari katika Hospitali ya Kojani

Mhe. Ali Khamis Bakar– Aliuliza:

Naipongeza Wizara ya Afya kwa kuipatia nyumba ya daktari katika hospitali ya Kojani, ili kuondosha usumbufu kwa daktari atakayepangiwa kuwepo katika kituo hicho. Hata hivyo, lengo la nyumba hii limeondoshwa na baadhi ya wananchi kwa kuitumia vibaya ambako kumeondoa haiba yake.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kuirejesha nyumba hiyo katika ile dhamira yake na kuondosha migogoro na wananchi.

(b) Je, ni lini serikali itatoa kauli yake juu ya mazingira hatarishi yanayoondoa usalama wa nyumba hii na pia kuhatarisha usalama wa wafanyakazi watakaotumia nyumba hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar swali lake Nam. 50 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, nyumba hii iliyojengwa kwa ajili ya wafanyakazi wa Kituo cha Afya cha Kojani ni Mradi wa wananchi kupitia Mradi wa *TASAF*. Nyumba hii ilipokamilika ilikuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekti, nakiri kwamba kipindi cha nyuma kulitokea mivutano baina ya wanakijiji na uongozi wa Kituo cha Afya cha Kojani, wanakijiji hao walitaka pia kuitumia sehemu ya nyumba hiyo kwa shughuli zao.

Hata hivyo, kwa wakati huu mivutano hiyo haipo tena na sasa wafanyakazi wa kituo cha Kojani wanaishi katika nyumba hiyo kama ilivyokusudiwa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mazingira ya nyumba hii yapo salama na hapakuwa na viashiria vyovyote vilivyoripotiwa vinavyoashiria vitisho ama kutoweka kwa amani.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii inaonesha kuwa wafanyakazi wetu wanaendelea kuishi kwa amani na kwamba wapo salama wao na mali zao.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ambayo ya utekelezaji kabisa ili kuondoa tatizo kwa wana-*TASAF* hao ambao walikuwa nyumba hiyo

wanaitumia kwa kuwa wana *TASAF* waliridhia kabisa nyumba hiyo watumie watu wa afya naunga mkono suala hilo lakini swali langu lipo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuondoa tatizo kabisa wizara imejipanga vipi watu wa *TASAF* wale kuwatafutia pahala angalau lile liwe ni suluhisho la mwisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimeweza kutangulia kusema kwamba nyumba hii imejengwa kupitia mradi wa *TASAF* ambao ni mradi wa serikali na malengo na madhumuni hiyo nyumba haikujengwa kwa malengo mengine yoyote, isipokuwa ni ile ile azma ya serikali kuona kwamba huduma za Afya zinapatikana katika kisiwa cha Kojani ili kusudi kuwaondoshea wananchi wa Kojani usumbufu waliokuwa nao hapo awali. Sasa baada ya matumizi hayo kutokana na uelewa kidogo wa wananchi, wao waliamini kwamba nyumba ile wanaweza wakatumia kwa shughuli yoyote na sio ambayo iliokusudiwa na serikali. Lakini tumeweza kuwafahamisha na kwa sasa serikali kupitia ofisi ya Rais Tawala za Mikoa basi nitaka muhakikishi Mhe. Mwakilishi kwamba hatutegemei kutatokea tena mzozo wa aina yoyote katika nyumba ile na matokeo yake azma ya serikali ilivyokusudiwa ndivyo ambavyo nyumba ile itatumika na si vyenginevyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja na nyongeza. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kupitia Naibu Waziri kwa kujibu swali lake vizuri sana na naamini asingelijibu vizuri ilikuwa ni ufuatiliaji wake kwa sababu naamini keshakwenda mara mbili kuhusu jambo hili jambo kweli matatizo haya yalikuwepo lakini kwa ufuatiliaji wake na serikali jinsi inavyojitahidi suala hili limemaliza salama tena salama sana.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo kama hilo litakuwa lipo tena jengine katika uzio wa hospitali ile. Je, unaushauri gani na kauli gani uzio ule ambao kuwa sasa hivi ushakuwa mbovu wa hospitali ile ili kufanyiwa ukarabati wa juu kabisa. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Makame Said Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nichukuwe fursa hii kuzipokea sana pongezi ambazo amezitowa kutokana na juhudi ambayo tumeifanya katika kupitia katika kituo kile kukitembelea mara mbili zaidi, Mhe. Mwenyekiti pia na yeye naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza sana kwani nilipokwenda Kojani alikuwa ni mchango mkubwa sana katika kufanikisha hayo ambayo nimeweza kuyajibu hapa leo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la uzio naomba nikiri nako kuna changamoto ambazo ziliweza kuripotiwa na ambazo tumezibaini na kama nilivyoweza kusema kwamba wajibu wa serikali ni kuhakikisha kwamba ni kutatuwa kero za wananchi kila pahala na kila sekta mahala popote pale

zilipo ndani ya nchi hii. Hivyo, basi naomba nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba changamoto ile pia nayo itaondoka kama ambavyo imeondoka ya tatizo kubwa lilokuwepo la nyumba, isipokuwa naomba anipe muda kidogo tunajipanga baada ya kumalizika kuweza kupokea vizuri vituo vyetu pamoja na mambo mengine, basi tumuhakikishie kwamba uzio ule tunauchukulia hatua, ili kusudi kituo kile cha serikali na nyumba zake pia ziweko katika hali usalama lengo wananchi waweze kupata huduma kama serikali ambavyo imekusudia.

Nam. 13

Utambulisho wa Makamu wa Pili katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Simai Mohammed Said - Aliuliza:-

Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sura ya Nne, Ibara 105 (b) bado inamtambua Waziri Kiongozi wa SMZ huku mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar 2010 imemtambua uwepo wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

(a) Je, ni kitu gani kilichopelekea hadi sasa kushindwa kufanya marekebisho hayo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa zaidi ya miaka minane.

(b) Je, ni upi utambulisho wa Makamu wa Pili wa Rais pale anaposhiriki katika sherehe za Muungano huku utambulisho wake ukiwa haujatajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Sura ya Nne ibara ya 105(b) inamtambua Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati ambapo mabadiliko ya Katiba ya Zanzibar ya 2010 imetambua uwepo wa Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Aidha, ni kweli kwamba takriban miaka minne Serikali ya Jamhuri ya Muungano haikufanya marekebisho ya Katiba kulingana na marekebisho yaliyofanywa na Katiba ya Zanzibar. Itakumbukwa kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwaka 2011 hadi 2013 imeanzisha Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa lengo kuu la kukusanya maoni kwa ajili ya kurekebisha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utaratibu huo uliendelea kwa kuundwa Bunge Maalum la Katiba mnamo mwaka 2014. Hivyo, kwa kuwa bado utaratibu huo unaendelea tunaamini kwamba Katiba mpya itakapokuja hakuna shaka marekebisho hayo yatazingatiwa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwamba utambulisho wa Makamo wa Pili wa Rais utakuwa ni ule ule wa Makamo wa Rais wa Zanziabr pindipo atakaposhiriki katika sherehe zozote

zinazohusu Muungano kwa sababu katika Sura ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano imetambua uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vile vile, ibara ya 102 (1) na (2) zote zimetambua uwepo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kueleza kwamba katika ibara ndogo ya (2) kwamba bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii na katika ibara zifuatazo katika sura hii ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaundwa na itatekeleza madaraka yake kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mukhtadha huu bado Makamo wa Pili wa Rais atatambulika kama ni Makamo wa Rais wa Zanzibar, kutokana na kutambuliwa kwake katika marekebisho ya Katiba ya 2010, licha ya kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano haijaingiza marekebisho hayo kwenye Katiba hiyo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nimpongeze sna Mhe. Waziri kwa majibu mazuri nilikua nina swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, tumeona katika miaka ya nyuma pale panapohitajika kufanya marekebisho katika Katiba zetu tumeona mabadiliko ya 10 kwa upande wa Zanzibar mabadiliko ya 13 pamoja na 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzinia.

a) Sasa ni kwa nini kufanya marekibisho haya ya kuweka sawa juu ya utambulisho wa Makamu wa Rais hasa ni ambae ni kiongozi mkubwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kumekuwa kunasuasua kwa sababu ya kusubiri au kutumia jina la Katiba mpya ili utambulisho wa Makamu wa Pili ukawa sahihi baada ya Waziri Kiongozi ndani ya Katiba ya Muungano na tukenda sambamba kutokana na hadhi yake kiongozi wa kitaifa na utambulisho wake ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

b) Amezunguza amejibu vizuri juu ya katiba zetu na kutaka kusubiri Katiba mpya nimuulize tu Mhe. Waziri Katika hizi Katiba mbili zetu ambazo tulizokuwa tunazo, ipi ipo juu baina Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar ipi iko juu baina ya Katiba hizi mbili ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu marekebisho ya nafasi ya Makamu wa Pili wa Rais kurekebishwa kutambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyo sasa hivi inatambuliwa kuna nafasi ya Waziri Kiongozi na haijatambua kuwepo kwa nafasi hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lakini niseme kwamba kama nilivyosema awali katika jibu langu mama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imetambuliwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sasa wakati serikali inatambuliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hivyo, nafasi ya Makamu wa Pili wa Rais akiwa ni sehemu ya Serikali ya Zanzibar basi moja kwa moja anaingia. Kwa hivyo, sio suala la kusua sua bali utambulikaji wake uko pale

pale na hadhi yake ipo pale pale. Lakini kubwa zaidi wacha tusubiri hiyo Katiba ambayo tunatarajia muda ujao marekebisho yote hayo yatakuwepo, lakini utambulisho wake upo pale pale na hadhi yake ipo pale kwa sababu Serikali ya Zanzibar inatambuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Unapozungumza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ni sehemu ya Serikali ya Zanzibar kwa hivyo hilo nadhani liko wazi.

b) Swali jengine kwamba ipi Katiba iliyokuwa juu zaidi nadhani Mhe. Simai Mohammed Said unalielewa hilo, tulipozungumzia Zanzibar tunaongozwa na Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 na unapozungumzia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, kwa uelewa zaidi Katiba Zanzibar tunaitumia katika Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaitumia kwa upana wake katika Jamhuri yote ya Muungano wa Tanzania nadhani nimekujibu nashkuru. *(Makofi)*

Nam. 272

Msaada kwa Waandishi wa Habari Kuandika
Habari za Uchumi na Maendeleo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Zanzibar imejaaliwa kuwa na vivutio vingi vya kiuchumi ambavyo vingetangazwa vizuri vingevutia zaidi wawekezaji na kuisaidia nchi yetu kupata mapato na maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, inaonekana hakuna msaada kwa waandishi wa habari za maendeleo kuwawezesha kuripoti habari za uchumi kitalamu.

Je, wizara imejipanga kuwapatia mafunzo waandishi wa habari, ili waweze kutangaza vivutio vya kiuchumi kitaalamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 272 kama ifuatavyo:-

Hivi sasa, Shirika la Utangazaji Zanzibar limo katika kujipanga kiutekelezaji zaidi na moja wapo ya mkakati wake ni kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu wafanyakazi wake kwa lengo la kufikia huko kwenye uandishi wa fani maalum (*specialization*), ili tuwe na waandishi waliobobeya kwenye fani mbali mbali ziwa za kiuchumi, afya, kilimo na kuwawezesha kutangaza vivutio hivyo na vyenginevyo kitaalamu zaidi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza maswali madogo sana ya nyongeza.

a) Sasa hivi ni waandishi wangapi ambao wanapewa *program* ya mafunzo ya kusimamia mambo ya utalii, afya na mazingira ili waweze kuripoti habari zao zikiwa na uchambuzi

wa kina kama tunavyoshuhudia katika mbali mbali duniani, sijui itakuwa kanipata au nirudie tena.

b) Waandishi wangapi mumewapa mafunzo ya programu maalum kwa kuhusiana na habari za Baraza la Wawakilishi na Bungeni, ili waweze kuripoti na kuzichambua kwa kina.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi lenye kipengele (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, waandishi ambao kwa sasa hivi tumewapa mafunzo ya kiichumi lakini na fani nyengine kwa kutangaza zaidi kiuhalisia, kwamba bado hatujatenga waandishi sahihi ya kujikita katika fani ambazo zimetwaja katika swali lakini na fani ambazo amezizungumzia Mhe. Mjumbe. Ila tu waandishi wetu wa habari ni mahodari sana na wapo waandishi ambao wamejikita katika hizi fani. Kwa mfano, tuna mwandishi ambaye anaitwa Zuhura Mgeni Ali mwandishi huyu kajikita masuala ya kiafya.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba bado hatujawapa mafunzo au taaluma zaidi lakini pia kuna mwandishi anaitwa Mgeni nae pia kajikita katika masuala ya biashara. Lakini Mhe. Mwenyekiti hili nilichukue kwa Mhe. Mjumbe tutahakikisha kwamba tumewapa mafunzo kama nilivyojibu katika suala la msingi ili kuona kwamba wanapata mafunzo katika Baraza la Wawakilishi. Kwa upande wa Baraza la Wawakilishi lakini na kwa upande ule ambao amelizungumzia katika swali lake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Saraha Said : Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa sababu ya asubuhi njema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuamka salama usalimini. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, mimi nataka nimwambie kwamba uandishi wa habari ya taaluma yake, muhimu ni kujua lugha. Sasa nataka nimwambie waziri katika *ZBC* ana waandishi wangapi ambao wanajua lugha sahihi za Kifaransa, za Kichina pamoja na Kiingereza sahihi, sio *yes* na *no* ambao wamejiwekea watakapokuwa wanafanya *interview* za watu wanajua huyu *qualified* wa Kichina na huyu *qualified* wa Kifaransa naomba kujibiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mhe. Suleiman Sarahan Said, kwamba kuna umuhimu mkubwa ya waandishi wa habari kujua lugha mbali mbali ambazo zipo ili na wale wageni wanapokuja katika taifa letu ili wasikie na wao wamepata matangazo kwa lugha ambazo wazifahamu. Lakini, Mhe. Mwenyekiti naomba nimjibu Mhe. Mjumbe, kwamba suala hili sijalifanyia utafiti wa kina. Kwa hivyo, nalichukua na nitalifanyia utafiti wa kina baadae tutakaa kwa pamoja nimpe majibu yaliyo na usahihi ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri ka majibu yake mazuri na katika majibu yake amesema kwamba Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*) limo katika

kujipanga kutekeleza mambo mbali mbali ya kutangaza yakiwemo mambo ya kiuchumi, na vivutio mbali mbali.

a) Kwa mnasaba huo Mhe. Mwenyekiti, mashindano ya kombe la dunia yanatarijiwa kuanza rasmi mwezi ujao na Wanzanibari ni wapenzi wakubwa mchezo wa mpira wa miguu, kwa mnasaba huu wa kuitangaza Zanzibar na kutangaza mashindano hayo. Je, *ZBC* imejipanga vipi kuyatangaza mashindano hayo kutoka Russia.

b) Kama hawakujipanga kuonesha Russia moja kwa moja. Je, wana mpango gani wa kuungana na *TBC,* ili kuonesha mashindano hayo ili Wanzibari waone mashindano hayo katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake Mhe. Nassor Salim Ali lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali kupitia wizara yake ya habari ni kuhakikisha kwamba wananchi wake wanatapata habari sahihi, kwa wakati na kulingana na hali ya *technology* ambayo sasa hivi ...

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali analojibu Mhe. Naibu Waziri halihusu swali la msingi, kama ataendelea kwa msaada wa kiti chako sawa, lakini suala la msingi ni mambo ya kale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku sijakusikia bado.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali alilojibu Mhe. Naibu Waziri si swali la msingi aliliouliza Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, fanya marekebisho, maneno maneno.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Anatakiwa asijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa Mhe. Jaku Hashim suala hili halikumpasa yeye kuinuka na kusema kwamba halihusu kujibu yeye. Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi yako wewe ambae sasa hivi unakiongoza kiti hichi cha Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wakati tumo Barazani tuna Kanuni ambazo zinatuongoza katika Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba kaona kwamba jibu hili halifanani na jibu mama, nilitaka nimjibu tu Mhe. Mjumbe kwa faida ya wananchi wetu kwamba, wizara yetu imejipanga na hili, na mimi nitalipokea kama hawataona *live,* tutahakikisha kwamba tumejiunga

na vyombo vya wenzetu ili kuona wenzetu wanaona mashindano hayo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Nam. 83

Kufanya Ukarabati Madawati Yaliyoharibika

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza**:-**

Kumekuwa na tatizo kubwa la upungufu wa vikalio katika skuli zetu. Hata hivyo, yapo madawati mengi kwenye skuli mbali mbali ambayo yanaweza kufanyiwa matengenezo na yakaweza kutumika na kupunguza pengo la upungufu wa madawati.

(a) Je, ni idadi gani ya madawati ambayo yanahitaji matengenezo, ili yaweze kutumika.

(b) Je, kuna mpango gani kwa wizara kupanga bajeti kwa ajili ya kuyakarabati madawati yaliyoharibika, ili kuweza kuendelea kutumika tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 83 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo. Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa upo upungufu mkubwa wa vikalio katika skuli zetu za Unguja na Pemba. Pia, ni kweli kuwa katika baadhi ya skuli zetu vipo vikalio vilivyovunjika na vinaweza kutengenezwa.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Katika mwaka 2016/17, wizara kwa kushirikiana na Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kwa Unguja na Skuli ya Sekondari ya Kengeja kwa Pemba, ilifanya zoezi la ukaguzi wa vikalio katika skuli ili kujua idadi ya vikalio ambavyo ni vibovu na vinaweza kufanyiwa matengenezo na kutumika tena. Jumla ya vikalio vya wanafunzi 6,000 (viti, meza, dawati) kwa Unguja na 5,000 kwa skuli za Pemba vilionekana kuwa ni vibovu. Wizara kwa kutumia mafundi wa skuli hizo za ufundi ziliweza kukarabati jumla ya vikalio vya wanafunzi 3,414 kwa Unguja na wanafunzi 3,400 kwa Pemba.

Kwa mwaka 2017/2018, tathmini ya kujua ubora wa majengo, vikalio na miundombinu mengine ya skuli zote za serikali, inaendelea na idadi ya vikalio vibovu vinavyohitaji kufanyiwa matengenezo vitajulikana mara tu baada ya kukamilika kwa zoezi hilo. Napenda kuchukuwa fursa hii kuendelea katoa wito kwa uongozi wa skuli na kamati za skuli kusimamia matumizi mazuri ya vifaa vyote vya skuli, ili viweze kudumu kwa muda mrefu kwa vizazi vijavyo na kuendelea na juhudi ya kuvifanyia matengenezo vikalio vya skuli.

(b) Mhe. Mwenyekiti, wizara inatenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa vikalio na pia kuvifanyia matengenezo vikalio vinavyovunjika. Vile vile, wizara itaendelea kuzitumia na kuziwezesha skuli zetu za sekondari za ufundi za Mikunguni na Kengeja kuvifanyia matengenezo vikalio vya skuli. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa, ninavyofahamu kulikuwa na utaratibu wa skuli kupeleka ripoti wizarani kwa kila miezi mitatu, ripoti ambayo zinatakiwa ioneshe maendeleo ya skuli, mafanikio na changamoto zake na mambo yote yanayohusu skuli husika.

(a) Je, nilitaka nijue kwenye hizi ripoti zinazotumwa wizarani huwa hazioneshi idadi ya vikalio au madawati ambayo yamevunjika kwa kila miezi mitatu ili wizara ikapata kujua.

(b) Ningependa kujua katika skuli za Jimbo langu la Konde kama vile skuli ya Makangale Konde Msingi A na B pamoja na Msuka, ambapo nilitembelea nikaona yapo madawati mengi ambayo yameharibika hayajafanyiwa ukarabati. Ni idadi gani ya madawati yale yaliyoharibika kwenye skuli hizo ambayo yanaweza kutengenezeka na nini lengo la wizara ya kuyakarabati kwa haraka iwezanavyo madawati yale, ili kupunguza matatizo yaliopo pale katika skuli zile. Ahsane sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Seif Omar Abeid masuali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali ina utaratibu wa kupokea ripoti kutoka kila skuli na ripoti hizo zinaingiza mambo mengi mno, maendeleo ya kitaalamu na miundombinu na mengineyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ili kuweza kujiridhisha kwa sababu wakati mwengine mambo ya ufundi yana ufundi wake ndio maana tukapeleka mafundi kwenda kutathmini hali halisi ya samani zilivyo katika maskuli. Mwaka uliopiita tulifanya na tugandua idadi ambayo tumeitaja katika maelezo yetu ya awali hapa. Vile vile, hivi sasa mafundi wetu wanaendelea kufanya tathmini idadi kamili ya kila skuli itaonekana baada ya kukamilika ukaguzi huo ambao unaendelea hivi sasa Ahasante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunazo ya Amali, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara kwa juhudi kubwa ambazo zimejipanga kuhakikisha matatizo ya vikalio katika skuli zetu yanaondoka. Pamoja na jitihada hizo nampongeza kwa dhati Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendesha harambe kubwa katika Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwaki, Baraza la Wawakilishi la zamani na katika michango yote hiyo pamoja na Baraza la Wawakilishi tulichangia kuna zaidi ya bilioni moja nakuendelea.

Je, Mhe. Waziri pamoja na jitihada hizo na fedha hizo zilizopatikana ni madawati mangapi yamepatikana hadi hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman swali lake ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba suala hili linashughulikiwa na kamati ambayo iliyounda na Mhe. Rais wa Zanzibar mwenyewe na mpaka sasa kupitia mchango huo bado haijanunuliwa madawati hata moja, isipokuwa zabuni imeshakamilika na Kampuni ya Kichina imepatikana, na taratibu nyengine za kisheria za Mikataba zinaendelea baina ya serikali na Kampuni ya kichina. Baada ya hapo ndio tutajua vimepatikana viti vingi ngapi au samani gani nakadhalika. Ahsante sana.

Mhe. Hamida Abdalla Issa: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali naomba kumjibu swali moja la nyongeza:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara yako inapata misaada mbali mbali kuhusiana na masuala haya ya madawati, lakini pia inao Mfuko wa Madawati. Je, wizara yako ina mpango gani wakuwatumia amafundi wetu wa pale Mikunguni *Trade* Skuli, ili kupunguza gharama.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hatuoni kwamba tunaiongezea mzigo serikali kutokana na wanafunzi ambao tunawasomesha na mafundi pale Mikunguni *Trade* Skuli alafu kushindwa kuwatumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Hamida Abdalla Issa lake ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika utaratibu wa kutoa kazi za kiserikali ni kwamba mfumo ulioko ni kutoa zabuni, zabuni inapotangazwa basi makampuni yanaruhusiwa kuomba, hatuna upendeleo maalum kwa sababu kazi zinatolewa katika mfumo wa zabuni. Lakini hata hivyo kwa kazi zile ndogo ndogo ambazo tunaamini wanaziweza kwa mujibu wa uwezo wao, mafundi wa *Trade* Skuli unawapatia kazi hizi kama nilivyosema, haya madawati yaliyotengenezwa yametengenezwa yametengenewa na mafundi wa *Trade* Skuli pamoja na mafundi wa Kengeja Sekondari Skuli. Ahsnte Sana.*(Makofi)*

Nam. 23

Utaratibu wa Kusamehe Ushuru kwa Baadhi ya Bidhaa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Mhe. Mussa Foum Mussa – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa na utaratibu wa kusamehe ushuru kwa bidhaa muhimu kama vile mchele, unga wa ngano, sukari na tende kila ifikapo mwezi Mtukufu wa Ramadhani, lakini mara nyingi kwa walaji msamaha huo hauonekani.

(a) Je, Mhe. Waziri jambo hilo ni kweli.

(b) Kama ni kweli kwa mwaka huu wa 2018 wizara ina mkakati gani juu ya jambo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake Nam. 23 (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara imechukua hatua kwa mujibu wa Sheria ya Biashara nambari 14 ya mwaka 2013 ambayo imeweka kifungu kinachozungumzia suala la bidhaa zilizo chini ya usimamizi wa serikali *(control goods).* Sheria hii kupitia kifungu hichi imempa Waziri mamlaka ya kuzitangaza bidhaa zilizo chini ya uangalizi wa serikali. Hata hivyo, basi kwa kupitia kifungu hiki wizara imezitangaza bidhaa kuu muhimu tatu za chakula ambazo ni mchele, unga wa ngano na sukari zikiwa kama ni bidhaa zilizo chini ya udhibiti wa serikali *(control goods).*

Katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhan bidhaa hizi *(control goods)* hupewa msamaha huo wa kodi kwa asilimia zero pamoja na kutoa msamaha wa kodi kwa bidhaa ya tende ambayo huwa na matumizi makubwa kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Kwa hivyo, basi kwa kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramdhani bidhaa za Mchele, Unga wa Ngano, Sukari na Tende zinatarajia kuuzwa kwa bei ya kawaida, na Wizara ya Biashara iliendelea na kazi zake za ukaguzi wa bei kwa bidhaa hizi muhimu ili kuhakikisha kuwa bei zinabaki kuwa nafuu. Wizara inaomba ushirikiano na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, kupitia Masheha kusimamia bei hizi elekezi, ili manufaa yalokusudiwa katika msamaha wa kodi kuwafaidisha wananchi wa Zanzibar.

(b) Kutokana na umuhimu wa msamaha wa kodi kwa bidhaa muhimu za chakula (mchele, sukari, unga wa ngano na tende) kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ambapo matumizi ya bidhaa hizo yanakuwa ya kiwango cha juu, Wizara ya Biashara na Viwanda ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imendelea na utaratibu wake wakusamehe msamaha wa kodi kwa bidhaa hizo ili kusaidia kupatikana bidhaa hizo kwa wingi. Aidha, kwa kuhakikisha lengo hilo Wizara ya Biashara na Viwanda kuweka bei elekezi kwa wafanyabiashara kwa madhumuni ya kuhakikisha msamaha huo wa kodi uliotolewa unafikia lengo lililokusudiwa. unawafaidisha wananchi wa Zanzibar. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. waziri naomba kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. waziri kwa kuwa wananchi wa nchi hii wakwezi na wakulima, hua wanategemea sana unapotoka msamaha huu na wao wapate unafuu kwa mwezi mtukufu wa Ramadhan. Je, nikuulize kabla ya kuingia Ramadhani mchele, sukari na unga wa ngano, ulikuwa unauzwa bei gani na baada ya kuingia Ramadhani unauzwaje.

(b) Mhe. Mwenyekiti, hivi karibu tumemsikia Mhe. Waziri akitoa bei elekezi za unga wa ngano, sukari na mchele. Je, bei hizo zinafuatwa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mussa Foum Mussa swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mhe. Mussa Foum Mussa na wawakilishi wote humu ndani kuipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayongonzwa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuleta Mswada humu ndani wa Sheria Nam. 5 mwaka 2108 iliyokuja na Sheria ya Kuunda Tume ya Ushindani Halali na Kumlinda Mtumiaji.

Mhe. Mweyekiti, tume ile tayari keshateuliwa Mkurugenzi Mtendaji anashughulikia masuala mazima ya usimamizi wa bei wa nchi hii.

Mhe, Mwenyekiti, je bei ilikuwa kiasi gani kabla ya Ramadhani na baada ya Ramadhani bidhaa zinauzwa kiasi gani. Mhe. Mwenyekiti, tarehe 15 Mwezi huu wa 5 Mhe. Waziri Biashara na Viwanda, Wizara ya Biashara ilifanya *Press Conference* ya kuhakikisha kwamba, baada ya msamaha wa kodi uliotolewa tarehe 10/5/2018 kuhakikisha bidhaa muhimu tende, unga na sukari zinauzwa kwa bei nafuu.

Mhe. Mwenyekiti, katika *Press conference* tuliwaomba Masheha, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, kuhakiksha wanasimamia bei hizo. Vile vile, tulitoa *hot line,* kama bei zimepanda tupigiwe lakini mpaka asubuhi ya tunaandoka ofisini hakuna mtu yoyote aliopiga simu kwamba bei zimepanda.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumwambia Mwakilishi, kwamba Wizara ya Biashara na Viwanda imejipanga na imejidhatiti kwa dhati kuhakikisha tunalinda bei hizi zisipande na watu wetu wapo uwanjani kila dakika kila saa, kama kuna mtu yeyote ana *complained* zidi ya upandaji wa bei atuletee *official* tuko tayari ku-*act.*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, jibu la kwanza hujamjibu la bei aliyotaka. Mhe. Waziri, kwa majibu ya nyongeza. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana kwa majibu mazuri sana aliyotoa na ni majibu sahihi kabisa aliyoyatoa.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Mhe. Mussa Foum Mussa naomba nitoe elimu kidogo kwa sababu, kwa kipindi kirefu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatoa msamaha kwa vyakula hivi 3 hapa Zanzibar. Vyakula hivi vinalipiwa 10% ya kodi zake, lakini kama ingelikuwa ilipiwe hivi mia juu ya mia ingekuwa ilipiwe 25% kama wanavyolipa sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, huu msamaha kwa ajili ya mwezi Mtukufu wa Ramadhan ni msamaha maalum kwa kipindi kifupi, nacho ni kipindi cha mwezi mmoja mpaka tarehe 10 Juni, 2018, msamaha huu unakwisha. Lakini hapo nyuma kabla ya msamaha huu, bei za vyakula hivi, kwa mfano,bei ya mchele, bei ya sukari, bei ya unga ngano, kama sukari, sukari bei yake ilikuwa isizidi shs.18,000/= kwa sababu kwa gunia la sukari kwa hapa Zanzibar, tulikuwa tunakubaliana mpaka lifike shs. 70,000/=, kwa upande wa mchele kunatafautiana, mchele wa Mbeya bei zake

ni ghali kwa sababu ya usafirishaji kutoka Bara kuja hapa, kwa mchele wa mapembe tumesema bei yake isipindukie shs.2,100/= ambapo watu wengi ndio wanatumia mchele huo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya *exemption* tulikuwa tunategemea kwamba bei tulizozitoa bei elekezi ambazo hazikutautiana sana na bei zilizokuwepo hapo nyuma, utaweza kuwa na bei ambazo za vyakula, watu wataridhika na kuweza kununua, na mpaka sasa hivi hatujaona hitilafu yoyote kwamba bei imepanda kupidukia viwango tulivyoviweka. Maana ya bei elekeza kwamba tunasema unaweza kuuza chini ya shs. 2,100/-, lakini huwezi kuuza chakula chako kwa mfano mchele wa mapembe zaidi ya shs. 2,100/=. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mh. Masoud Abrahman Masoud: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa uteuzi alioupata. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, swali lipo pale pale, mchele wa mapembe kabla ya mwezi wa Ramadhani ulikuwa unauzwa shilingi 54,000/=, lakini sasa hivi unauzwa shs. 62,000/=, kwa sababu Mhe. Naibu Waziri ni mtetezi wa wakwezi na wakulima. Kwa hiyo, naomba atwambie hatua gani serikali iliyochukua ya kuwadhibiti wafanyabiasha wanaouza mchele 62,000/-. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na nampongeza sana Mhe. Masoud Abrahman Masoud kwa kuwatetea wananchi ambao ni wakwezi na wakulima. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimtoe wasiwasi, kwamba nakushukuru sana kwa suala lako naomba tulichukue na kulifanyia kazi, lakini na wewe ushichoke kutuletea *complain* kwamba mtu gani, duka fulani, pahala fulani. Serikali imetoa bei elekezi, bei lakini duka la Mzee Juma au la Mzee Ali hafuati matakwa ya serikali. Sisi tutaweza kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, Ahsante kwa kuniona na mimi ukaweza kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyo mfahamu Mhe. Waziri kwenye majibu yake mama kwamba msamaha wa kodi unatolewa kwa wafanyabiashara wanaoingiza biashara za unga wa ngano, sukari, na tende na mchele. Lakini kama tunavyofahamu ndani ya nchi yetu hii ndani ya Zanzibar yetu hii pia tuna kiwanda cha sukari ambacho kipo Mahonda na kinafanya kazi zake hizi.

Je, kuna utaratibu wanaofanya katika huu msamaha ambao wanautoa kwa wafanyakazi wanaoingiza.

Je, wizara hawaoni kwamba wanakikwaza kile Kiwanda chetu cha Sukari ambacho kinazalisha sukari hapa hapa na ni hasara gani inayopatikana kwa huu msamaha ambao unaotolewa kwa wafanyabiashara wanaoingiza na hasara inayotokana na ndani ya kiwanda chetu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii ya kumpongeza sana Mhe. Hidaya Ali Makame kwa kuonesha kushirikiana na serikali katika kuendeleza Sera ya Viwanda Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tunacho Kiwanda cha Sukari Mahonda, kiwanda chenye historia kubwa Zanzibar na ni kweli wafanyabiashara wanaingiza sukari. Lakini, nata nikutoe wasi wasi, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko jambo hilo linalijua na ndio yenye mamlaka ya kusimamia viwanda Zanzibar. Kwa hivyo, suala hili tutalifanyia kazi kwa karibu sana na tunakuomba usubiri maneno yake na mambo utaanza kuyasikia kwenye bajeti yetu. Nakuomba sana utegemee mema na mazuri katika kukilinda kiwanda chetu cha Mahonda Ahsante.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umemaliza, lakini kuna tangazo mbele yangu hapa kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, anawatangazia Wajumbe wa kamati hiyo baada ya maswali na majibu kukutana katika ukumbi au chumba cha mkutano. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nasimama kwa kutumia kanuni ya 46 (1), halkadhika kwa kutumia Sheria ya Nam. 4 ya mwaka 2007, na ikazia kwa kutumia kifungu cha Katiba cha 45 (3) pamoja na Nam. 2 cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wiki ya mwanzo ya Baraza la Wawakilishi tulipoanza nilizungumza kwa kutumia Kanuni ya 42 baada ya kipindi cha maswali na majibu, kuzunguzia juu ya suala zima la watoto au vijana waliokuwa chini ya umri wanaotumia pasola, au vyombo vya moto vy maringi 2 bila ya kufata utaratibu wa kisheria, na ili katika kuokoa muda niliomba kwamba serikali ilipokee hili halafu lifanyiwe kazi na tupatiwe majibu, ni jambo lipi ambalo wamelifanyia kazi lakini hadi leo tangu wiki ya mwanzo bado sijapata majibu yoyote au mnong'ono wa aina yoyote kutoka serikalini. Kwa hivyo, nilitaka nipate kujua kwanza ni hatua zipi za kisheria zimechukuliwa juu ya watoto hawa wanaotumia vyombo vya moto ambayo wako chini ya umri.

Halikadhalika siku ya tarehe 15/05/2018 katika swali langu la msingi Mhe. Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutumia Kanuni yetu ya 40(4) aliahidi kwamba atanipatia majibu ya usahihi kwa maandishi. Swali langu lilikuwa ni kujua idadi gani ya wachumi kwa upande wa Zanzibar wamependekezwa na SMZ katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao watawakilisha Tanzania kwa upande wa Zanzibar.

Sasa majibu haya mawili nilikuwa naomba kwamba umeshapita muda mrefu zaidi ya wiki na zaidi na sijapata majibu yoyote. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ni kaka yangu Mhe. Mohamed Aboud Mohamed anipe majibu kidogo ili nipate kujua ni muda gani tunauhitaji kwa upande wa serikali. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, serikali imesikia na Mhe. Waziri yuko tayari kujibu swali lako.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, aidha nimshukuru Mhe. Simai Mohamed Said kwa maelezo yake. Kwanza nimtanabahishe Mhe. Mjumbe kwamba Baraza linaendelea kikao chetu hakijamalizika kwa hivyo, majibu yake atayapata katika muda huu ambao Baraza linaendelea na atayapata kwa kina. *(Makofi)*

Kuhusu suala la watoto, vijana wanaopanda *pasola* utaratibu wa kisheria upo, Sheria ya Usalama wa Barabarani, wasimamizi wa sheria wakiongozwa na Jeshi la Polisi wapo, kinachotakiwa ni kutekelezwa kwa sheria. Mhe. Mwenyekiti, alichokieleza siku ile Mhe. Mwakilishi alitaka utekelezaji wa sheria uchukue nafasi yake. Mhe. Mwenyekiti, kupitia Baraza hili tukufu, nawaagiza Askari wa Polisi kuchukua hatua zote za sheria, ili Sheria ya Usalama Barabarani itekelezwe na wale wote wanaovunja sheria sio usalama barabarani tu, yeyote yule anayevunja sheria hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. Kwa hivyo, natoa wito kwa askari wafuate utaratibu ili kutekeleza wajibu wao. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na mjadala wa kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto na mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma akifuatiwa na Mhe. Mwanaidi Kassim na Mhe. Amina Idd Mabrouk ajitayarishe.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii lakini pia niwashukuru waziri na watendaji wake wote katika wizara hii, pia niwape pole kwa kazi ngumu ambazo zimo katika wizara yao.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii niseme pia ni wizara ya wanawake na nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuona ipo haja ya wizara hii kuiweka ili wawemo na wanawake waweze kupeleka kilio chao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi kama sikosei Mhe. Mjumbe mmoja hapa alizungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusiana na wawakilishi ambao wamo humu kwamba wengine wamechaguliwa na wa majimbo. Mimi ni mwakilishi mwanamke kupitia jimbo, lakini naumwa sana na wanawake wote pia waliochaguliwa humu kupitia makundi tofauti. Mhe. Mwenyekiti, wanawake wale wamepigiwa kura katika makundi yao lakini bahati nzuri Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili alilitolea ufafanuzi vizuri namshukuru sana.

Sasa nije katika kitabu moja kwa moja mchango wangu nataka nijikite katika suala zima la programu ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, nimekipitia hiki kitabu ukurasa nambari saba. Mhe. Programu ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji wanasema kuwa Mfuko wa

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi una jukumu la kutoa mahitaji na huduma nyengine za kifedha zenye masharti nafuu kwa wananchi wenye kipato kidogo kutokana na maeneo yote ya Zanzibar, ili waweze kuzalisha mali kwa kujiajiri na kupunguza umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, hii programu ni nzuri sana, lakini katika *bullet* ya (iii) wamesema kuwa imetoa mafunzo kwa wakopaji 1,702, wanawake 983 na wanaume 719. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi wa fedha, mbinu za kubuni miradi mipya, utayarishaji wa mipango ya biashara, misingi ya kilimo bora, uvunaji na utunzaji wa mazao. Niwapongeze kwa mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika programu hiyo bado nimeona kuwa mara nyingi katika maelezo ya Mhe. Waziri tunaona kuwa imesimamisha na kusajili vyama, imetekeleza zoezi, imeimarisha utendaji wa vijana, imetoa mafunzo, yaani imeimarisha uwezo wa kiutendaji. Kwa kweli, naomba tu kuitanabahisha wizara hii, hii ni bajeti inayozingatia matokeo, sasa kama ni kama ni bajeti inayozingatia matokeo niko hapa, tayari wameimarisha, wamesimamia, wamefanya kila kitu nasema tena niwapongeze kwa hilo. Lakini nataka kujua nini faida yake au yale matokeo kwa kuzingatia hii programu ambayo tunasema inazingatia matokeo, hivyo nataka nijue imeendeleza, imefuatilia matokeo yake yakoje katika ule ufuatiliaji wake.

Tumeona humu wameeleza hivyo, lakini pia katika hizo *SACCOS* na usimamizi na uimarishaji wa vyama vya ushirika kuna *SACCOS* mbali mbali ambazo wameziimarisha, wameendeleza kufuatilia, wamefanya yote hayo. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nataka kujua hilo kwamba matokeo yake yakoje baada ya ufuatiliaji, baada ya tathmini, baada ya utekelezaji matokeo yake yakoje, kwa sababu hii ni programu inayowezesha wananchi kiuchumi na wananchi hawa kama watawezeshwa kiuchumi kwa mujibu wa maelezo ya hiki kitabu basi nina imani umasikini utatoweka au umetoweka, lakini kama wakituandikia tu kuwa imesimamia upatikanaji, umesimamia maelekezo, umetoa mafunzo hatujapata yale matokeo yake basi nahisi bado tutabaki kule kule kwenye ule umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, katika wizara hii na katika kila takwimu iliooneshwa humu vikundi vilivyosajiliwa wameainisha wanawake wangapi na wanaume wangapi na katika takwimu hizi wanawake ndiyo wengi. Na wanawake ndio wenye matatizo mengi na wanawake ndio walezi wa familia.

Mhe. Mwenyekiti, kama itakuwa tumeainisha tu kwa maneno sifikirii kama ule umasikini utaondoka. katika programu hiyo hiyo ndogo ya usimamizi na uimarishaji wa vyama vya ushirika nimeona kuwa katika kifungu namba 18. Mhe. Mwenyekiti, amesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2018 programu ya usimamizi na uimarishaji wa vyama vya ushirika imepanga kusajili vyama vya ushirika 300, lakini kuna malalamiko katika hivi vyama vya ushirika wanasajili tunashukuru sana na kama wamejipangia kusajili hivyo basi mimi niwapongeze.

Mhe. Mwenyekiti, Lakini ule usajili wanaofanywa zile kumbukumbu zake inawezekana au inaonekana kuwa hazipo. Vyama vingi vya ushirika havina muendelezo vinabadilika kila wakati sasa sijui ni vyama vipi vya ushirika ambavyo bado vinaendelea na vimekaa vizuri na vinafanya kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika Programu ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi amesema Mhe. Waziri katika hotuba yake, wizara ilifanya ziara ya mafunzo *SIDO* Dar-es-Salaam kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na shughuli za usindikaji wa vyakula, watengenezaji wa sabubuni pamoja na baadhi ya mashine zinazotumika kutengeneza bidhaa hizo. Wajasiriamali hao walikuwa 15 Unguja na Pemba walishiriki katika ziara hiyo, Mhe. Mwenyekiti imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana.

Lakini bado naiomba wizara kwa nini waende *SIDO* Dar-es-Salaam, na wakachukua wajasiriamali 15 hawa kidogo, lakini Kizimbani yupo mtaalamu pale wa kusindika vyakula badala ya kwenda Dar-es-Salaam basi wangemtumia huyu wa hapa. Kwa hivyo, kama walichukua wajasiriamali 15 tukiunganisha pengine na usafiri, tukiunganisha na malipo yale ya kwenda kule basi nadhani wajasiriamali 30 kama tungemtumia huyu mtaalamu aliyekuwepo Kizimbani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naiomba sana wizara wazingatie hata wale wataalamu waliokuwepo ndani ya Zanzibar kuwatumia, ili tupate wajasiriamali wengi ambao wamepata yale mafunzo.

Mhe.Mwenyekiti, nije katika programu ya masuala ya usawa wa kijinsia na uendelezaji wa wanawake. Katika zile *bullets* Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu:

> "Kwa mwaka wa fedha 2017/18 program imetekeleza yafuatayo:-
>
> Imehamasisha wanawake kuimarisha vikundi vya Ujasiriamali ambapo vikundi 122, Unguja 17 na 105 Pemba vilifanyiwa ufatiliaji na tathmini ya vikundi hivyo."

Mhe. Mwenyekiti, narudi tena kwenye swali lile lile wamefanya ufatiliaji wamefanya tathmini nini matokeo yake.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile imeadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tarehe 08/03 Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa ni "Wakati Umefika Tushirikiane Kuleta Mabadiliko ya Wanawake Vijijini". Mhe. Mwenyekiti, ujumbe huu kama wizara wameuchukua kwa vitendo ni ujumbe mzuri sana au ni mabango tu yamewekwa kwa ajili tu ya kutangaza kuwa wakati umefika tushirikiane kuleta mabadiliko ya wanawake vijijini, basi sifikirii kama tutafika pahala.

Mhe. Mwenyekiti, tunayo Sheria ya Ardhi Namba 12 ya mwaka 1992 kifungu cha 45 kimeweka utaratibu wa umilikaji wa ardhi na katika umilikaji huo kuna zile heka 3 ambazo zilitolewa na Mhe. Rais wa Kwanza wa Zanzibar Mhe. Abeid Amani Karume Mwenyezi Mungu amrehemu alipo. Mhe. Mwenyekiti, taratibu hizi si za urithi kama tutafata taratibu za kurithisha, ili mwanamke aweze kurithi siyo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi anapomiliki heka tatu mwanamme au mume akiondoka duniani kwa mujibu wa taratibu hizi basi mmiliki pale ni mwanamke ambaye ni mke ingelikuwa kama ni masuala ya urithi tungesema zingekwenda kwa taratibu za urithi kwa dini, lakini hii umiliki tayari hii sheria ipo. Sasa nataka niiulize wizara labda wamewahamasisha vipi wanawake kuweza kujua sheria zile ambazo zinawagusa wanawake moja kwa moja katika kutekeleza au

kutetea maslahi yao wakiwa ni wanawake nataka nilijue hilo. Lakini wakisema tu imefanya mikutano imehamasisha, imefanyaje lakini je, wamejipanga vipi katika kutoa yaani kisheria mwanamke anaposimama akitetea haki zake ajue anasimama kwa sheria. Mhe. Mwenyekiti, wanawake wengi hawajui na hii ndio wizara ya wanawake wawape mafunzo kama haya Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, katika programu hiyo hiyo kuna Programu ya pili ndogo Programu ya Mapambano dhidi ya Uzalilishaji ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, wameunda kamati tofauti, programu hii ina lengo la kukuza kuitikia kuratibu mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake nchini.

Mhe. Mwenyekiti, imefanya uzinduzi wa mpango kazi imeimarisha utekelezaji lakini Waheshimiwa tumepitisha sheria, sheria ile imesainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar tunampongeza sana kwa sababu ilikuwa ndio kilio cha wanawake wengi au watu wote wa Tanzania hii au Wazanzibari kuhusiana na masuala ya udhalilishaji. Lakini, bado nina wasi wasi na wasi wasi wangu tayari Serikali Kuu imeshatimiza wajibu wake Baraza la Wawakilishi limetimiza wajibu wake, nawashukuru katika *bullet* yao ya kwanza, pili, tatu na nne kuna kamati ishirini na nne kupinga ukatili wa udhalilishaji ambazo zimejengewa uwezo juu ya dhana ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, wamejengewa uwezo kamati hizo na wizara nipongeze.

Lakini, bado Mhe. Mwenyekiti bado haya masuala yapo na yanaendelea. Mhe. Mwenyekiti, juzi tu Wilaya ya Kati kuna mtoto wa kike masikini kakutwa amekufa kama wizara na matukio bado yanaendelea je, wao wanawashirikishaje masheha. Mhe. Mwenyekiti, kuunda kamati si tatizo tunaweza tukawa na kamati nyingi lakini ufatiliaji wake ukoje.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana au naiomba sana wizara hii pamoja na kuunda kamati nyingi basi wafate zile Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, Serikali za Mitaa sasa hivi zinafanyakazi kisheria. Kwa hiyo, wawe karibu na masheha najua wapo karibu nao, lakini waziri kuwa karibu nao kwa sababu masheha ndio wanaojua mtaani kwao kuna kitu gani na kuna mtu na kitu gani. Kwa hiyo, wawekee hata ulinzi wakipata zile taarifa kwa sababu unakuta watu wengi wanahofia na kuogopa. Inawezekana jirani kafanya kitu kibaya au kafanya kitu cha uzalilishaji lakini ile kufichiana na kuogopana. Kwa hiyo, naomba sana watumie masheha lakini kupitia na ulinzi pia wakae nao katika mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika programu hii imetengewa fedha. Programu ya Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhalilishaji kiambatanisho namba moja 2017/2018. Makadirio ilikuwa milioni mia moja na hamsini lakini walipata milioni mia moja na thalathini na sita sawa na asilimia tisini.

Mhe. Mwenyekiti, asilimia tisini ni kubwa kwa kiasi, lakini kiambatanisho namba 12 ukurasa wa 61 kuna kifungu kile Q010201 Mapambano Dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, makadirio yamekuwa ni bilioni moja kama sikosei nukta saba. Kwa kweli, nina wasi wasi Mhe. Mwenyekiti, kwamba 2017/2018 walikuwa wamejipangia kupata milioni mia moja. Lakini kipindi hiki ni bilioni mia moja nukta saba.

Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atueleze wizara kwa nini mwaka huu wa fedha zimeongezeka au zimekuwa nyingi kwa sababu gani, na pili ni kasoro gani zilizojitokeza katika mwaka uliopita mpaka wakaona kuwa fedha zile walizokadiria na walizozipata zikawa kidogo mpaka wakafikia kuomba bilioni moja nukta saba. Mhe. Mwenyekiti, waje watupe ufafanuzi nawaomba sana na natumai Wawakilishi wote wakipata ufafanuzi wa hili basi nina imani hii hoja itaungwa mkono vizuri sana kwa sababu mna wanawake, mna watoto katika wizara hii ili watimize ule utekeleza wao.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia sasa nije katika suala zima la hii Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango na Sera, kuna taasisi mbali mbali ambazo zinaajiri watu. Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yake nimeona kuwa bado kuna migogoro na hasa katika upandishaji wa mishahara. Kwa kweli bado migogoro ipo na sisi ni Wawakilishi wa wananchi wanatwambia katika zile taasisi ambazo wanazifanyia kazi. Taasisi ya kwanza Upendo na nadhanni malalamiko yao yeshakwenda. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuambie taasisi hii wamefikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna malalamiko mengine kuna taasisi ya UMAWA nayo pia wanalalamikiwa sana kuhusiana na upandishaji wa mishahara japo kuwa katika kitabu chake nimeona kanuni za taasisi ambazo haziwezi kulipa kima cha chini cha mshahara kupitia Mhe. Rais kama alivyotangaza lakini wameweka kanuni. Kwa hiyo, nataka kujua ni taasisi gani au vigezo gani walivyovitumia ili kwa kutunga hiyo kanuni kuwa na taasisi hii ina uwezo wa kulipa hivi na taasisi hii inaweza kulipa hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia napenda sana kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Chukwani kwa kunichagua mimi niwe Mwakilishi wao. Jengine la mwisho katika uimarishaji wa vyama vya ushirika nimesahahau hilo muhimu kuna mitandao ya kifedha ambayo wamewaunganisha nayo wajasiriamali wale. Kwa kweli, nataka kujua tu labda watawasaidiaje kwa sababu hii mitandao ya kifedha ina masharti magumu saa nyingine kikundi hakiwezi kupata pesa kama hakina pengine eneo kuweka lakini pia na riba ni kubwa, lakini nataka nijue labda wanawasaidiaje wale wajasiriamali katika hii mitandao ya kifedha baada ya kuwaunganisha.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba nitoe mapendekezo yangu kwa wizara hii, waone kwamba au serikali ione kwamba sasa ipo haja ya kuweka ile Benki ya Wanawake, ili wanawake wanapokuwa na vikundi vyao basi tayari wawe na benki yao kwa uhakika. Mhe. Mwenyekiti, inawezekana *PBZ* imetoa Tawi la *Islamic Bank*, kwa nini *PBZ* hii serikali isiishauri au serikali ikaweka hiyo benki ya wanawake. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwa mchango ambao umewasilisha, sasa naomba nimwite Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa akifuatiwa na Mhe. Amina Iddi Mabrouk

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto ya mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya katika Baraza hili tukufu. Pia nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jinsi anavyotuletea maendeleo katika nchi yetu na pia namuombea kwa yale ambayo kayapanga ayatekeleze Mwenyezi Mungu amjaalie ayafanikishe kadri ya uwezo wake. Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake kwa umahiri na kusema kweli tumeifahamu vizuri sana. Nikiendelea nimpongeze Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote katika wizara hii kwa mashirikiano yao wanayotoa ili kuona tunapata hotuba iliyokuwa mahiri. Pia pongezi za dhati ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali pamoja na Wajumbe wake kwa kutusomea taarifa yao ambayo ipo sahihi na haijaficha kitu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nachangia katika kitabu hiki moja kwa moja, nianze katika suala la Soko la Jumapili la Muembekisonge ambalo limewajumuisha jumla ya wajasiriamali 40.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli niipongeze wizara kwa jitihada yao iliyochukua, lakini pia naiomba wizara bado ijitahidi kuhusu masoko haya ya wajasiriamali wetu. Kwa kweli wajasiriamali wetu hawa wanajitahidi sana katika kutafuta bidhaa zao tatizo masoko. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi baada ya Soko hili la Jumapili la Muembekisonge namuomba, basi wafanye kwa makusudi au jitihada za makusudi kuona kwamba wanakwenda katika maeneo mengine ya ndani na nje ya Zanzibar, ili kuona wajasiriamali hawa wanaondokana na tatizo hili la kiuchumi, kwa sababu hapa katuandikia wajasiriamali 40 lakini tunaamini kwamba tuna wajasiriamali wengi katika nchi yetu. Kwa hiyo, namuomba achukue jitihada za makusudi kuona wajasiriamali wetu hawa wanapatiwa masoko ya ndani na nje.

Mhe. Mwenyekiti, nimetaka kulisemea hili kwa sababu wajasiriamali wengi ni wanawake na hii ndio wizara yetu ya wanawake kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri pamoja na kazi zote walizokuwa nazo basi washirikiane na Mhe.Waziri wa Biashara wakae pamoja waweze kutafuta masoko, ili kuwaokoa akina mama hawa ambao wao ndiyo uti wa mgongo katika familia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu pia niipongeze wizara kwa kusimamia Kituo hiki cha Kutengenezea Vifaa vya Kutumia Umeme wa Jua kilichopo Kibokwa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kwa kweli, katika kituo hiki mimi nimefika nilipokuwa Mjumbe wa Kamati ni kweli kipo na jitihada zao nimeziona wizara na hapa pia wametuandikia katika kitabu chao hiki cha bajeti kwamba kulikuwa kuna wakulima 13 tayari wameshawalipa fidia na tayari eneo hilo lipo katika kituo hiki. Kwa hiyo, nawapongeza sana waongeze jitihada na wakulima hawa nawapongeza sana kupisha serikali ili kuona kituo chetu hiki kinabakia na kinazidi kuendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nije katika suala la wazee, naipongeza sana wizara kwa jitihada inayochukua ya kuwahudumia wazee wetu, ni kweli mimi Limbani, Welezo na Sebleni kote nimefika, hivi sasa kusema kweli wazee wetu wapo katika maeneo mazuri sana wanakula kwa wakati, wanapata mahitaji yao kwa wakati na pia katika taarifa yao wametwambia kwamba wamepatiwa gari. Kwa hivyo, naipongeza sana wizara kwa kazi zao nzuri wanazozifanya ni kweli kipindi kilichopita nilikuwa katika kamati hii miaka mitano ni kweli mafanikio yanapatikana, kwa hivyo naiomba wizara izidishe jitihada katika masuala haya ya wazee

isiwaache nyuma iongeze nguvu iwalee wazee wetu. Kwa kweli, nyuma tulikotoka kulikuwa kuna changamoto nyingi lakini sasa hivi tunashukuru changamoto hizi zimetatuka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, nije katika suala la udhalilishaji kama Waheshimiwa Wajumbe wengi wamegusia suala hili la udhalilishaji na mimi pia niungane nao niipongeze hatua ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutia saini muswada wa Sheria ya adhabu na Sheria ya Mwenendo wa Jinai.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sheria hii tayari imeshatiwa saini tunashukuru baada ya malalamiko mengi ya wananchi kwamba sheria iliyokuwepo ilikuwa haina meno, sasa hii sheria iliyokuwepo ni nzuri inahitaji utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, sheria nyingi tunapitisha Barazani lakini utekelezaji wake ni mgumu, sheria tumeipitisha ishatiwa saini nawaomba wanaohusika na kuitekeleza sheria hii waitekeleze kwa uadilifu. Kwa kweli, naipongeza wizara kwa jitihada inazochukua wizara inachukua jitihada mpaka inapofika hatua ya wao wanapohusika lakini mbele wao kama wizara hawahusiki, mimi ninaiomba wizara iamue kwa makusudi baada ya hatua hizo wanazochukua za kuwasimamia wanawake na wale wanaodhalilishwa ili kufika katika vyombo vya sheria ihakikishe inatoa elimu bado wanawake ndiyo ambao tuna kilio kikubwa sana kuhusiana na suala hili la udhalilishaji na kina baba wapo lakini wanawake ndiyo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri suala hili lazima kutolewe elimu kwa wananchi, wananchi wako tayari na wanajua kama kuna sheria hii ishapitishwa na ishatiwa saini lakini bado wana hofu utekelezaji wake. Kwa hivyo, elimu hii ikiwafikia ili wawe na imani kwa sababu wanawake wameondoa imani kutokana na usumbufu wanaoupata katika mahakama, lakini mkitoa elimu kwa wananchi na nyinyi mkiwa mmewasimamia naamini matatizo haya yatamalizika au yataongezeka, kwa sababu mimi ni Mwakilishi wa Wanawake katika Mkoa wa Magharibi tayari niliwahi kufanya ziara nikaulizwa kuhusu sheria hii, lakini bado wanapata wasi wasi sheria itakuwepo lakini itatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma sheria ilikuwepo lakini tulikuwa tunaona changamoto zilokuwepo, wananchi hawapati haki zao kuanzia maeneo husika, kuanzia polisi na kwengine kunakohusika. Kwa hiyo, naiomba wizara hapo ambapo wanapohusika wao ambapo wanafanyia kazi wajitahidi naamini wanajitahidi, kwa sababu taarifa zao zinatueleza kwamba wao wanashughulikia mpaka katika mkono kwa mkono lakini tatizo baada ya kufika mahakamani wao wanakuwa hawawezi kufika kule, kwa hili tukiwa na mashirikiano naamini tutafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na wenzangu kuhusu pencheni, nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuliona suala hili ili kuwafariji wazee wetu waliotimia miaka 70 kwa kupata posho la shilingi 20,000. Kwa kweli, naiomba wizara pamoja na changamoto zilizokuwepo walisimamie suala hili kwa umakini ili kuona matatizo, changamoto na malalamiko yaliyokuwepo viondoke ili suala hili liende vizuri. Nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar sana kusema kweli hapa kafanya kitu kizuri sana na pia naomba awamu zitakazokuja na nyingine ziendeleze suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika Kamisheni ya Kazi, Sekta Binafsi. Mhe. pia niipongeze Wizara kwa hatua ambazo wamechukua katika sekta hizi binafsi lakini bado kuna changamoto. Kuna changamoto katika sekta hizi binafsi za mishahara bado halijakaa vizuri, lakini pia katika suala la kuwekewa mikataba vijana wetu. Malalamiko yapo kwa vijana wetu bado sekta hizi binafsi hawawafanyii haki, hawawatendei usawa kama sekta nyingine binafsi zilizokubali. Kwa hivyo, naiomba wizara yako ijitahidi na hili, iongeze nguvu ione suala hili na changamoto zilizokuwepo zinaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi kwa sababu wizara hii nilikuwa Mjumbe wa Kamati miaka 5 ya Baraza lililopita. Kwa hiyo, mengi yaliyotekelezwa naamini wamefanya kwa mashirikiano ndiyo maana kitabu hiki cha bajeti leo wametuwasilishia hakina changamoto nyingi, lakini changamoto kubwa zaidi ambayo waliyotwambia katika kitabu hiki cha wizara ni kuhusu majengo na vitendea kazi. Kutokana na hali hiyo, naiomba wizara ijitahidi ifanye kazi zake vizuri na pia changamoto hizi katika bajeti inayokuja tuone changamoto hizi zilizowakabili ziondoke japo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi mchango wangu nitafikia hapo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Magharibi naunga mkono asilimia mia moj. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa. Sasa namwita Mhe. Amina Iddi Mabrouk, akifuatiwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajitayarishe.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma muumba wa mbinu na ardhi na vyote vilivyokuwemo humu. Lakini pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti pia nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuteua uongozi wa juu katika wizara hii kuanzia Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wote wanawake. Hali hii inatokana na kwamba kuna umuhimu mkubwa katika wizara hii kuwepo wanawake, kwa sababu sisi wanawake ndio walezi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii ambayo imejieleza, imefafanua katika nyanja tofauti. Namuomba sana Mhe. Waziri aendelee kuchapa kazi pamoja na uongozi wake na sisi tumo humu kumuunga mkono. Baada ya maelezo au utanguzi huo naomba niingie katika kitabu ukurasa wa 15 nimpongeze sana Mhe. waziri kwa hotuba yake pia niipongeze sana wizara hii kwa kuona kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, uchumi ndio kila kitu, uchumi ndio uanaotufanya tuweze kuishi katika dunia hii. Kwa hivyo, nampongeza sana kwa kuwawezesha wananchi wetu, ili waweze kumudu maisha yao na familia zao. Pamoja na jitihada hizo bado hayaonekani maendeleo ya wananchi wetu, yaani bado hawaonekani kwamba wanafaidika na mchango huu wa wizara ambao wanawapatia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sababu kubwa inaonekana kwamba serikali na wizara kwa ujumla bado haijawa tayari kuwasaidia wananchi wetu hasa kina mama, mimi Mhe. Mwenyekiti natokea katika Mkoa wa Magharibi, na akinamama wengi ambao wajasiriamali, lakini wajasiriamali wale wanatengeneza bidhaa lakini matokeo yake hawapati soko si la nje wala la ndani katika nchi yetu. Kwa hiyo, naiomba sana serikali pamoja na kazi nzuri ambayo wanafanya kwa wananchi wetu hususan akinamama. Lakini, bado wanatakiwa wajipange kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata soko la ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano miye katika Mkoa wetu huu wa Magharibi tunao akinamama wengi ambao ni wajasiri amali, na pale inapokuwa matangazo ya biashara yanapotoka huwa wanakwenda sana Maisara, lakini wanapokwenda kule Maisara wanaweza wakakaa toka asubuhi wakashinda pale pale, lakini masoko yanaonekana sio makubwa kama wanavyotarajia.

Kwa hiyo, naiomba sana wizara waangalie masoko ya ndani ya na nje. Mhe. Mwenyekiti, masoko ya ndani serikali kuhakikisha kwamba, wanayalinda ile bidhaa ambayo wanaizalisha, na kuilinda bidhaa ile inaonekana kwamba serikali itafute mbinu ione kwamba zile bidhaa za nje zinalindwa kwa kiasi fulani, ili zisiweze kuingia nchi yetu. Lakini sana hivi, ukenda masokoni utakuta bidhaa nyingi za nje zinaingia hapa kwetu Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, si kuingia tu katika nchi yetu lakini unakuta bidhaa ile ile ambayo ameitengeneza mjasiri amali wetu wa nchini, unakuta ile bei unakuta yule mjasiriamali wa kwetu bei yake kubwa kuliko yule ambaye bidhaa imetoka nje bei inakuwa kubwa sana. Mpaka mtu unajiuliza hii biashara kweli hii bidhaa imelipiwa kodi. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti serikali yetu ina kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba ile bidhaa ambayo inategenezwa kwetu, inapopelekwa nje kutafutia soko kwa sababu wajasiri amali wetu bado ni wachanga, hawawezi kutafuta soko nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine kulinda bidhaa yetu kama hatujalinda bidhaa yetu basi itakuwa ni sawa na *zero* wananchi kila siku, wizara itatengeneza mbinu mbali mbali ya kuwakwamuwa wananchi wetu kimaendelea lakini hatma yake maendeleo kwa wananchi wetu hayaonekani. Kutokana na hali hiyo, naiomba sana wizara izingatie na iyafanyie kazi shughuli zote na mwenendo mzima wa biashara za wajasiriamali wetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niingie katika ukurasa 31, nimeona katika kitabu hichi. Kwanza naipongeza wizara sana kwa kufanya utafiti ambao kujua nguvu kazi ya vijana tulionao, naamini kwamba utafiti huu utasaidia sana kwa taifa letu. Vile vile, naipongeze tena wizara kwa kuona kwamba utafiti wao umegundua tunao vijana karibu 500. Mhe. Mwenyekiti, ninesema kwamba vijana 500 ni wengi sana kwa taifa letu, na vijana hawa kama tutawatumia vizuri basi nnaamini kwamba nchi yetu itapiga hatua. Lakini pamoja na idadi hiyo Mhe. Mwenyekiti ambayo wizara imetowa lakini bado tuna vijana ambao wana fani tofauti katika vijana hawa 500.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa 500 ambao wana fani tofauti, lakini hatma yake ukipita mitaani unawakuta vijana wanazurura ovyo hawana kazi. Mhe. Mwenyekiti hili jambo lakusikitisha sana, tena ni hatari sana kwa taifa letu, kwa sababu vijana wale wanapokuwa hawana kazi maalum

wakazururа mitaani, matokeo yake wanajiingiza katika matendo yasiyostahiki, lakini pia wanajiingiza katika matendo ambayo kinyume na utamaduni wetu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo kubwa sana na malalamiko makubwa sana kwa vijana wetu, wako vijana wamesoma vizuri na kumaliza vyuo vikuu mbali mbali, lakini wako mitaani wamekosa ajira. Mhe. Mwenyekiti, wakati huo huo, kuna wafanyakazi ambao wamefikia umri wa kustaafu bado wako kazini, Mhe. Mwenyekiti hili jambo sio zuri, lakini utakapouliza utaambiwa hawa wana ujuzi maalum ndio maana bado wako kazini.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa tukiendelea kuwaweka mitaani, tukiwa hatuwapi fursa ya kwenda kufanya kazi, sasa huo ujuzi maalum wataujua wapi. Kwa hiyo, naiomba sana serikali vijana wetu tunao na wanaweza Mhe. Waziri nakuomba sana ulizingatie hili, kwa sababu nashukuru kwamba Naibu Waziri kwa kiasi fulani bado ni kijana, kwa hivyo vijana wanaotembea mitaani tu, akiwa hana kazi maalum hili jambo linasikitisha. Vile vile, kwa wale wazee ambao tayari wameshafikia umri wa kustaafu basi wapewe haki yao, wamepe kiinua mgongo chao, ili waende wakafanye shughuli nyengine sio kuendelea kuwaongezea tu miaka makazini, hili jambo Mhe. Waziri, Mhe. Mwenyekiti sio zuri kwa serikali yetu.

Nikiendelea na machango wangu nije katika Programu ya Uratibu wa Masuala ya Usawa na Kijinsia na Uendelezaji wa Wanawake, lakini mchango wangu nitaendeleza na Programu ndogo ya Mapambano dhidi ya Udhalilishaji na Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, suala la udhalilishaji limekuwa kubwa katika nchi yetu, kama utakuwa unasikiliza kipindi cha Mawiyo kila siku asubuhi machozi yanaweza yakakutoka. Kwa kweli, kila kukicha kila siku aidha kuna matokeo mawili au matatu ya udhalilishaji, hasa watoto ambao umri kuanzia miaka minne na kuendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hili janga la kitaifa, yaani sio janga la Amina wala mwengine ni janga la kitaifa, pia sio janga la Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, isipokuwa ni janga la wananchi wa Zanzibar wote. Kwa hivyo, naamini kwamba kama tutashirikiana natumai litapungua, kwa sababu nafuatilia sana katika vyombo vya habari haioneshi kwamba hili jambo linapungua bali linaongezeka siku hadi siku. *(Makofi)*

Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kusaini ile Sheria ya Mwenendo wa Jinai Zanzibar na Sheria ya Adhabu, hii nnaamini kwamba kama tutalifanyia kazi kwa uwaminifu na uwadilifu mkubwa, basi masuala haya ya udhalilishaji yatapungua. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeona hapa kuwa imetengwa milioni bilioni 1.7 ya pesa ambazo zinatakiwa kutumika. Lakini kilichonishangaza Mhe. Mwenyekiti programu mbili zimechanganywa kwa wakati mmoja, kuna programu ya uratibu wa masuala ya usawa na jinsia na uwendelezaji wanawake, vile vile kuna programu ndogo ya mapambano dhidi ya udhalilishaji na wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sijategemea kwamba hizi programu zitachanganywa, kwa sababu nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti programu ya mapambano dhidi ya udhalilishaji inatosha kuwa programu moja, kwa sababu programu hii ya udhalilishaji hivi sasa ndio kilio kikubwa kwa nchi yetu ya Zanzibar, na hii programu hii inahitaji pesa za kutosha ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa

hiyo, programu hii pesa zake unapochanganya kwa pamoja sidhani kama ufanisi wake unaweza kuleta tija.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka kipindi kilichopita mwaka jana tuliidhinisha pesa karibu milioni mia tatu, lakini hesabu hapa naona katika kiambatanisho walipata karibu shilingi milioni mia mbili, lakini Mhe. Mwenyekiti kazi ambazo zilizofanywa hawajaonesha mafanikio yake, haiyaonesha jinsi gani tatizo hili la udhalilishaji limepungua katika nchi yetu, lakini leo katika kitabu hichi wameomba pesa karibu bilioni 1.7 ili waweze kufanikisha programu hii.

Kwa kweli, Mhe. Mwenyekiti mwaka jana na mwaka huu, pesa imeenda mbali sana. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri katika hili atakapokuja kufanya majumuisho basi atueleze tufahamu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba programu hii bilioni 1.7 wana mikakati gani kuhakikisha kwamba suala zima la udhalilishaji litapunguwa kwa kiasi kikubwa kwa nchi yetu.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti atakapokuja Mhe. Waziri atwambie kwamba Programu ya Mapambano dhidi ya Udhalilishaji wametenga kiasi gani, pia Programu ya Uratibu wa Masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uendelezaji Wanawake wamepanga kutumia kiasi gani. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unapoona hivi tu kidogo tu inatupa mashaka hatufahamu, hasa ukizingatia kipindi kilichopita wameeleza tu, lakini hawajutueleza kwa undani suala hili limepungua kiasi gani, na matokeo yake linaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa wa 41, nizungumzie juu ya usimamizi na usalama wa afya kazini. Naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuona kwamba ipo haja lakini pia juhudi mbali mbali wanazifanya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanakuwa salama katika makazini kwao. Kwa kweli, tunafahamu sote kama kazi nyingi zinakuwa hatarishi hasa kazi za ujenzi, kazi za umeme kazi hizi zote zinakuwa zinamahatarishi yake katika maeneo yao ya kazi, lakini Mhe. Mwenyekiti hawajatwambia kwamba wanakuwa wanatembea kila baada muda gani kuhakikisha kwamba hayo maeneo ya kazi yanakuwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sote tunafahamu kuna wafanyakazi wengine huwa wana ukaidi, jana Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa natoka nyumbani nakuja Barazani nikakuta gari la taka linachukua taka, kwa bahati gari lile linawanaume isipokuwa mwanamke mmoja, lakini nilichosikitika ni kwamba mwanamke yule yule ndiye ambaye hajavaa *mask* wale wengine wote wamevaa *mask,* sasa Mhe. Mwenyekiti nikamuuliza mbona hujavaa *mask* akasema yeye haipendi. Kwa hiyo, Mhe. Waziri hayo pia ni mambo ya msingi kuhakikisha kwamba makazini kwetu yanakuwa salama, lakini pia wafanyakazi wetu wanafata taratibu ambazo wamejiwekea.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nimuombe sana Mhe. Waziri yale ambayo nimeyachangia, basi aje kunijibu kwa ufasaha lakini zaidi hizi pesa aje anieleza nifahamu ili niweze kuunga mkono hoja yake kwa asilimia 100, lakini hivi sasa naunga mkono hoja hii kwa 95. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Mjumbe. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan na Mhe. Simai Mohammed Said ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa ya kuchangia machache katika Hotuba yetu hii ya Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimsifu waziri kwa kitabu chake ambacho kwa hatua moja ama jengine amekichambua katika hali ya utafiti aloufanya, hata mimi mwenyewe nimeukubali sana, nimshukuru sana amechambua mambo mengi, yeye kama binaadamu amejitahidi ili kueleza hali halisi ambayo katika wizara yake mambo ambayo mengine ni faida mengine ni changamoto sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaenda katika mambo mengine katika kitabu na mengine mambo ya jumla.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri kidogo atakapokuja aweze kunieleza kidogo utaratibu ambao ameufanya kuhusu kujitahidi na kufatilia mikopo yake ambayo ameitowa kwa wajasiri amali na jinsi ilivyofanikiwa kurudishwa, wakati tuna mikopo mingi ambayo ni ya wananchi vile vile, pamoja na vijana ambayo ni ya J.K na A.K hii imefeli au kwa upande mmoja fedha zake zimeishia mitini. Lakini nimshukuru Mhe. Waziri mtaji tuliompa bado anauwendeleza, niliona kwenye kitabu karibu asilimia tisini na ngapi unarudishwa kwa hivyo, si vibaya na sisi akatuelekeza katika mkopo wetu huu wa J.K na A.K umefikaje na yeye amefanikiwa vipi, ili tuweze na sisi katika mikopo yetu ambayo tunatowa isiweze ikawa inapotea bure. Mhe. Waziri hilo nikusifu maana yake katika kitabu chako umesema vizuri sana, na mimi naona nikuunge mkono sana.

Lakini, Mhe. Mwenyekiti pia nataka nizungumzie kitu kwamba naipongeza sana serikali, katika hali halisi ya kujitahidi kutunga sheria za udhalilishaji. Lakini Mhe. hili nafikiri inawezekana pamoja na mambo mengine ni sababu kubwa yako wewe peke yako au kwa wizara yako, kufuatilia kwa ukaribu sana mambo hayo na kuweza kuyamudu bila ya kuingia serikali kuu.

Haya mambo kama alivyosema Mhe. Amina Iddi Mabrouk ni jambo la kitaifa tukilijadili kuhusu wizara kama tutafutika mzigo ambao “punda afe lakini mzigo wa bwana ufike”. Kwa kweli, hivi sasa limekuwa si la wizara tena hili janga la kitaifa na serikali kuu ningeiomba iingilie kati kuisaidia sana wizara pamoja na kwamba ni wizara, lakini sijaliona mimi jeshi la wizara kwa hivyo wala vikosi vyengine vya wizara ambayo ya wanawake. Kwa kweli, wanawake mara nyingi wao kama wadau, wanaenda kujishajihisha na kuweza kuelezea lakini inaonekana tumefika pahala tumegonga ukuta, sasa lazima serikali ichukuwe mkondo wake kwa kuisaidia wizara. Ningeomba hili waziri, uje ulitolee ufafanuzi kama kutakuwa kuna haja ya kuweza kulisemea basi uje unieleze tunafikiaje, ili kuondoa au kulipunguza tatizo kubwa ambalo linaleta matatizo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la hawa watu waliokamatwa au waliopelekwa katika vyombo vya sheria ambao wanapelekwa katika masuala ya udhalilishaji. Mhe. Mwenasheria Mkuu juzi amesema kwamba anacho kifungu chake, kilichosema kwamba zinatakiwa kesi ziondoke kwa haraka ili kila mmoja aweze kupata haki yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti nataka nijue na kama Mhe. Waziri atakapokuja kama hawezi ampishe Mhe. Mwanasheria Mkuu atueleze hizi kesi ambazo za udhalilishaji sitakuwa na kipimo au muda gani zimalizwe, kwa sababu kwanza zinatia hasara katika serikali, munamuweka mtu

kule anakula, anafanya mambo mengi anafanya kitu gani, hebu tume na *limit* miezi mitatu, mwezi mmoja kesi hii imalizwe ili tusiwe tunakunja watu tu tukiwatia kwenye majela ambao matatizo yake serikali nayo inachukuwa mzigo ambao matokeo yake hatuyajui, kwamba pengine mtu yule hana sheria, hana hatia au ana hatia basi lijulikane katika kujifunza katika mambo tulizungumza kwamba ni Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumuunga mkono Mhe. Amina Iddi Mabrouk katika masuala ya vijana, kwa kweli tumekuwa na utaratibu unapofika wakati katika mazunguko mengi inakuwa tunabeba vijana mitaani tu na kuwapeleka rumande au kuwapeleka maeneo.

Mhe. Mwenyekiti, vijana kwa kweli kama wazazi hawawezi, lakani vijana tunapowasomba tukawapeleka rumande tunawafanya wawe sugu, tunawatia katika mazingira ambayo yanakuwa katika mazingira hata mzazi akimwita mimi siogopi tena, kule polisi na jela nimeshakwenda sana majibu yake yanakuwa kama hayo. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri akiona kumetokea suala kama hili basi asiwe nyuma kuingia polisi akaweza kulijua tatizo la vijana, kwa sababu hawa vijana ndio sisi tulikuwa vijana, mimi hapa ukiniambia mimi nani, nilikuwa kijana wa zamani, kwa hivyo hakuna hata mtu mmoja aliyekuwa hakupitia ujana.

Kwa mfano, Mhe. Said Soud Said alikuwa kijana wa zamani, kwa hiyo kila mmoja amepita ujana na ujana maji ya moto kila mmoja unamuendesha kivyake, lakini kijana hajakuwa mtu wa kuharibika kiasi hicho, kwanza kumuangalia na kuweza kumpa mafunzo mpaka akaelekea. Kwa hiyo, naomba sana na hasa maeneo mjini Mhe. Mwenyekiti wakati mwengine tunachukua hatua za dharura za vijana hawa kuwasomba somba, basi naomba Mhe. Waziri wewe katika maeneo humo humo katika kuangalia nini haki za binaadamu na mambo mengine tuweze kuziangalia vijana wasiwemo katika mkumbo sana wa kuwaweka ndani ovyo ovyo, *otherwise* tuwe tunajua tunawaweka vipi katika masuala kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa kuipongeza sana na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jitihada zake kubwa alizofanya kuwaona wazee katika pencheni zake na maeneo mengine. Nataka nimuulize Mhe. Waziri tokea kuanzishwa kwa utaratibu na Mhe. Rais kutoa pencheni kwa wazee, wajawahi kuja watu wowote wakaulizana tunafanyaje, Mhe. Rais alifanyaje au mnaendeshaji habari hizi za wazee au sisi ni watu wa kwanza na hatujapata watu ambao wanatuiga.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sisi lingekuwa jambo hili limefanywa na Rais wa pahali fulani na sisi tungesema Rais fulani amefanya hivi kwa nini na sisi Rais wetu hajafanya hivyo. Sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri tokea kufanya Mhe. Rais wa Zanzibar mambo haya, hawajawahi kuja viongozi wa nchi nyengine wakauliza Mhe. Rais wa Zanzibar amefanyaje na yeye ametekelezaje na amefanikiwa kwa asilimia mia moja pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar katika juhudi hizi, kwa kweli malalamiko ni machache kuliko mafanikio. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho akatuelekeza nini ambacho Mhe. Rais na yeye amefanikiwa na yeye ameigwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mambo haya ya ndoa, udhalilishaji wanawake na watoto ambayo yamekithiri na mambo mengine ambayo tunayaona mpaka juzi Mkuu wa Mkoa wa Dar-

es-Salaam kawaita watu waliokuwa wana watoto waliokuwa baba zao hawawajui na pengine wanajuana lakini labda mafao yao yalikuwa hayapo au hawayapati.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam siwezi kusema kwamba tumpe pongezi, lakini kwa kiasi fulani alifanikiwa kuna wengine walitaka wasitajwe wakaendeleza kwenda kuwasaidia watoto. Lakini wengine ndio naona mwenyewe atamalizana nao, sasa hili wewe sijui unalichukuaje kwa upande wetu wa Zanzibar kwamba linaweza kuchukulika hapa au halichukuliki, waliokuwa wenyewe kama na Waheshimiwa Wajumbe wapo hapa kabla na wao hawajaitwa waweze kujikubalisha kwamba nitasaidia au vipi, ili angalau tupunguze haya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze zaidi katika changamoto hizi tunabaadhi ya nchi kama Msumbiji na nchi nyengine za Afrika ya Kati na nchi nyengine hata *South Africa* wanazo tabia hizi. Zamani tulifika pahala kwa ndoa hizi zetu sisi za Kiislamu, ndoa za mkeka, maana yake mkono tu ukimpa zimekwisha. Lakini utaratibu ni kuwa na heshima na wazee na wazee wakiwaita watoto walikuwa wanaweza kulimaliza hili suala na wakaka na watoto. Sasa hivi ndoa hizi ndizo zinazoleta balaa mtu mmoja unamkuta anazaa karibu matumbo kumi, kumi na tano, atawahudumikia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kama kutakuwa na utaratibu hizi ndoa zikabadilika zikawa na mkataba. Kama mtu anafanya kazi basi ijulikane kabisa katika mshahara wake mwanamke anapata ngapi, ili akiondoka aondoke na chake, ili ajijuwe hasa kwamba mimi nakaa kwenye ndoa hii maana yake mapenzi hakuna lakini nibakishe na hichi nilichokipata. Mhe. Mwenyekiti, kama mapenzi yapo sio kila siku tungeachana inaonekana mapenzi hayapo, hivi sasa tunakwenda katika kujuana kipesa pesa, sasa kama ni mpesa pesa basi tugawane sote.

Ningeshauri kama kutakuwa na kifungu cha kuweza kuweka mikataba basi unamwambia mnapanga kabisa wewe mshahara wako ni fulani mimi napata ngapi na wewe unapata fungu lako siku ya kuachwa unajijua tu wala huendi tena kwa Mhe. Waziri ukalalamika maana cha kwako umeshapewa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hapo nazungumzia habari ya kuhusu *DNA* hii kwa upande wake Mhe. Waziri ikiletwa au ikiwepo itamsaidia katika kesi zao, haitosaidia au italeta mtafaruku zaidi au itafanya nini. Maana sisi tunapigia kelele sana *DNA* iletwe au iwepo. Siku moja alisema kwamba *DNA* itakapokuja hapa haitokuja kwa maana ya kupimwa watoto, itakuja kwa maana nyengine. Sasa wewe kama itakapokuja kama itakuwa haitumiki katika jitihada zako za kufanya mambo hayo zaidi itakuwa katika udhalilishaji. Je, *DNA* itakusaidia au haikusaidia au itapunguza matatizo kama haya katika kuangalia kwamba nani kafanya makosa au nani hana makoa au kesi imalizike kwa wakati kutokana na muda huwo, kuliko hiyo *DNA* kupeleka Dar-es-Salaam na mambo mengine yanakuwa yanachukua muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika mbili.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Haya Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli, niliona hapa katika kitabu kwenye ukurasa wa 5 katika kifungu cha 9 kilikuwa kinazungumza kwamba Wizara inatarajiwa kukusanya kiasi cha shilingi milioni 800,091,078 kwa ada za usajili, ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, ukaguzi wa mikataba ya nchi za nje, ukaguzi wa maeneo kazi vibali.

Mhe. Mwenyekiti, hili nimeiona lakini sasa je, hii *target* itafika kutokana na sababu ambazo zimetoka kwamba kuna vibali vya kutoka nje ambavyo vimezuiwa kwa wafanyakazi wetu, kuna meli zetu zimezuiwa, kuna wafanyakazi wetu wanakwenda, sina uhakika hii *target* utaifikia uliyoitaja hapa au itakuwaje. Naona mambo ya nje vibali vyake vimekuwa na utata, sasa hii *target* ya kukusanya kwa vibali hivi itafika au vipi, utakapokuja kama una nafasi ya kuweza kuichangia utachangia.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 6 katika kifungu cha 13 kinachosema, Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi. Nilikuwa nizungumzie kwamba mfuko wako umechangia. Lakini nilikuwa nimeona ilikuwa milioni 1,700,000 na hivi sasa uko kama milioni 2,300,000 na *something* kwa sababu Mwenyekiti amenipeleka mbio itabidi na mimi niseme mbio.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie Mhe. Waziri kutokana na hali ya kipesa kama hivi ilivyo, amechukua juhudi gani katika mabenki haya ukiachia Benki ya *PBA*, kuna Benki ya NMB, Benki za CRDB, ambazo zinawataka wateja na kuweza kukopesha na mambo mengine ambayo yeye angechukua kama dhamana, wale ambao ni wateja wazuri ambao anawahisi kwamba fedha hizi anawapa lakini haziwatoshi, akaweza kuwachukuliwa dhamana katika mabenki au akawasaidia vipaumbele wakaweza kuliendeleza hili gurudumu ili na wao wakachukua juhudi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo dakika moja tu. Nazungumzia kwamba kuna suala la unyanyasaji wa kijinsia lakini upande wa wanaume ameusahau. Kwa kweli, wamo wanaume humu wananyanyaswa, lakini tunachukulia nguvu za kiume kama tunazitizama hivi tunavyoziona kama ni jibaba kubwa lakini likifika ndani, Mhe. Mwenyekiti mimi nadhalilishwa wakati mwengine, sasa pakukimbilia mimi sipaoni, maana idara hii hana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja akanambia kwamba mimi nafanyaje. Jibaba kubwa usione hivi lakini wakati mwengine nadhalilishwa ndani na mama, pengine ana mambo mengi mimi simuwezi, lakini wale wanawake wanakwenda kule kusema, mimi nakwenda kusema wapi. Kwa hivyo, atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri naomba atueleze. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, moja tu hili la mwisho hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja Mhe. Mwenyekiti. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said na baadaye atafuatia Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Nadir Yussuf Abdul-latif ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kwa ajili ya kutoa mchango wangu. Niendelee tu kukuomba na kukutaka radhi kwamba bado kifua changu sio kizuri, kwa hivyo nikikohowa sina nia mbaya yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa jimbo la Tunguu ambaye nikiwa leo hapa kama ni msemaji wao na ni mtetezi wao na niwaahidi kwamba nitatumia muda wangu kuweza kuwasemea na kuweza kuishauri serikali kwa mujibu wa Katiba inavyotutaka zote.

Pia, nichukue nafasi hii kuwapa pole au kuungana na wenzetu wa nchi ya Cuba juu ya ajali iliyotokezea karibuni ya ndege tunatambua zaidi ya watu 100 wamefariki. Mimi kwa upande wangu Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Tunguu natoa rambi rambi za pole kwa kupitia Afisi ya Makamu wa Pili pamoja na kuungana na Mhe. Rais kwa kutambua kwamba nchi ya Cuba ni marafiki wetu wakubwa wa Zanzibar na tuna mahusiano ya kisheria, kwa hivyo *Inshallah* Mwenyezi Mungu ataweza kudumisha umoja wetu na Mwenyezi Mungu azilaze roho za waliopoteza maisha yao katika ajali mahali pema. Aamina.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juzi nilipokuwa nasoma katika tarifa za magazeti ya kitaifa nimeona nchi za Falme za Kiarabu ambayo ni *United Arab Emirates* pamoja na Dubai kwamba wameamua sasa watafungua Ubalozi mdogo wao katika visiwa vyetu vya Zanzibar. Kwa hivyo, wataungana na nchi ambazo zipo hapa kama China, Mozambique, Oman na wengine wote waliokuwepo tutakuwa na sisi tuna ubalozi mdogo wa Falme za Kiarabu hapa Zanzibar. Naamini itawasaidia wananchi wetu sana na pia kuwaunganisha wafanyabiashara na wale wengi ambao wanasafiri kwenda katika nchi za Kiarabu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Rais kwamba haya ndiyo matunda ya Mapinduzi yetu lakini pia na ile safari ameifanya kwenda katika nchi za Falme za Kiarabu. Sasa tunaweza kuona matunda hasa katika kuweka ramani ya Zanzibar katika nchi na kutambulika zaidi katika mashirikiano yetu ya kimataifa pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuimarisha uchumi wetu.

Baada ya hapo naomba niende katika mchango wangu, mimi sitokuwa na mengi sana. Kwanza nitaanza na upande wa udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika ukurasa wa 60 wa kitabu alichosoma Mhe. Waziri pamoja na ukurasa wa 108 cha Mhe. Haji Omar Kheir au Tawala za Mikoa Mwenye dhamana aliposoma bajeti yake. Kwa mfano, ukiangalia Mkoa wa Mjini Magharib takwimu juu ya watu waliodhalilishwa takwimu hazipo sawa, ukiangalia kwa Mkoa wa Mjini ambapo tawala za Mikoa walivyoziweka pamoja na Wizara ambayo leo Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto aliposoma bajeti yake kuna tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme ni vizuri wizara zetu au serikali hii yote kwa pamoja wakawa na *data base* moja ambayo inawasaidia kuweza kufanya maamuzi au wanapofanya uhakiki na kuangalia yale wanayoyakusudia, basi wakawa na takwimu ambazo serikali au wizara zote zinakuwa zinakwenda sawa. Natambua suala la udhalilishaji ni suala mtambuka, linaweza

likagusa maeneo tofauti, basi ni vizuri serikali yetu inapokuja wawe wana *data* moja, kama vile suala la utalii unakuta wakati mwengine wizara moja inaongelea *data* ambazo zinakuwa hazendi sambamba pamoja na wizara nyengine. Naomba kushauri suala hili litawasaidia zaidi katika suala la kufanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikamuomba Mhe. Waziri atakapokuja ameomba mara hii kwenye bajeti yake apatiwe bilioni 1.7 basi atwambie makusudio yake ili wananchi hasa wa Jimbo la Tunguu ambao nawawakilisha na ndugu zetu tofauti waweze kumsikia nini atatumia fedha hizi katika maeneo gani katika mapambano haya ya udhalilishaji.

Pia, ukiangalia kwenye kitabu chake suala la udhalilishaji, matokeo ukiangalia kuna tofauti baina ya 266 na watu mwaka jana na mwaka huu kufikia 406 kwamba idadi imeongezeka. Ni vizuri akatueleza ni sababu gani zimepelekea kuongezeka watu au inawezekana kwamba serikali sasa watu au wananchi wameshawishika zaidi kwa hivyo wamejitokeza zaidi kuweza kuonyesha au kwenda kuripoti matokeo au uhalifu kwenye suala hili umeongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka nizungumze suala moja ambalo nahisi juu ya udhalilisha umekuwa unatusumbua sana. Mhe. Mwenyekiti, kama unakumbuka wale wenzetu wa Afrika ya Kusini miaka ya nyuma au baada ya kiongozi wao Nelson Mandela alipotoka ndani ili katika kuleta umoja katika wananchi wa Afrika ya Kusini hasa walipotoka katika mfumo mzima wa utawala wa ubaguzi wa rangi wale Makaburu ilikuwa bado hakuna kupatana baina ya wale watu weuzi ambao ni Waafrika katika nchi ya Afrika ya Kusini pamoja na Makaburu. Kwa kweli, kitu kilichowasaidia wao walianzisha Tume ya Upatanishi ambayo ikiitwa na *Truth and Reconciliation Commission* na iliongozwa na Archbishop Desmond Tutu na iliwasaidia sana wananchi wa Afrika ya Kusini wale ambao walikuwa wakipambana au walidhalilika au waliathirika au waliumia kwa njia moja au nyengine wakati wakibaguana katika ule utawala wa Makaburu katika ile miaka ambayo waliyokuwepo wakitawala katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka nishauri vitu viwili kwenye suala la udhalilishaji, najaribu kujenga hoja kwamba bado wengi ambao tumo ndani ya Baraza la Wawakilishi na hasa baada ya kutunga sheria tunapata ukakazi na ugumu kuangalia ni vitu gani vinapelekea mpaka binaadamu anafika pahala kumkamata mtoto mwenye miaka minne, mitatu, mitano na kuendelea na kuweza kuwalawiti. Lakini pia ukiangalia katika hali ya kawaida ni kitu gani kinamfanya binaadamu huyu kuweza kuvutiwa kwenda kushika viumbe kama hivi. Inawezekana kwa upande wa visiwa vyetu tunahitaji watu waweze kuanza kuzungumza uchafu huu ambao unaofanyika.

Hoja yangu ni kwamba labda katika familia ambazo zimeathirika katika watu ambao wameathirika kwa njia moja au nyengine aidha katika watoto wao kubakwa, pengine inawezekana pia ikaleta mambo ambayo yakachipukia katika hizi familia ambayo yapo nje ya uwezo wetu sisi kufikiria (*very beyond our comprehensive mind).* Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kushauri kwamba wizara mwenye dhamana aangalie kwa undani Mhe. Maudline Cyrus Castico kama tunaweza kuwafuata *psychiatrists* watu wenye mambo ya wenye uwezo wao waanzishe japo kitengo cha watu kuanza kuzungumza ili katika maeneo haya tupate kujua hasa tunapambana na kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, tunapoimba wimbo wa udhalilishaji, kwamba watu waache lakini pengine tayari watu wameshaathirika kiakili katika familia na pengine tunaangalia koo tofauti hasa kwa udogo watu na uchache wetu tulivyo katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa hivyo, nishauri jambo hili sasa tuanze kuliangalia kisaikolojia ili kuweza kujitayarisha, kwa sababu mapambano haya tunahitaji mbali ya fedha au katika kutoa elimu, inawezekana tunahitaji vita ambavyo hatujawahi kuviona tangu Uhuru wetu sisi au tangu Mapinduzi kwa upande wa Zanzibar. Mimi nashauri waangalie *the other side of the coin* wajaribu ku-*twisty*, kuangalia katika suala hili tunaweza tukaunganisha nguvu zetu kiasi gani ili tukaweza kuwasaidia wananchi wetu.

Suala la pili ninalotaka kulizungumza ni suala la *DNA*. Mhe. Mwenyekiti, *DNA* mashine imezungumzwa sana hasa pamoja na Mhe. Naibu Spika, tangu mwaka juzi. Lakini *cost* za kufanya *DNA* juzi nilikuwa naongea na mtaalamu mmoja anasema alifanya *test* ya *DNA* Nairobi ilimugharimu dola 500 sawa kwa fedha ya Tanzania kama haitopungua shilingi 1,100,000 kwa *test* moja ya *DNA*. Kwa hivyo, naomba atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri katika suala zima la *DNA* ambalo najua litakuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Afya, atwambie hizi gharama ambapo hizi mashine itakaponunuliwa wamejipangaje na Afisi ya *DPP* pamoja na Jeshi la Polisi pamoja na wizara yake juu ya gharama za *DNA* atakuwa analipa nani ili katika kutafuta haki pale ambapo makosa ya kijinai yametendeka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nataka niende kwenye suala la ajira. Pahala pana mageuzi unapotaka kuonesha tofauti yoyote lazima utakumbana na mambo tofauti yatajichipukia. Kwa hivyo, hasa moja katika wizara hii ambalo nalitambua wamepata *challenges* au mtikisiko au mshtuko kidogo ilikuwa suala la ku-*introduce* viwango vya sekta vya chini kwenye sekta binafsi. Hivyo, nataka nishauri tu vitu viwili wala sina ni mbaya yoyote kumsaidia Mhe. Waziri na kutimiza majukumu yangu ya Kikatiba.

Mhe. Mwenyekiti, nijaribu kuangalia katika nchi zetu za Afrika katika suala la *minimum wage* hasa katika sekta binafsi, sasa ukiangalia kwa mujibu wa MKUZA na mambo ambayo tumejaribu kuyangaalia sisi za kuchajia uchumi wetu tumetaja kwamba ni *Tourism, trade and services* ambayo ni utalii, biashara na huduma.

Sasa ni dhahir kwamba nchi yetu sasa ukiangalia uchumi ambao tunautumia sasa hivi ambao zamani tukiangalia tulikuwa kwenye Ujamaa, lakini sasa hivi tunasema tupo katika *mixed economy* inamaana tuna Ujamaa, lakini pia tuna Ubepari (*capitalism*) lakini pia tunatumia *socialism* pia, vile vile kuna maeneo serikali bado itakuwa inadhibiti, sasa ili kuisaidia sekta binafsi na ukiangalia na nchi zetu jirani zinavyokwenda ukenda hapo Kenya tu basi na hasa sisi Zanzibar ambao tunategemea sekta binafsi pia iwe ni *engine* ya kusaidia au kuwa kama ni sehemu ya kukuza uchumi wetu.

Kwa hiyo, sasa nataka nishauri katika kuangalia viwango vya mishahara vya Kenya, ukingalia kwa mfano Kenya ukienda Mombasa viwango vya *minimum wage* viko tofauti na vya Nairobi na vile viwango vya *minimum wage* vya Nairobi viko tofauti na Kisumu, lakini ukiangalia pia viwango vya *minimum wage* vya upande wa kila sekta, sekta ya ujenzi, sekta ya huduma, sekta ya afya kila sekta ina bei zake ambazo zimewekwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nimshauri Mhe. Waziri ajaribu kuangalia kwa upande wa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwa kila maeneo katika sekta ya ujenzi, sekta ya viwanda, sekta ya biashara, sekta ya utalii ambao pia ndani yake ina malazi, ina huduma za kama kutoa vyakula, lakini pia kuna madaraja ya mahoteli na maeneo tofauti, waangalie kwa ujumla ni utaratibu upi utakuwa ni mzuri pia pamoja na katika viwango ambavyo vitakuwa *skill* na *low skill* lakini kwa kuzingatia na elimu, lakini pia katika wale *day workers* ambao ni *skill labour* na *unskill labour* ambao hivi sasa zimetoka katika shilingi 7,000 mpaka 25,000, 10,000 mpaka 30,000 kuangalia katika kila sekta ambazo zilokuwepo ni ipi itakuwa inaweza kuwasadia wananchi bila kuleta mtikisiko wowote na kuleta umoja baina ya sekta binafsi na serikali.

Baada ya hapo nataka nizungumzie suala la ajira la vijana. Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kwanza lazima nikubali ina mambo mengi, na ukiangalia kwa *resources* na fedha ambazo tunampa Mhe. Waziri tunaweza tukasema bado hazitoshi lakini kidogo ni kidogo lakini kile kidogo ulokuwa nacho unatakiwa ukifanyie kazi ipasavyo kwa mujibu wa utaratibu wa sheria na jinsi Baraza hili linavyoweka zile bajeti.

Leo ukienda hata ukiangalia Mji Mkongwe ni Mji wa kizamani lakini pia unavutia watu wengi sana kwamba ina maana hata kitu kikongwe bado kina mvuto wake. Sasa, niseme tu kwamba japo kidogo unachokipatia wizara hii lakini naamini Mhe. Waziri bado anaweza kufanya mengi katika kuwatumikia. Kwa hiyo, moja ambalo nataka nilizungumze la kumshauri Mhe. Waziri najua Mhe. Mwenyekiti, kwamba mara nyingi tunatumia nguvu sisi *backbenchers* kutoa ushauri ndani humu, lakini pia tunapata ugumu pia wakati mwengine kwamba majibu tunakuwa hatupati, bado nitaendelea kutimiza wajibu wangu kuishauri serikali, bado nikiamini kwamba ipo siku ndoto yangu ya kuwa ule ushauri tunaowapa serikali utaweza kuwa, sasa moja ambalo nataka nishauri kuhusu ajira kwa vijana.

Mhe. Mwenyekiti, tunapoongelea ajira kwa vijana tusiangalie ajira kuwasaidia wananchi wetu kuweza kuajiriwa ndani ya nchi husika au kwa mfano ndani ya Zanzibar au Tanzania, mimi nawapongeza sana wizara kwamba wameanza kuangalia kuwatoa vijana wetu kwenda kufanya kazi katika nchi tofauti zilizokuwemo ndani ya bara la Afrika na katika Falme za Kiarabu.

Sasa moja katika ambalo nataka nimshauri Mhe. Waziri aanzishe japo Kitengo cha Ubunifu cha ndani ya wizara hasa moja katika ambalo tutaweza kuwasadia vijana hasa baada ya kupata elimu ile ambao inaweza kuwasaidia kiufundi ni kutumia ubunifu na kuanganisha nguvu zao kwa pamoja, ili kuweza kujitoa katika suala la kujikomboa katika umasikini. Kwa hiyo, njia moja ambayo wanaweza kutumia ni kutafuta mitaji yao ya kifedha lakini pia kuangalia kitu ambacho Zanzibar kinahitaji au Tanzania lakini wapi wao wataweza kufanya. Sasa moja nililoweza kuwaunganisha ni kuwapatia elimu pia kujifunza kwenda katika maeneo nchi za jirani, pia kujifunza pia zinapotokea zile fursa kuwapeleka vijana wale ambao watakuwa wanaweza kwenda kujifunza katika maeneo.

Kwa kweli, si vibaya kuzungumza na nchi ambazo ni marafiki wenzetu kama Wachina serikali ya India pia wametumia muda mwingi hawa na wanao uzoefu mkubwa sana. Sasa nimuombe tu kwamba naamini hili litaweza kumsaidia na ataweza kufanikisha na *Ishaallah* Mwenye Mungu taweza kuwasadiai vijana wetu nikiamini kwamba wanaipenda serikali yao na serikali hii ipo katika kutekeleza wajibu wao kuwasaidia wananchi.

Baada ya mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nakuutumia ipasavyo dakika zangu kumi na tano, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi na niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza na niseme tu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa mategemeo yangu kwamba waziri atapokuja atatupa ufafanuzi mzuri na wakutosha ahsante sana. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sasa, naomba nimwite Mhe. Mgeni Hassan Juma na baadae akifatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi kidogo niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai na uzima na ambae ameniwezesha leo hii kusimama ndani ya Baraza letu Tukufu kwa ajili ya kuweza kutoa mchango wa mambo mawili matatu katika wizara hii.

Pia, nimpongeze sana Me. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wote wale ambao wanatumikia wizara hii katika hali ngumu hususan katika hali ngumu ya kibajeti, lakini bado wanamoyo wa kuendelea na kutumikia taifa lao.

Mhe. Mwenyekiti, sitokuwa na mengi sana ya kusema, na mambo mawili matatu na ni mengi zaidi ni masuala mazima ya kushauri wizara, lakini kabla ya kuanza kusema hayo niseme tu kwamba naunga mkono hotuba kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia katika ukurasa wa 6, ambao unazungumzia suala zima la namna walivyoweza kusaidia wananchi katika Programu ndogo ya Mfuko wa Uwezeshaji, niwapongeze sana wizara kwa hilo na ninaamini kwamba katika wale ambao wamefaidika kupata mikopo na kama ninavyosema hizi taarifa zilokuwemo ndani ya kitabu chao ni kwamba wengi kwa asilimia nafikiri tisiniini na tayari wameshakuwa wanalipa mikopo hiyo.

Kwa hiyo, naiomba sana wizara walitizame suala zima la kuona namna gani mikopo hii imebadilisha maisha ya wale ambao wamekopa, kwa sababu tukisema tu kwamba wanarudisha mikopo mtu anaweza kufanya njia yoyote jambo lolote ili anahakikisha anaweza kurudisha mikopo, lakini muhimu ni kutizama *value for money*.

Lazima tuangalie tufanye tathmini sasa ya kuona je hii mikopo inawasaidia vipi wananchi na hususan kwenye yale makundi ya wanawake vijana pamoja na watu wanaoishi na ulemavu. Kwa hiyo, naomba sana wizara wasimamie suala zima la kuona fedha ambazo zinatolewa zinabadilisha maisha ya wananchi, Mhe. Mwenyekiti hilo naona ni jambo muhimu kulifanya.

Jambo jengine nichukue fursa hii nimpongeze sana na nasema hili kwa sababu Mkurugenzi anayehusika na masuala ya ushirika. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mkurugenzi kwa sababu nakumbuka tulikuwa na ziara katika maeneo yetu mimi na Mhe. Mwakilishi Saada Ramadhan Mwendwa na tuliwahi kujaribu kumuomba Mkurugenzi kwamba tunataka aje awape mafunzo

wanawake kuhusiana na masuala ya ushirika. Mkurugenzi alikuwa kwenye likizo nakumbuka vizuri sana lakini akanambia kwamba naweka pembeni likizo yangu nakuja kutoa mafunzo na alikuja mwenyewe binafsi na hakuja siku moja alikuja siku saba na Mkurugenzi tukaaenda mpaka kwenye ziara wakati yeye yuko, kwa kweli ulikuwa ni uzalendo mkubwa sana, nampongeza sana kwa hilo. (*Makofi)*

Lakini Mhe. Waziri suala ambalo nimeliona katika kutoa yale mambo ambayo mmeyafanya ya kuunganisha na kuanzisha sakosi mbali mbali pamoja na kuanzisha vikundi vya ushirika mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana wizara iangalie upya hasa katika maeneo yetu katika maeneo yetu majimboni utakuta kuna vikundi vingi sana vidogo vidogo vya ushirika ambavyo vikundi vile mara nyingi sana havileti tija au faida kwa wale ambao wanajishuhulisha na shughuli zile za ushirika. (*Makofi*)

Kwa kweli, mara nyingi sana vikundi hivi vinakuwa vinategemea sana msukumo wa Wawakilishi wao au Wabunge wao. Sasa naomba wafanye tathmini katika majimbo yote na kujua vikundi vingapi vya ushirika vilivyomo katika kila jimbo Unguja na Pemba na kuona namna gani wataweza kuunganisha nguvu na kuwa katika kila Wilaya angalau au Mkoa kuwe na *SACCOS* moja ambayo itauunganisha vikundi vyote vya ushirika. (*Makofi*)

Hiyo itasaidia sana tunasema umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, ili kuvipa hivi vikundi vidogo vidogo vya ushirika viwe na uwezo wa kuweza kukopa katika taasisi mbali mbali pamoja na kukopa kwenye mfuko huu, kwa sababu mara nyingi sana hivi vikundi vidogo vidogo vinakosa mikopo kutokana na hali halisi hata katika shughuli zao ambazo wanazifanya.

Vile vile itakuwa ni sababu moja ambao itasaidia katika kutoa elimu ya ujasiriamali kwa upeo mkubwa zaid kuliko kuingia katika vikundi vidogo vidogo. Kwa hiyo, naomba sana pamoja na kushauri suala hilo liangaliwe upya tuone namna gani tutaweza kusaidia wananchi katika kuhakikisha kwamba wataweza kupata mikopo na misaada mbali mbali kutoka katika taasisi za kifedha na taasisi nyengine.

Lakini, pia nimegundua kwamba bado kuna biashara mbali mbali zinazofanyika ambazo hazijarasimishwa kwa maana ya kwamba kuna watu wanafanya vitu lakini hawako rasmi, na hii inasababisha vile vile kuwarudisha nyuma katika maendeleo ya shughuli zao za ujasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, nikisema hivyo ninakumbuka wakati tulikuwa na wageni wetu hapa kutoka Arusha tulikwenda ziara tukatembea katika eneo moja tukakuta kazi nzuri sana ambayo inafanya ya kutengeneza milango ya Zanzibar, wanaita *Zanzibar Door*.

Sasa katika utafiti wangu nikagundua wale watu hawako rasmi lakini nikagundua vile vile hata hawajui fursa gani ambazo wanazikosa, sasa unakuta wengi wapo kama hawa ambao kwa kuwa hawapo rasmi, hawatambulikani wanakuwa ni vigumu kuweza kuendelea lakini kazi ile ambao ilikuwa inafanywa pale kwa kweli ni kazi nzuri sana, ile peke yake inaweza kusaidia katika kukuza uchumi wa nchi. Vile vile, kuwasidia vijana kupata ajira, kwa sababu tumewakuta vijana wengi wanafundishwa kazi za mikono wanachonga milango wanachonga meza wana-*decorate decoration* za kiasili za Kizanzibar, wanafanya hizo kazi na wamefanya kazi nzuri sana nilikuta meza mimi nilishangaa katika kutembea kwangu kote sijawahi kuiona duniani meza nzuri ajabu, lakini kazi zile haziko rasmi.

Kutokana na hali hiyo, inabidi sasa tuwarasimishe ili waweze kuzalisha kazi kama zile nyingi, na hizo kazi zitaweza kusaidia kwa sababu wale wanaweza kuzalisha zaidi wakaweza kupeleka nchi za nje pamoja na kukuza soko letu la Utalii. Kwa hiyo, naomba sana waendelee kutafuta na kufanya utafiti na haina haja kwamba lazima watu waendee kwao wawafate wao waambie sisi tunataka hapana watoke waendee katika maeneo na washirikiane kama na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa washirikiane, ili waweze kutambua miradi ambayo wanaweza au wajasiliriamali ambao wanaweza kuwasadia katika kurasimisha.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitoe pongezi zangu nyingi sana katika suala hilo hilo la masuala ya ushirika, natoa pongezi kwa Mhe. Waziri kwa kufufua upya Soko la Jumapili. Mhe. Mwenyekiti, Soko la Jumapili ni zuri sana na wananchi wengi hasa akinamama wanakwenda pale kwa ajili ya kuuza biashara zao na kwa ajili ya kujipatia riziki, nipongeze kwa sababu hili soko lilianza kuyumba na wale akinamama hawana sehemu nyengine za kwenda lakini wizara imehakikisha kwamba lile soko linafufuka na kuweza kinamama kuuza bidhaa zao na kujipatia riziki.

Sasa, naomba sana paboreshwe lile eneo liboreshwe lifanywe liwe bora zaidi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora hayupo haipendi hii kauli lakini ile kuboreshwa ile eneo kufanywa bora zaidi na kulifanya lile eneo likawa ni eneo ambalo hata wageni wetu wakija watalii wanaweza kutembelea eneo lile na kusaidia basi katika suala zima la kununua bidhaa ambazo zinatengenezwa Zanzibar, na hiyo iyende sambamba na kuwaongezea uwezo, kuwaoongezea *skills* mbali mbali uwezo mbali mbali ambao wataweza kujifunza na kuona namna gani wataweza kujipatia riziki katika suala lao.

Lakini, nimehisi hilo ni muhimu sana, kwa sababu juzi tulikuwa tunazungumzia suala la utalii hapa na tukaona kwamba bado tunatafuta vitu vyenye asili ya Kizanzibar ambavyo tutakuwa na uwezo wa kuonyesha dunia wa kuona kwamba hii ni *product* ya Zanzibar, lakini hilo lazima tulifanyie kazi sana lile eneo tayari tumeliweka kama ni eneo la kihistoria, lakini hata hivyo maeneo kama haya vile vile yanatumika katika nchi mbali mbali yanatumika katika kutengeneza bidhaa ambazo zitakuwa *unique* kabisa ambazo bidhaa hizo watalii wakija wanaweza kuzinunua.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kuendelea kuwasaidia na kutoa *support* hususan kwa wazee wetu, nalisema hilo kwa sababu nadhani kwa upande wa Afrika Mashariki nzima nafikiri Zanzibar tumekuwa ni kigezo kizuri sana katika suala hilo. *(Makofi)*

Nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa hatua ambayo ameifikia kwa kutoa posho hata kwa wale ambao hawajawahi kufanya kazi ya aina yoyote, lakini kwa sababu wao walikuwa ni wananchi wa Zanzibar basi wao vile vile wananufaika na fedha hizo. Kwa hiyo, niseme kwamba nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar lakini naipongeza na wizara kwa kulisimamia hilo, kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar anaweza kuwa na nia njema, lakini wizara ikashindwa kulisimamia napongeza sana wizara kwa kuweza kulisimamia hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na suala moja najiuliza hapa katika bajeti nakwenda katika suala zima la udhalilishaji Progamu ya Uzalilishaji wa Kijinsia na nafikiri tayari kuna wengine

wameshaliuliza kwa sababu wengi hapa tumejiuliza tulikuwa katika makadirio ya 2017/2018 pesa zilikuwa kidogo sana nakumbuka hapa tuliwahi kuziongeza pesa katika fungu hili.

Mhe. Waziri, lakini naamini atakuja na majibu mazuri katika 2018/2019 fedha hizi zimepanda hadi kufikia 1,700,000,075, nataka kujua nini kitafanyika kwa pesa hizi ambazo ziko hapa kwa sababu tunaona katika kipindi hiki zimetumika 150,270,000, lakini sasa tumeona zimepanda na zimekuwa 1,700,000,075. Kwa hiyo, tulikuwa tunataka kujua ni hasa ni kitu gani kuna programu gani ambazo zinatakiwa kufanyika. Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la udhalilishaji bado ni changamoto tunakufahamu kwenye masuala hayo ya udhalilishaji tunakufahamu sana mheshimiwa umekuwa masuala haya unayapa kipao umbele na unafanya kazi kubwa sana wewe pamoja na watendaji wako, lakini kuna mambo ambayo lazima sasa hivi yafanyike.

Mhe. Mwenyekiti, sijui kama kitengo chako kinachoshughulikia masuala mazima ya ushauri nasaha sijui kinafanya kazi vipi. Lakini, tumekwenda katika maeneo mbali mbali tumegundua kwamba wale *victims* wale waathirika hawapati ushauri nasaha kuna tatizo nafikiri Mhe. Simai Mohammed Said amelizingumza hilo kidogo kuna tatizo, kwa sababu tukiwaachi tu wananchi tukasema kwamba limeshatokea mtu keshaathirika tunasubiri kesi tu, tunasubiri mahakama ifanye maamuzi hilo peke yake halitoshi tunataka kuona wale waathirika na waathirika sio mtoto tu kwa sababu mtoto anapoharibiwa, au mtoto anapofikwa na mzazi anaathirika, mzee anaathirika hata majirani wanaathirika.

Kwa hiyo, sijui wizara yako ina kitu gani ambacho kinafanya kina mpangilio au katika fedha hizi labda utatuambia kwamba katika fedha hizi vile vile suala zima la ushauri nasaha litakuwemo.

Jambo jengine ambalo nataka kuligusia ni suala zima la usawa na kijinsia. Mhe. Mwenyekiti, hapa katika suala zima la usawa wa kijinsia nina mashaka makubwa na kazi ambayo inafanywa na wizara yako.

Mhe. Mwenyekiti, wakati hapa tumeshapitisha bajeti nafiri sijui tatu lakini Mhe. Waziri hii ni kazi yake Mhe. Mwenyekiti kuna bajeti zinafika hapa hazina uchanganuzi wa wanawake na wanaume katika masuala ya ajira, lakini katika masuala ya elimu mafunzo ambayo wanapata Mhe. Waziri wizara yake hilo ni muhimu sana na mheshimiwa wizara yako ndio inatakiwa kulisimamia hilo, lazima tupate taarifa inayohusisha mchanganuo wa wanawake na wanaume wanaofaidika katika ajira lakini katika mafunzo mbali mbali ndani ya wizara zao, mheshimiwa hiyo ni kazi yako ya kuifanya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine kwa sababu nimetizama katika ukurasa katika masuala ambayo wamesema wameyafanya katika 2017/2018. Mhe. Waziri sijaona kitu hasa cha kukamata katika haya mambo ambayo mumeyafanya yanayohusiana na usawa wa kijinsia mumezungumza zaidi kushiriki katika kufanya makongamano na kushiriki katika maadhimisho haitoshi, tunapo zungumzia usawa wa kijinsia tunazungumzia ku-*monitor* usawa wa kijinsia tunatakiwa tu-*monitor* katika kila wizara, katika kila sekta, katika kila taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni kazi ya wizara yake Mhe. Waziri hapa hamna jambo hilo lakini pia tunazungumzia sheria ziko sheria tunajua kwamba ziko sheria zinakandamamiza wanawake, zinakandamiza akinamama sheria hizo je mnazifanyia kazi na mnashirikiana vipi na Mhe.

Mwanasheria Mkuu, kuna Sheria ya Masuala ya Ajira, sheria ile ina mapungufu mengi kina mama wanateseka katika maeneo yao ya kufanyia kazi inaitwa *Labour Decree* kuna matatizo. Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti kama wizara yake haitosimamia hapa huo usawa wa kijinsia ambao tunauzungumzia ambao tunasema kwamba tunashiriki tu katika vikao sio lengo, tunapozungumzia usawa wa kijinsia sio lengo kushiriki au kutengeneza makongamano, isipokuwa lengo ni kuhakikisha kwanza tunapeleka elimu katika maeneo mbali mbali ikiwemo kwenye wizara, watu waweze kuona ule usawa uko wapo wenyewe wako ndani ya mawizara waone usawa uko wapi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika suala hili wizara ijipange kwenye nchi za wenzetu tunaona kwamba wana wizara maalum ambayo inashughulikia masuala ya jinsia, sisi lakini tunayo na ndio tunaona kwamba ndio kimbilio letu tunapozungumzia usawa wa kijinsia ni wizara yako Mhe. Waziri. Kwa hiyo, naomba hili litiliwe mkazo, mimi nimevunjika moyo Mhe. Waziri sikufichi nimevunjika moyo sana kuona kwamba hapa tunazungumzia kuimarisha vikundi vya ujasiriamali kuna, lakini kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, mikutano miwili na Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, hizo hazitoshi Mhe. Mwenyekiti hii sio usawa wa kijinsia. Usawa wa kijinsi ni kuwekea mikakati namna gani tutapata usawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Mhe. Waziri, nafikiri umenielewa vizuri sana, hivyo namuomba Mhe. Waziri kwamba haya masuala kama anaweza kuyajibu atajibu na utatoa ufafanuzi, lakini naomba sana ayafanyie kazi na najua anao wataalamu, kwa sababu watalamu wake sisi UWAWAZA huwa tunawatumia sana kwenye masuala ya jinsia tunawatumia, tunawashukuru sana kwamba tunakuwa nao tukumbuke kwamba tunasaini mikataba ya kimataifa, ambayo inahusiana na masuala haya ya kijinsia kwa hiyo tuone namna gani ile mikataba tunaweza sisi tukaifanyia kazi.

Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii basi nimtakie kheri Mhe. Waziri ili aweze kufikisha salama na vizuri kabisa, naomba sana watu wamuunge mkono lakini naomba Mhe. Waziri aendelee kufanya kazi, kupigania haki za wanawake hususan kwenye masuala ya ajira. Kwa kweli, ajira katika taasisi mbali mbali wanawake bado hawapati mishahara inayostahiki, tunaomba hiyo kazi uifanye Mhe. Waziri na anajua kwamba nimeshawahi kwenda kwake, kuna watu wamekuja hapa kwa Naibu Spika, wamekuja kwa Naibu Spika na kutaka uwasaidie. Mhe. Mwenyekiti, hatua alofikia Mhe. Waziri ni nzuri, naomba ashike kamba hiyo hiyo pamoja na kuwasaidia sana kuhakikisha wanawake Wazanzibari wasinyanyaswe kiholela.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe na baadaye atafuatia Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mwenyekiti, kunipa nafasi nikachangia hotuba ya Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niungane mkono na wake wote waliotangulia kumshukuru Mwenyenzi Mungu kutujaalia leo Ramadhani tukawepo hapa na wale wote waliowapongeza, waliowashukuru viongozi wa wizara hii. Vile vile shukrani zangu za dhati kabisa ziende kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa uteuzi wa kijana Ali Ameir au Ali Suleiman Mrembo kuwa

Mkurugenzi wa Utumishi pale katika wizara ile tunaamini kwamba vijana sasa tunaanza kuonekana na tunaminiwa na tunafanya kazi kweli nimpongeze sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika hoja bila ya kupoteza muda nimejaribu kupitia kitabu hiki cha makadirio ya mwaka 2018/2019 na nikaangalia kile kitabu cha mwaka jana bado yake mapungufu tuliyosema mwaka jana mwaka huu yamo tena, kitabu chako Mhe. Waziri kizuri sana lakini kina kosa muongozo hapa mbele yaliomo (*contents)* nini maana yake, maana yake unaturahisishia sisi hata kusoma kutafuta mafungu inakuwa vizuri tulisema kitabu cha mwaka jana na narudia tena kusema kitabu kinachoingia ndani ya Baraza la Wawakilishi vingi vimekuja vyote hivi vinayo yaliomo (*contents)* imo lakini hiki chako cha mara ya pili mwaka jana hakijakuwemo na mwaka huu vile vile tatizo nini.

Mhe. Waziri nafikiri hilo tu si suala kubwa sana, ili kitabu kipendeze kiwe kizuri zaidi, basi angalau iwemo *contents* hapa yaliomo, ili iturahishie sisi kusoma au tunaona kifungu cha ustawi naenda namba fulani mpaka hivi hivi lakini hicho ndio hivyo lakini mambo mengine yote mazuri na mheshimiwa hongera na mheshimiwa hongera sana kwa kazi zako unazofanya. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme hilo. *(Makofi)*

Vile vile, nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa bila ya hata unafiki katika suala ambalo unalisimamia juu ya Ustawi wa Jamii tumeona juzi tu Mhe. Naibu Waziri wako kwenda kukabidhi gari. Baraza lililopita tulipiga kelele humu kwamba pale wazee wapatiwe gari panatokea mgonjwa pana nini *Alhamdulillah* Mhe. Waziri msikivu umelifanya hilo suala ma juzi Naibu Waziri kakabidhi gari hongera sana Mwenyezi Mungu akutangulie Yesu akusimamie.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele na mchango wangu nisimame katika Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi naona hapa imeandikwa mambo mazuri *Alhamdulillah* bajeti ya mwaka huu 2017/2018 imewekwa milioni mia sita na sitini laki nne sabini na moja elfu nzuri. Lakini ukiangalia kwamba tulizipanga tulikutumia 2018/2019 ni milioni mia sita kuna upungufu kidogo je, mahitaji yamepungua au kipi kilichopeleka kwamba watu wanakwenda mbele sisi tunarudi nyuma katika masuala kama hayo, kwa sababu kila siku *demand* zinaongezeka.

Sasa wakati atakapokuja kufanya majumuisho atufahamishe kwa nini mwaka huu 2017/2018 tuliweka hizi kutumika milioni mia sita na sitini lakini tulichokipanga kwenye bajeti ijayo 2018/2019 tulipanga milioni mia sita lakini kuwapa watu mia sita. Kwa hiyo, kidogo hapo kuna walakini namna gani ndio leo kwamba tunaweza kutoa mbuzi moja pengine au mbuzi wawili kwa kundi la watu kumi au ishirini inakuwa haileti maana kibuzi kile kimoja, bora tu utowe mbuzi moja kwa watu watatu au wanne wanajua namna gani kinachofanyika, nilitaka niseme hilo kidogo ulipime juu ya hii mikopo inavyotoka.

Lakini kuna suala zima la uwezeshaji mimi nakumbuka wizara yako ina shamba pale Muungoni je nyinyi wenyewe mumejipanga vipi kuliendeleza shamba lile je munalijua kwanza kama wizara ina shamba pale Muungoni na lile shamba mumeliendelezaje, kwa sababu nyinyi mnaendeleza wananchi kiuchumu, munawashajihisha nyinyi wenyewe je mumeweka kwamba sehemu ile shamba darasa kwa wale ambao wananchi mnaotaka kuwasaidia katika fani ya kilimo, nafikiri eneo lile pale mnalo lakini sijui vizuri taratibu zake liko vipi au kama watu

wengine washajichukulia, basi namuomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho nitamuomba sana atufahamishe juu ya suala ya lile shamba pale Muungoni.

Vile vile, nikiendelea mbele nende katika suala zima la Ustawi wa Jamii hapo hapo nagusa juu ya kadhia ya Nyumba yetu ya Kulelea Watoto pale Mazizini siyo Forodhani, kwa sababu Forodhani ilikuwa zamani imehamishwa Forodhani imekuja Mazizini. Mhe. Mwenyekiti, yalikuja maswali hapa kwenye Baraza hili hili kuhusu umiliki wa nyumba ile pale, lakini inasemekana kuna baadhi ya watu wamefunga baadhi ya vyumba ya nyumba ile, je ni kwa misingi gani wafunge na kwa nini wafungu ya kwao, serikali siyo ya kwetu wametuazima baadhi ya vyumba wanavitumia au ni ya serikali lakini imewapa watumie wale watu ndio maana wakaamua kufunga.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho atusaidie kuhusu kadhia ya ile nymba tatizo nini, nakumbuka au nafahamu kwamba naambiwa ya Taasisi ya *ZAYADESA* sitaki kusema nani *ZAYADESA* wala sijui iko chini ya nani, lakini nimeambia tu kwamba *ZAYADESA* ndio wamiliki.

Ikumbukwe tu tulikuwa na Nyumba yetu Forodhani ya Kulea Watoto Hayati Mzee Karume aliwatengea watoto pale iwe karibu na Forodhani nasikia pana *park*, pana bahari, pana *park* nzuri tu, lakini baadaye watu waliondelea kusoma waliosoma sana wakasema tuwaondoe kule tuwapeleke huku tuwakimbize wanaweza kupata starehe pale za Forodhani na bahari tuwaeke huku Mazizini, nyumba imejengwa vizuri *Alhamdulillah*, lakini inasitisha kwamba baadhi ya vyumba nyinyi wenyewe wizara hamvitumii vimefungwa, kwa sababu gani vifungwe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika hicho wakati atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri atupatie majibu *atleast* watu wetu waweze kutufahamu ni azma nzima ya uwepo wa nyuma pale namna gani, mambo mengine *Alhamdulillah* kule kwa wazee sasa hivi nashukuru wanakula mlo ambao wenye kufahamika mlo wa *menu* kabisa. Kwa kweli, nimpongeze sana yule dada pale mimi namjua yule mimi nimesoma naye darasa moja Bi Ashura yuko kule Welezo anafanya kazi vizuri, kwa hivyo nishakwenda kumtembelea si mara moja mara mbili Mwenyezi Mungu amzidishie anafanya hayo, kwa sababu ya uzalendo wake na imani yake, kwa sababu asingekuwa mzalendo na imani yasingefanyika kwa sababu walikuwepo watu pale mwanzo lakini hawayafanyi hayo, kwa sababu si wazalendo na hawana imani yule bibi *Alhamdulillah* ana imani na uzalendo anafanya hayo nashukuru sana. *(Makofi)*

Nikiendelea mbele vile vile niende katika suala zima wenzangu wengi walopita hapa wamelizungumzia lakini na mimi sitokuwa vibaya pia kuzumgumzia juu ya kwamba hili fungu la Q0101 Kukuza Ustawi wa Jamii, Jinsia, Uendelezaji, Wanawake na Watoto bajeti iliyopita hapo mwanzo mlitenga *just* milioni 50,000,000 tu, lakini kwa umadhubuti na umahiri wa Baraza la Wawakilishi wakasema hata bajeti hii haiwezekani kumpa nguvu Mkurugenzi kwenda kupambana na udhalilishaji hili fungu liongezwe na bahati nzuri likaongezeka ikawa milioni mia tatu.

Lakini leo mumekuja na bajeti ya *one point seven billion* (1,700,000,000) pesa nyingi sana nafikiri mara tatu imeongezeka, sijui kuna programu nyengine za ziada za kufanya jambo jipya litakalotoka zaidi ya haya, tunaona bado udhalilishaji upo, unyanyasaji upo lakini zimetengwa

pesa nyengine kama hizi zimeongezeka. Mhe. Mwenyekiti, napata wasi wasi kuruhusu kukupitishia fungu hili sitokuwa tayari hili nilipitishe tu bila ya kupata maelezo yakina kabisa ya matumizi yake ya fedha hizi za *one point seven billion* (1,700,000,000)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kinywa kipana kabisa hili fungu natangaza kulizuwia hili fungu mpaka nipate maelezo ya kina kabisa ya kuweza kuniridhisha mimi na wananchi wangu kwamba tunaruhusu pesa hizi zikatumiwe na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto hapo baadaye tena nitakuruhusu lakini vyenginevyo sitokubali hata kama nitabakia peke yangu wacha nibakie peke yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika suala hilo hilo ya udhalilishaji. Kwa kweli, udhalilishaji Zanzibar upo mwingi na tumeomba unavyopigia kelele lakini inakuwa kama Zimamoto, Zimamoto husiki ving'ora vya *fire* mpaka moto uwake ndio wanakwenda nimeshuhudia nimeona kwa macho yangu kupitia televisheni tuliona kwenye kesi ya mama mmoja aliyechomwa moto Jambiani sijui wapi Makunduchi ulikwenda sijui Makunduchi au Jambiani sijui pahali gani nisije nikasutwa bure, lakini kesi ile imefikia hatua gani hatuzungumzi huko mahakamani lakini tulikuona kina unapo udhalilishaji mstari wa mbele upo lakini hatujui mwenendo wake zile kesi.

Lakini leo hii nathubutu kusemba kwamba kuna kesi moja imekaliwa kidedea na kila mtu ndani ya Baraza hili, imekaliwa kidedea nje na hata na baadhi ya viongozi wa baadhi ya taasisi kesi ya ndugu yangu Kiringo kila mtu anaijua, kila siku matelevision lakini udhalilishaji sio kesi ile tuu kuna kesi nyingi za udhalilishaji mbona hizi hatuzisikii zina tatizo gani au kule kwenye kesi ya Hassan Kiringo ina kitu gani kikubwa kwamba kila siku kwenye vyombo habari, ukiangalia KTV yeye, ukiangalia Sauti ya Tanzania Zanzibar yeye, ukiangalia lakini kuna kesi za udhalilishaji zaidi ya mia moja zinakwenda au kwa siku kesi kumi na tano lakini imeshupaliwa ile tu, nilitaka niseme hii nisieleweke vibaya, isipokuwa nataka nieleweke namna gani tunavyozibagua hizi kesi wengine tunaona tuwape umbele, wengine tuwape unyuma lakini hata katika usimamizi haustahiki hizi kesi zote ni mbaya sote tunapinga udhalilishaji, lakini na hizi nyengine tuzijue zinakoelekea mwenendo wake. Leo hii mtu hata ukimuuliza humu kesi ya Hassan kila mtu anaijua ilipofikia, je, ile kesi ya yule dada aliyechomwa moto kule Makunduchi imefikia hatua gani, hatuijui sisi na tulimuona alikwenda waziri au ile ya mtoto aliyetupwa imefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri yule mtoto mmoja aliyeibia na bandarini alinyanganywa nasikia kwamba yule mama amefungwa miaka mitano, hongereni sana naona mmefanikiwa. Sasa tulikuwa tunataka tujue yale matokeo baada ya kwishakufanya, hatuingilii Mahakama, lakini yale mambo ambayo yaliyozungumzwa baada ya Mahakama sisi tujue. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende katika Idara ya Ustawi wa Jamii kwa kuingilia masuala ya Mahakamani. Tunajua jambo la Mahakamani haliingiliwi lakini wizara yake kupitia idara hii inaingilia masuala ya Mahakama. Napenda nizungumze kuna kesi ya bwana Salum Mohamed Hassan, kesi hii Mhe. Waziri inamgusa sana na anaijua, kwa sababu ni miongoni mwa kesi zilizokuwa ndani ya familia yake na anatoa maelezo. Imeshafikia hatua mpaka mtoto

kubadilishwa baba juu ya kesi hii, lakini kimya na wakasema kwamba ah! Hii kesi iko Mahakama ya Kadhi sio tena Mahakama zetu.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kwani Mahakama ni Mahakama tu na hakuna aliyo na nguvu kuiingilia Mahakama. Suala likishakufika Mahakamani lifate utaratibu lakini kesi iko Mahakama ya Kadhi ameiingilia Mhe. Waziri anasema kesi hii iko Mahakama hii hapa ukatoa *summons* watu wamekwenda kuvunja majumbani wamechukuliwa watoto ni udhalilishaji wa hali ya juu.

Sisi tunapunguza udhalilishaji lakini Mhe. Waziri samahani sana nazungumza kwamba unaendeleza udhalilishaji kwa upande mwengine. Nina ushahidi wa kutosha hapa ninao huu hapa juu ya kadhia zile mpaka *birth of certificate* zilizobadilishwa jina la mtoto. Mtoto baba yake halali anabadilishwa jina anapewa baba siye, na cheti kile ni *fake* hiki hapa hata ku-*forge document* ya serikali Mhe. Waziri hili unalijua. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atapokuja kufanya majumuisho atupe maelezo ya kutosha juu ya kadhia hii, sitonyamaza katika hili kwa sababu ya namna ambayo unavyotumia *interest* katika taasisi hii na kulitamka neno kama hilo. Sasa basi naomba sana Mhe. Waziri katika suala hili la kesi haina haja kwamba ni kesi ya Mahakamani lakini huu mwenendo wake imefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, sina mengi katika kuchangia mchango wangu huu siungi mkono hoja mpaka atakapokuja Mhe. Waziri kunijibu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) kwa siku ya leo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu tuko Ramadhani ya saba, nafikiri panapo majaaliwa tuombe uhai na tuwatakie rehma waliotangulia mbele ya haki na sisi tukumbuke sote humu ndani na walioko huko nje ni binadamu ambao watakuwa mzoga mbele ya haki.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niombe ku-*declare interest* kwa mujibu mimi ni mjumbe halali wa kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, niendelee kumshukuru sana tena sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein na nitafautiane na kauli aliyoitoa Mhe. Haji Omar Kheri kuwa serikali hakunisikia vizuri lakini nilisema wizara yake tu mimi, sikusema serikali. Serikali hii iko makini sana chini ya utawala wa Dkt. Ali Mohamed Shein, tumeona mengi aliyoyafanya na anaendelea kuyafanya na juzi tu nilisema humu kuna jambo linakuja limelishuhudia Baraza la Wawakilishi la zamani kitu kilichotendeka cha kihistoria. Hii ndio nia ya dhati ya Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, tuseme tu kwamba mengi ameyafanya na anaendelea kuyafanya kwa kuwatumikia wananchi wa visiwa hivi viwili Unguja na Pemba bila ya kujali itikadi ya siasa, rangi wala ukabila. Vile vile tumeshuhudia wizara hii anavyoithamini na kuwajali wazee kwa kuwapa posho la 20,000 na shilingi 5000/- ni jambo la kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na nimtakie afya njema yeye na familia yake kwa mambo hayo anayoendelea kuyafanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe lakini bahati siku iliyopitishwa bajeti hii nilikuwa sipo kama kamati, lakini kuna kifungu kimoja kidogo ningekitoa jasho na kisingepita, bila ya kuja kusahau hiki nitahitaji maelezo. Ukurasa wa Q0121, Programu Q0103 Maendeleo ya Wanawake Kupinga Udhalilishaji, SQ010303 zimeingizwa pesa nyingi sana, nilikuwa niko Dodoma lakini hapa ningehitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti makini wa kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali ni Mwenyekiti makini sana na hekima zake zinatumika kwa hali ya juu. Ametusihi sana wakati mwingi tutumie busara zaidi kutokana na umakini wake, hata huko nyuma bajeti kitengo hiki kilikuwa hakina pesa. Jitihada za mwenyekiti zikatumika akaongeza fungu, mwenyekiti nikushukuru sana kwa umakini wako pamoja na Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote wa kamati hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini hizi pesa sio mchezo sijui kama ndio bilioni 1 maana yake hesabu zenyewe sizijui vizuri, bilioni 1,759,250,000. Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hivi vitendo havipungui vinazidi na hizi pesa ni nyingi mno. Wajumbe wamechangia humu kwenye kifungu hiki. Kifungu hiki Mhe. Waziri kitampa kazi sana na kitamsumbua pesa ni nyingi mno. Baada ya vitendo kupungua ndio kwanza vinazidi, hebu tuelezeni kuna nini wizara mmeshashindwa kazi. Baada ya kupungua kelele zote zinazopigwa na sheria kuleta bado vinazidi, hebu tuelezeni mmejipanga vipi wizara. Maana yake isije ikafika pahali nikenda nikateleza Ramadhani hii, waziri hapa *no* mimi kama nilikuwepo siku ile kwenye kamati pasingetosha, hili fungu itabidi tulipunguze Makamu Mwenyekiti naomba hapa tuje tusaidiane na Mjumbe wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohamed Said Mohamed hayupo hili fungu likatwe nusu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna mtu anayefuatilia kuliko kitengo cha *DPP*. Tulikwenda Pemba tulilia sisi machozi, wanapelekewa milioni 3 kwa mwezi tu, ndio pale niliposema wizara hii Mhe. Mohammed Aboud Mohammed Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wizara ipunguzwe. Hayo ni maoni yangu lakini, narudia tena siwezi kuingilia mamlaka ya Rais nitakuwa mtovu wa adabu na heshima ni kitu cha bure. Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kubwa, Pemba Ofisi ya *DPP* inafanya kazi vizuri sana hizi pesa Mhe. Mwenyekiti wa kamati hizi pesa tuombe utupunguzie kabisa apelekewe *DPP*.

Kitengo hiki kinafanya kazi usiku na mchana wala sina mashaka nacho, kesi za udhalilishaji Mhe. Waziri zinazidi kuongezeka pamoja na sheria, hebu tuelezeni chanzo ni nini baada ya kupungua muda wote huu, kelele zote zinazopigwa humu “hoi hoi nacho kilindo”. Sheria kali zinazotungwa hii wizara Mhe. Waziri sitaki kusema mengine sina nia ya kutaka kusema kama imekushinda au vipi aah, sitaki kufika huko rizki mpangaji ni Mwenyezi Mungu. Lakini hapa pana kazi fungu hili mheshimiwa lazima lipunguzwe liende kwa *DPP* kuna matatizo mengi na ndio wasimamizi wakubwa wa kuongoza. Kwa hapa naanza ku-*declare interest* nitazuia fungu hili mpaka nipate maelezo ya kina, vyenginevyo hizi shilingi 1.7 bilioni si kitu cha mchezo mnakwenda wapi Unguja na Pemba tu, vitendo havipungui vinazidi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika nyumba ya kulelea watoto iliyokuwepo Mazizini. Maslahi ya mazingira ya watumishi ni ya kazi ngumu hili sina uhakika nalo kuna harusi inaweza ikawa nzuri au ikawa mbaya. Nyumba ya Mazizini, Welezo na Sebleni wana pesa shilingi 50,000/- katika

mazingira magumu, hizi pesa nasikia zinataka kukatwa naomba zije zirudishwe kama lipo uje unijibu Mhe. Waziri kama halipo nitashukuru Mwenyezi Mungu, ndio jambo la kheri. Lazima tuwatetee kama lipo utanambia lipo kama halipo basi wala hakuna tatizo, mimi ni mmoja wa muungwa na ni msikivu, na hakuna aliyekuwa mkamilifu isipokuwa mmoja tu, hili natetea.

Mhe. Mwenyekiti, nyumba ya kulelea watoto Mazizini Mhe. Waziri inavuja sana. Kwa kweli, hapo kidogo naomba unisikilize sana Mhe. Waziri na watendaji wake waliokuwepo huko juu nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mtoto aliokotwa juzi sijui au lini, sijui kama juzi au miezi mitatu iliyopita aliokotwa mtoto na nasikia jina umembadilisha Mhe. Waziri. Sijui kanuni zinakuruhusu au utaratibu uko hivi au mapendekezo tu umembadilisha, inavyosemekana jina umempa jina lako wewe, sasa sijui utaratibu ukoje. Nitahitaji maelezo maana mimi nikenda nikaota mtoto nikenda nikambadilisha jina tujue ndio sheria zinavyosema au utaratibu. Kuna mtoto yupo pale nasikia jina umembadilisha umemwita jina lake Maudline Cyrus Castico, sasa tueleze ni kweli, si kweli.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Idara ya Kazi hasa wale watumishi wanaotumikia kupata mambo ya ajira, wale vipando vyao kidogo ungewatafutia japo vespa mbili au tatu au pawe pana posho maalum la mafuta. Uwaandalie mazingira ya kazi wale wanaovaa makofia kwa hili wanafanya kazi katika mazingira magumu sana kitengo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu sio mkubwa sana kwa wizara hii kwa vile ni mjumbe sitaki kuisemea sana. Mengi nimezungumza kwenye kamati lakini hili fungu tu Mhe. Waziri aje anielimishe mimi elimu yangu ni ndogo. Mwaka jana Mhe Mwenyekiti alipiga kelele zikaongezwa pesa lakini sijui kama alizitumia zote au sio zote, lakini hii 1.7 mnatupelekesha pahali pabaya. Narudia tena kwa mara ya tatu kesi bado zinazidi muarubaini wake haujafika pamoja na sheria zinazotungwa.

Mhe. Mwenyekiti, juzi niko bandarini ametoka mwanamke Mwanza kaja kaiba mtoto Fuoni ama sikosei, mimi nikataka kuingilia kesi kwenda kumuombea ugomvi nikauliza vipi, nikaambiwa huyajui. Kwa hiyo, akapelekwa kituo cha Malindi hapo hapo nikampigia simu Makamu Mwenyekiti wangu ananishukuru basi hapo hapo akafanya kazi Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo mwenyekiti wangu sikumpata basi nikampigia Makamu Mwenyekiti wangu akafuatilia. Mtu katoka Mwanza kenda kamchukua mtoto wa miezi sita ananyonya kinyonyo cha kudanganyia yuko kwenye boti, hilo tukio nimelishuhudia kwa macho yangu, jina limenitoka tu kidogo nasikia ameshafungwa miaka mitano. Nilikuwa sina habari kama kafungwa, lakini tukiachia jambo hili litazidi ndio pale Mhe. Rais aliposema anawashangaa mawaziri walioganda ofisini, si maneno yangu hayo Dkt. Ali Mohamed Shein anawashangaa mawaziri wanaoganda ofisini gazeti la Zanzibar Leo hili hapa.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Mawaziri msigande maofisini, Manaibu Waziri tunayokukosoweni hapa hatukutakieni mabaya mawaziri wala hatukuja kwa mipasho kuoneshana misuli, wala umwamba. Tuko kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar tunaikosoa serikali ni wajibu wetu. Kutoka mtu akataka kutunisha kifua Mhe. Waziri ah! Twendeni kwa hoja wananchi Mhe. Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili kama alivyosema wanatusikia na wanafahamu tunachokizungumza, wanajua na wanapima, mawaziri jitumeni si maneno yangu haya gazeti hili Dkt. Shein anawashangaa mawaziri wanaoganda ofisini, muda haupo tu ningelisoma hili hapa, jitumeni mawaziri. Ameandika hapo Julai 4, 2014 mawaziri jibuni hoja za wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mhe. Simai Mohamed Said hakujibiwa, Mhe. Hidaya Ali Makame amekaa pembeni hapa akasema nitauliza nini nyongeza, kafanyeni utafiti msikae tu maofisini. Mhe. Rais wa Zanzibar tumshukuru sana tena kakupeni magari ya kifahari jambo la kheri tutampata wapi Rais kama huyu sisi. Kuna watu wameota uwaziri humu ndani hawakuupata neema zake Mwenyezi Mungu na Dkt. Ali Mohamed Shein, tufike pahali msitake kutuhukumu *backbenchers* mawaziri, tujengeni hoja kama alivyosema Mhe. Mohamed Aboud Mohamed wananchi wanatusikia, hiki chombo ni kwa niaba ya wananchi wala sina nia ya kutaka kulidhalilisha jimbo la Ikulu mimi wala viti maalum, mmeni-*quote* vibaya *hansard* ninazo naziheshimu na nitaendelea kuziheshimu, binadamu hujafa hujaumbika, usicheke kilema wakati hujaumbuwa.

Kwa hiyo, Mawaziri jitumeni tusigande ofisini, masuala wanayoulizwa na wajumbe yafanye utafiti yapimeni wajibu wetu *backbencher* kuikosoa serikali, hamuyaoni yote hata timu ya mpira kocha akiwepo juu ndiye anayeona makosa ya mchezaji, mawaziri fanyeni kazi msigande maofisini wala msije mkani-*quote* vibaya gazeti hili hapa. Mawaziri wengine Dkt. Ali Mohamed Shein anazungumza na watu wanakwenda miayo hivi, ni aibu sitaki kumtaja waziri mimi wewe kiongozi wako anazungumza unakwenda miayo. Kwa hivyo, tufike pahali waziri wajibu wao wajue msiwalaumu *backbencher* twendeni kwa hoja, zungumza nizungumze hata Mawakili Mahakamani kule husokatana wakafika nje wakapeana mikono, tusije tukaonekana tuna kiburi hizi nafasi za kupita kesho hazipo. Waheshimiwa muda tu huu na Katiba inatueleza humu tunapewa semina.

Mhe. Mwenyekiti, kazi na wajibu wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi imeandaliwa na Ibrahim Mzee tulipewa darasa hapa mwaka 2016. Kazi na wajibu wa Baraza la Wawakilishi zimetajwa kwa Kanuni kwenye kifungu cha 5a(2) cha Katiba ya Zanzibar kwamba ni kutunga sheria na kuisimamia na utekelezaji wa shughuli za umma *legislative and oversight function*. Halikadhalika kazi kwa wajibu mahsusi wa Baraza la Wawakilishi umeanishwa kwenye kifungu cha 88 cha Katiba ifuatayo ni: Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitajika kuwepo sheria.

Mhe. Mwenyekiti, hili nakuulizeni…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia muda wako dakika mbili nakupa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante dakika mbili hizo hizo Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, pia kujadili shughuli za kila wizara wakati kikao cha mwaka cha bajeti katika Baraza la Wawakilishi moja ya majukumu yetu Mhe. Waziri.

Tatu, kuuliza maswali mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi. Ni wajibu wetu kukuulizeni mawaziri mengine hamuyaoni mnakiri kwa kweli masoko machafu mpaka uvae *rainboot*. Nashukuru kusema ukweli ndio wajibu wetu hamuwezi

kuyaona kadhalika na kusimamia mipango ya maendeleo ya serikali katika njia ile ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa, ndio wajibu wetu *backbencher* na haya mambo leo uko mbele kesho uko nyuma.

Mhe. Mewnyekiti, baada ya maelezo hayo nitahitaji maelezo ya kina kuhusu kesi za udhalilishaji na yule mtoto Mhe. Waziri kumbadilisha jina. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Waheshimiwa Wajumbe nampa dakika tano Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na baadae nampa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa sababu alikuwa na dharura muhimu akimalizia ni Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza na mimi kunipa nafasi kwa muda mchache sana ili kuweza kuyasema na mimi yangu ambayo nimekusudia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pili niishukuru kamati yangu, viongozi wa wizara wote ambao tunaambatana nao katika ziara zetu lakini katika kutekeleza majukumu yetu. Kipekee nimshukuru Mhe. Waziri kwa muongozo, nasaha na mipango ambayo anatupa ili kuona wizara hii na sisi wana kamati tunafanya kazi na majukumu yetu ambayo yanahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema nigusie tu moja kwa moja katika ukurasa wa 25 kuzungumzia mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nianze sana kwa kuipongeza serikali kwa kuweza kuongeza bajeti kwa mara mbili yake ukiachilia mbali bajeti iliyopita ya mwaka jana. Kwa kweli, kwenye hilo serikali tuipongeze sana na tunatambua dhamira njema ya serikali yetu juu ya kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kama mimi ni Mjumbe wa Kamati na yale ambayo tumeyakuta kwenye jamii, tuseme wazi kabisa kwamba dhana ya udhalilishaji bado watu hawajaifahamu. Hawajaifahamu kwamba bado haijafika kwa walengwa husika, kwa sababu mpaka tunavyokwambia Mhe. Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe tunakokwenda jambo la udhalilishaji bado hawalijui. Wanachoamini wao udhalilishaji ni kuharibiwa mtoto, udhalilishaji wa mambo madogo madogo, lakini dhana ya udhalilishaji yenyewe haitambulikani. Kwa hivyo, naomba sana kwa kushirikiana na viongozi wetu, kwa kushirikiana na serikali kama sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni wasemaji wakuu wa wananchi twende kwenye maeneo yetu tukatoe elimu tufahamishe kitu gani udhalilishaji ili tatizo hili tuliondoe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwenye kesi hizo hizo tumekuta matatizo ya kwamba wengi wao wanao-*solve* ni familia zenyewe, wakishakukaa wanapanga kesi hizi zinamalizwa kienyeji, lakini kibaya zaidi hawa wenzetu wa vyombo vya sheria hawatupi mashirikiano mazuri na ya kutosha kwenye kesi za udhalilishaji, hatimaye kesi zetu wanazibadilisha. Kwa hivyo, sisi tuwaombe Ofisi ya *DPP*, wenzetu wa Jeshi la Polisi tushirikiane vizuri kama kesi ya udhalilishaji basi isemwe kwamba hii kesi ya udhalilishaji na kama ya kukashifiwa isemwe hii kesi ya kukashifiwa, wafanyaji wa haya ni sisi Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Pia, niseme kwamba kwenye changamoto hii wenzetu madaktari ushiriki wao ni mdogo sana, ushiriki wao ni mdogo kwa kujifanya wababaishaji. Kesi inasemwa kwamba hii tayari mtu ameshadhalilishwa lakini madaktari wetu wanabadilisha na kusema vitu vyengine. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu atujaalie yasitukute sisi wala familia zetu lakini inasikitisha sana kwenye uadilifu huo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla dakika zangu hazijamaliza niende kwenye ukurasa wa 38, kwenye upatikanaji wa ajira za staha na usalama wa afya kazini. Mhe. Mwenyekiti, bado baadhi ya watendaji wetu hawajaifanyia kazi sera ya ongezeko la mshahara na kima cha chini cha mshahara. Hili kuna baadhi ya mahoteli, baadhi ya wawekezaji wengine bado wafanyakazi wetu wanawalipa mshahara ule ambao wameuzowea mapema. Kwa kweli, elimu ile bado nayo haijafika, lakini kutokana na taratibu ambazo wenyewe wamejiwekea bado wanawadhalilisha wafanyakazi wetu lakini pia wanawasumbua vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya viwanda bado watumishi wetu hawako makini, wanatumwa kazi ya ufuatiliaji badala yake wanawakandamiza vijana wenzetu au wanawakandamiza wafanyakazi wetu kwa kuweka maslahi yao mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kwa pamoja na kwa dhamira njema kabisa na wizara tujaribu kushauriana kwa kina ili kuona hawa watendaji wetu waliokuwa siwaaminifu wapewe kazi ya ziada, lakini kama kunahitajika adhabu mbadala inayowahusu hawa wawajibishwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naenda kwenye ukurasa wa 43, usimamizi wa viwango vya kazi vya kimataifa na majadiliano ya pamoja kazini. Mhe. Mwenyekiti, hapa nizungumzie zile ajira ambazo tunaingia nazo mkataba nje ya nchi ikiwemo nchi za Qatar na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tupate uelewa wa pamoja, kuna baadhi ya hizi kampuni ambazo zimepewa jukumu la kusafirisha vijana, kusafirisha wananchi wetu bado hawana uaminifu na wao. Kijana anakuwa na tamaa, wazazi wanakuwa na tamaa, vijana watoke wende nje wakatafute riziki lakini kuna baadhi ya mianya ya rushwa ambayo inatawala katika mashirika yale. Unaweza ukakuta mtu kuna taratibu ambazo zinatakiwa zifuatwe lakini kupitia njia ya panya zinatolewa zaidi ya shilingi milioni mbili kugharamia safari ile. Kwa hivyo, tuombe sana wana mashirika lakini na vijana wenzetu waelimishwe juu ya uvujaji na kupinga rushwa hii ya kuweza kufanya kazi katika maeneo ya nje.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru baada ya kusema hayo naunga mkonop hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nakupa dakika kumi kwa sababu muda tunauhitaji na Mhe. Waziri ya Elimu na Mafunzo ya Amali aweze kusoma leo *paper* yetu, tumalizie na Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) amalizie.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kwa kunipa dakika za kutosha, dakika kumi zitanitosha na ukitoka nje tuonane nikupe *box* la tende. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi nzito wanazozifanya na kusimamia haki za wananchi na hasa katika sheria hizi za udhalilishaji na mambo ya kufanya jinsia moja kwa watoto wanawake na wengineo. Wamekuwa wakali sana kuhakikisha sheria hizi zinasimamiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nitaomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2018/2019. Nitaanza kuzungumza suala la Nyumba ya Kulelea Watoto iliyopo Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka tujue ukweli nyumba ile ya Mazizini ni ya serikali, ya wizara, au ya mtu binafsi, au ya kampuni, au chochote tu tuje tupewe jibu, kwa sababu undani wa nyumba ile hatuufahamu. Wale watoto kuna vyumba vimefungiwa vimewekwa vitu vya watu wa nje lakini cha ajabu kwamba mpaka leo vitu havijatolewa wizara haitoi jibu kamili kuhusiana na umiliki hasa wa nyumba ile ni ya nani. Lakini vile vile cha kushangaza watoto wale sijui aje atoe sababu atuelezee kwa nini wamehamishwa Forodhani na kuja kuwekwa Mazizini wakati Forodhani pia ni sehemu nzuri ya watoto wale kuweza kutembea, kuogelea, kuona mazingira ya watu tofauti na huku. Sasa tuelezwe ile nyumba imejengwa na nani na mmiliki ni nani. Vile vile aje atuhakikishie kwa *title deed* aje atuoneshe *title deed* ile warka ni wa nani katika nyumba ile.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la unyanyasaji katika makampuni hasa mahoteli, viwanda na mambo mengineyo kwa Wazanzibari au wafanyakazi kwa jumla. Tumesikia na tumeona na tuna ushahidi baadhi ya taasisi kwamba zinanyanyasa Wazanzibari hasa katika viwanda na mahoteli, wamekuwa wanyanyasaji wakubwa hasa wakaazi wa Zanzibar na wazaliwa, wameshazowea kuwaambia Wazanzibari na kuna kipindi iliwahi kutoka kauli hapa kupitia wizara hii kwamba Wazanzibari hawaishi sababu, mara wakipewa kitu hiki hawawezi.

Kwa kweli, mimi nasema uongo, Wazanzibari wanaweza kazi, Wazanzibari wako *fit*, Wazanzibari wamesoma na Wazanzibari pia wako makini kwenye kila kazi na ndio maana ukakuta asilimia 100 au 98 hata Zanzibar tunaendesha wenyewe Wazanzibari hatujachukua Wazungu hapa. Washauri tunao Wazanzibari, Mawaziri Wazanzibari, Manaibu Wazizi na Wawakilishi wote Wazanzibari kwa sababu tunaweza kazi na nchi inakwenda na *GDP Per Capital* ya Zanzibar imepanda na *income source* zote ziko juu kwa sababu kazi tunaweza. *(Makofi)*

Pia, Wazanzibari tuko *fit* vile vile na ndio maana ukakuta tunao wake zaidi ya wawili kwa sababu tuko *fit*, leo anakuja kusema mtu kwamba Wazanzibari hawawezi kazi. Kwa hiyvo, naomba hiyo wizara ije itujibu kwamba wamepita sehemu ngapi au taasisi ngapi kuweza kuzungumza na *management* ambazo zinanyanyasa Wazanzibari hasa katika masuala ya mahoteli na viwanda. Kumekuwa na viongozi katika sekta tofauti wana mtindo mtu anapokwenda kuomba ajira hasa akiwa mtoto wa kike wanamwambia atembee nao kimapenzi ndio wampe kazi na haya mambo yapo. Sasa wizara ije itwambie sehemu ngapi wamewakamata watu wa namna hii au wamekwenda kwenye taasisi ngapi ambazo wamekaa na wafanyakazi kusikiliza matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, nina ushahidi mmoja *Drop of Zanzibar* siku za *public holiday* wao wanawafanyisha kazi watu halafu hawawalipi na hizi *document* nimekuja nazo na baadae maelezo mazuri nitakuja kuwapa wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka kuzungumza ni suala la fedha za kaya masikini. Hivyo, naomba wizara ije inijibu kwamba katika kuhakikisha wanakuza mambo ya kazi na masuala mengine ya wananchi kuweza kujitegemea kiuchumi, wao wamekaa nao kuwawezesha vipi wananchi wangu wa Jimbo la Chaani, kwa sababu wanalalamika kwamba hawawezeshwi na vile vile wakienda wanazungushwa. Sasa Mhe. Waziri akija aje anijibu kwa Jimbo langu la Chaani wananchi wangu wamewasaidia vipi na vikundi vipi walivyowasaidia. Kwa kweli, kuna upande wa Kandwi, Pwanimchangaji, Kinyasini na Chaani wanalalamika sana kwamba hawapitiwi wala hawajui kinaendelea nini wanazungushwa zungushwa.

Jambo jengine naomba wizara hii isimamie mambo haya kikamilifu kwa sababu ukiangalia suala la wanawake na watoto wanaonyanyaswa masuala haya yako mengi. Vile vile, ukiangalia hawa wabakaji wanaoharibu watoto mimi nilipokuwa nikiizungumza hii *point* mnaona Mhe. Nadir Adul-latif labda kaingia na mambo mengine, lakini hawa watu si wa kuishi nao wewe mtu unakwenda kumlawiti mtoto mdogo wa miaka mitao au sita anakwenda kumnajisi mtoto halafu anaachuliwa. Kwa kweli, mimi nashangaa sana wale wazee ambao wamemkamata yule mbakaji hala wanakwenda kufanya naye mazungumzo kwenda kumuachilia. Mzee anapewa shilingi 200,000 anatufa kesi haya mambo ni ya maajabu kabida.

Hata hivyo, wizara haifanyi kazi yake ipasavyo kwa sababu inatakiwa haya masuala wayafuatilie wachukue hatua zilizokuwa ngumu. Kutokana na hali hii, ndio maana napendekeza hawa watu wanyongwe, lakini nikisema hivi nitaambiwa haya mambo ni *human rights*, kuna *human rights* nyengine zinaharibu tusiwasikilize watu wa *human rights* kila siku wanavyotaka wao lazima na sisi tuwe na sheria zetu kali. Kwa mfano, kuna nchi wameweka sheria za kunyonga watu wanaovuta madawa ya kulevya, wanaobaka, wana akili zao wale na nchi ambazo zinafahamu. Lakini, leo sisi kitu kidogo tunasema *human rights* hawa watu wabakaji na watu wengine wasiachiliwe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukiangalia cha kushangaza hapa Zanzibar mwizi wa nazi na ndizi akikamatwa *Wallahi-Laadhiim* anauliwa, lakini anakamatwa mtu aliyebaka, aliyelawiti *red handed* kabisa kakamatwa anaachiliwa. Huyu ndio wa kuuliwa, mtu kama huyu asifike hata polisi, ukiangalia haielekei kabisa mwizi wa nazi anauliwa lakini mbakaji anachukuliwa kituo cha polisi au kwenda kumalizana kesi na wazee, mambo haya tumeona wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nakohoa isije ikafuata ile sheria ya kukohoa, kwa sababu mambo haya ndio kama mnavyoyasikia mtu akikohoa mara kakamatwa. Mimi sijakoholea Waheshimiwa nina matatizo ya kifua nasema kabisa, nikikoholea mtu nina matatizo ya kifua na watu wengi wanajua.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie suala la wizara husika kupitia Mhe. Waziri mwenyewe na ustawi wa jamii, wamekuwa baadhi ya watendaji wanakiuka pia Katiba ya nchi Mhe. Abdalla Maulid Diwani kalizungumza hili suala, mimi nam-*support* hili suala lipo, *documentation* zipo, hata *voice recorded* baadhi ya simu ambazo Mhe. Waziri kapiga

kumpigia mtu kupitia na yeye mwanawe pia ipo, ukiangalia vielelezo vingi vipo. Hakuna haja ya kuzungumza mambo kwa urefu kwa sababu ya muda ni mdogo, lakini ninachotaka kusema kwamba Waheshimiwa Mawaziri mumeaminiwa, lakini anapokuja kuharibu mmoja au wawili inakuwa taswira yote inakuja kuwa si nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kupitia Ustawi wa Jamii na waziri mwenyewe inafika hatua mpaka wanamfundisha mtu apite wapi kwenye njia za kushinda kesi. Mtoto yule kaeleza Mhe. Abdalla Maulid Diwani kabadilishiwa mpaka cheti. Sasa naomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ au Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora wizara zao husika zikamkamate huyu mtu aliyekhushi hiki cheti kwa kubadilishiwa jina la baba yake.

Suala hili, Mhe. Waziri analifahamu huyo mtoto inasemekana ana undugu wa damu kabisa na wanaachilia haya mambo, leo mtu ana heshima zake ni mtu mwenye dini yake, anakuja mwisho kutengezewa mazingira ambayo anaambiwa eti kazaa nae nje wakati cheti cha ndoa kipo, ushahidi wa huyo mwanamke mwenyewe kafungua kesi upo na mambo mengineyo. Hii inaelezea historia vipi wizara inavunja Katiba ya nchi. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote hayo nina nia ya kuzuia kifungu cha Programu ya Ustawi wa Jamii pia kutumia Kanuni ya 111 kuunda Kamati Teule, ili kuweza kuchunguzwa Mhe. Waziri pamoja na kitengo cha Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio tutakuja kujua ukweli wa mambo yako vipi, kwa sababu tayari wizara hii kupitia waziri kuna rekodi zaidi ya mbili ambazo anavunja Katiba na kashiriki na wenzake hasa katika mazingira haya, akiwemo yule mtoto wa mwanzo aliyetoroshwa hilo natoa mfano tu ameshiriki. Suala hili sasa hivi mtoto anabadilishwa jina la baba yake na baba yake yuhai anafuatilia bado watu wanamfundisha njia yule mwanamke vya kwenda ku-*cheat*, ili ashinde kesi na tunawajua wanaofuatilia haya mambo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie Kanuni ya 111 kuunda Kamati Teule, ili tuweze kufanya uchunguzi wa masuala haya na kuyatolea ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba nikushukuru sana na mimi kwa sasa hivi siungi hoja hata asilimia moja, kwa sababu nina mambo yangu mpaka nije niridhike nayo ndio tutakuja kufahamiana hapo mbele. Baada ya hayo nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti ahsante, kabla sijachangia lolote naomba kunukuu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kifungu nambari 144.

> Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 Kifungu nambari 144 kinasema hivi:
>
> > "Utawala bora wa demokrasia ni moja ya vyanzo muhimu katika kuhakikisha taifa linakuwa na utawala unaozingatia sheria, uwazi na uwajibikaji ili kutoa huduma bora katika jamii".

Hii imeandikwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na mimi ni muumini wa Chama cha Mapinduzi. Kwa kuzingatia hilo, napenda nichukue nafasi ya kusema kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiko tayari kuona hoja ya udhalilishaji ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nakuomba ukae kidogo nampisha Mhe. Spika, ili aweze kuendelea. Mhe. Spika karibu.

(Hapa Mhe. Spika alikalia kiti)

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, naomba tuendelee.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi hii na sasa naendelea. Nilitaka niseme kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiko tayari kuona hoja ya udhalilishaji katika visiwa vya Unguja na Pemba inaendelea kwa kasi kama hivi ambavyo inaonekana. Vile vile, Wizara hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto imekuwa mstari wa mbele kuzuia harakati hizi, ili zisiendelee na tumeona juhudi zao sehemu mbali mbali wanazozifanya katika kuzuwia udhalilishaji. Sikatai kama hakuna changamoto, lakini jitihada ambayo inaoneshwa na wizara hii lazima Wazanzibari tuchukue nafasi ya kusema kwamba tumepiga hatua kubwa katika kuzuwia udhalilishaji katika nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kwa Mhe. Waziri kwamba sasa umefika wakati yeye pamoja na kamati yake maalum ambayo labda ataiunda awe anafanya ziara katika mikoa yetu ya Unguja na Pemba kila mwezi mara moja, ili kuona ni kesi ngapi zimefunguliwa katika vituo vya polisi na kwa nini zimechelewa, ili kuifanya serikali isiingie katika lawama ya hoja kama hizi.

Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba Serikali ya SMT na Serikali ya SMZ inajidhatiti katika kuzuwia hoja hii ya udhalilishaji kwa Watanzania wote. Sasa kama kuna watu ambao kwa makusudi wanachukua utaratibu huu wa kudhalilisha basi na serikali zote mbili zitapambana na watu hao. Hatuko tayari kuona hoja hii inaendelea, tunatoa wito kwa madaktari, tunatoa wito kwa maaskari wanaokamata kesi hizi wahakikishe kwamba wanafanya wajibu wao katika mazingira ya kuifanya serikali ionekane mbele ya jamii inafanya kazi yake. Sasa kama kuna mtendaji ama polisi au daktari hataki kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi aache kazi mara moja. Kwa kweli, sisi tumetumwa na wananchi kuja kukaa humu na kuwatungia sheria pamoja na kuwasimamia sheria, ili waweze kupata haki zao zinazowajibikia.

Sasa ni jambo la kusikitisha sana, kuona kwamba kesi zinapelekwa lakini zinakosa ushahidi na ushahidi unakuwa upo. Lakini kwa nini haziendi Mahakamani inakuwa sasa serikali inaingia katika lawama kwa visingizio vidogo vidogo.

Kwa hivyo, Wizari hii ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto lazima tuisaidie kwa nguvu zote na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sisi kama viongozi tulioletwa na wananchi basi tuwe tayari kuyafichua haya na pahala pazuri pa kuyafichuwa haya milango ya mawaziri wote iko wazi unapoliona tatizo kama hili ni lazima usingojee Baraza la Wawakilishi nenda kwa waziri yoyote umpe taarifa kakusiliza sawa hakukusiliza Mawaziri Wasiokuwa na Wizara Maalum wapo tutafikisha hoja hii kwa Mhe. Rais wa Zanzibar wakati wowote mkituletea hoja kama hizi sisi tutafikisha hoja hizi kwa Rais na tutaanzia kwa Makamu wa Pili wa Rais

kwani ndie Mtendaji Mkuu wa Serikali. Sasa leo kuja kusikia hoja kama hizi Wazanzibari zinasikitisha sana wakati serikali yenu ipo viongozi wenu wapo, milango iko wazi ni jambo la kusikitisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wawakilishi hii Serikali ni ya Chama cha Mapinduzi na wao wameletwa na Chama cha Mapinduzi na Chama cha Mapinduzi inataka tena kushindana 2020. Sasa je, serikali hii hatutaki kuona mbadala wa serikali, serikali yetu ni hii 2020 serikali ni hii hii. Maana ninaamini kwa maneno yalioandikwa humu 2020 hakuna *CUF* hapa. (*Makofi*)

Nakiomba Chama cha Mapinduzi kupitia Baraza la Wawakilishi wachapishe vitabu hivi kwa wingi sana wavitoe wananchi wasome, ili waone ule uhalisia wa mambo ya Zanzibar yalivyokuwa yanatakiwa kufanywa humu. Si hoja kungojeana humu tukaja tukapakana matope tukaipaka serikali matope kwa dhamira eti za kukomoana. (*Makofi*)

Hii ni Serikali ya Mapinduzi na lazima tudumishe Mapinduzi, lazima tudumishe Chama cha Mapinduzi ndio hakina mbadala. Chama cha Mapinduzi ndicho kinachoongoza nchi na naendelea kuwaambia siku zote na nitaendelea kuwaambia kwamba hivi vyama vyengine vidogo vidogo AFP, CHADEMA na vyenginevyo ni vidumbaki kwenye beni, vikilia beni litalia, visilie beni litalia. (*Makofi*)

Sasa, nyinyi mnakwenda kuhangaika halafu mnakuja huku mnalalamika. Sikilizeni bwana tumeletwa humu na wananchi kuwatumikia na kuna wengine humu wanakaa wanasema aah! Yule kwa nini harudishi kadi ya CCM mnanijua historia yangu mimi. Mimi nimeanza kutumikia Chama cha Mapinduzu nyinyi mko skuli wengine, wengine hamjajua hasa nini maana ya uongozi. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Muongo!

Mhe. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Leo, mkija kumuona mtu anatetea chama anatetea Mapinduzi. Tunatetea Mapinduzi yetu na bila ya Mapinduzi tusingeingia humu tusidanganyane, isiwajie imani kwamba labda nyinyi mmekuja humu kutokana labda ya bidii zenu na akili zenu, Mapinduzi ndio yaliyowaleta humu na Mapinduzi yalifanywa na Chama cha Ukombozi cha *Afro- Shirazi* na Chama cha Ukombozi cha *Afro-Shirazi* kimefanya mbadala wa jina sasa iitwe CCM. Sasa hii CCM ndio chama cha Ukombozi sasa leo tukija humu tunakomowana tunafanya nini tunawapa nafasi wapinzani huko wanaotaka serikali. Hii serikali ni yetu...

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, una dakika mbili.

Mhe. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, ahsante naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf.

UTARATIBU

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Spika, nasimama kwa Kanuni ya 59(3) mtu kuzungumza mambo yasiyofaa. Mhe. Spika, tupo haja kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za nchi Waheshimiwa wote Wawakilishi tunazungumza kwa niaba ya wananchi na sisi ndio wa kuyasema hayo kwa sababu sisi ndio tumetoka kupitia Chama cha Mapinduzi sio yeye na tunachokiongea tunaakili zetu kwamba tunaongea sisi tukiwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi.

Sasa Mhe. Waziri azungumze mambo ambayo anapaswa yeye kuzungumzia na asituingilie sisi mawazo yetu, maoni yetu na ushauri wetu katika serikali na suala hili tumeliona kwamba yeye ni katika waziri peke yake anaejaribu kuwaangilia Waheshimiwa Wawakilishi kuvunja Katiba na Kanuni za Baraza la Wawakilishi kutufundisha tuzungumze nini.

Sisi haweza kutufindisha yeye wala mwengine tuongee nini, tunazungumza kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, tunaomba muongozo wako na ajirekebishe na iwe hili suala ni mwanzo na mwisho.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona mapema sana mnaanza kuwa wakali sana. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nadhani Mhe. Soud Said Soud (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) sikuona huo uzito kwamba alikuwa analazimisha kwamba analazimisha lazima muongee kama anavyotaka yeye, mko huru Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa Kanuni changia unavyoweza, changia unavyopenda yeye mwache azungumze hivyo anavyozungumza Mheshimiwa isikuguse kiasi hicho.

Kwa hivyo, wewe fanya shughuli yako wananchi wako wamekutuma wanakusikia, nafikiri hamna tatizo hamna haja ya kuvutana Mheshimiwa umefunga kwanza. Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea. Mhe. Waziri wa Afya nitakupa uongee kuhusu suala la *DNA*.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nikushukuru kwanza naomba niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu tunaendelea na Mfungo wa Ramadhani *Alhamdulillah*.

Pili nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri na naamini kabisa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wataiunga mkono.

Mhe. Spika, nilikuwa nasema suala la *DNA* lakini naona niseme jambo moja. Kwamba suala la udhalilishaji ni suala la mtambuka. Mtambuka linaanzia toka kwenye familia kwenye jamii yenyewe kwenye mila na desturi, kwenye dini zetu lakini vile vile kwa taasisi zetu mbali mbali. Kwa hivyo, sote tuna wajibu kabisa kusimama kidete kuona hili jambo si la wizara moja au la waziri ni jambo la mtambuka ni jambo la kila mmoja wetu tunahitaji kulisimamia kwa pamoja.

Mhe. Spika, sisi ambao tumetoka huko nyuma zamani tulikuwa tukiona shilingi ikianguka hapa mjini ilikuwa inaokotwa na inapelekwa polisi, mtu kaokota shilingi anapeleka polisi, kwa sababu

uadilifu ulikuwa mkubwa na imani ya dini ilikuwa kubwa na hili lazima tulikubali kwamba imani imepungua sana. Ndio maana mtu anaweza akadhalilishwa na mtoto mdogo kwa sababu hiyo. Kwa hiyo, nasema ni suala la jamii tulichukulie kama ni jamii tunahitaji kupambana nalo kwa nguvu zetu zote.

Pale tunapoona mwenzetu anahusika na taasisi fulani hakutekeleza wajibu wake tumshughulikie yeye kama yeye ni mmoja tusi-*generalize* suala. Suala ni tatizo kubwa sana wala si tatizo dogo hata kidogo. Kwa mfano, leo unamkuta Shekhe au Padri anafanya, yaani yule mtu unaemtegemea asifanye vibaya ndio anafanya vibaya. Kwa hivyo, nasema ni suala la maadili ambayo yamebadilika sana tunahitaji kusimama kidete kupambambana nalo kwa nguvu zetu zote. *(Makofi0*

Kwa kweli, niseme kwamba nimshukuru sana Mhe. Waziri amehangaika sana anajitahidi sana masikini ya Mungu anatoka usiku saa nyengine anakwenda wakati wa mvua mimi nimeshamkuta nae katika sehemu mbali mbali anahangaika na hili jambo, lakini si jambo la peke yake ni jambo letu sote lazima tusimame kidete.

Tukikuta madaktari hawafanyi vizuri tuwaseme kabisa wala tusione haya, lakini na wanaofanya vizuri tuwaseme na wao wanaofanya vizuri anaefanya vibaya tumshughulikie mtu yule ambaye anaefanya vibaya, hii ndio *concern* yangu kubwa na naomba nikubaliane nao kabisa kabisa kwamba wako wanaofanya vizuri tuwaseme, wanaofanya vibaya tuwashughulikie kwamba wanafanya vibaya mimi hilo halinipi shida hata kidogo na ndio maana tumekuwa kila wakati tunapita mahospitalini, tunapita kila pahala kuhakikisha kabisa wananchi wanapata huduma zinazotakiwa, mawaziri wote wanakwenda kwa wananchi kufanya shughuli zao. Kwa kweli, kama hatufanyi hivyo Mhe. Spika, ushahidi tusingekuwa sisi leo na Bajeti Tegemezi ya asilimia saba kutoka thalathini kama si jitihada hii ya mawaziri wote waliofanyakazi na Mhe. Rais wetu na muongozo alioutoa tusingefika huku.

Tusingefika bajeti ya kujitegemea kiasi hichi leo *donors* wametuacha mkono tunajitegemea. Bajeti tumetoka *eight hundred million to one point two trillion* tumejitegemea tumefika hatua nzuri sana tusijione kwamba hatujafanya kazi, tumefanya kazi kubwa nzuri tunahitaji tunahitaji kuilea kazi hii, ili ilete matunda kwa watu wetu niseme hilo la kwanza.

Pili Mhe. Spika, baada ya serikali kuona kwamba taasisi peke yake hazitoshi ndio maana serikali baada ya kupata ushauri wa ndugu zetu Wawakilishi kwamba sasa iagizie *DNA machine* na nataka nitoe taarifa rasmi kwenye Baraza lako kwamba pamoja na kwamba kwenye hotuba hii tutakuwepo. Kwa hivyo, *DNA machine* itaagiziwa *process* zote za tenda zishakamika mtu anaetakiwa kuleta keshapatikana, kitu cha kucheleweshe kidogo ni kupata taaluma ya ndani ya *DNA* na ni moja tulijifunza tulikwenda kwa wenzetu Dar-es-Salaam ambayo wanayo tayari. Tumekwenda na nchi nyengine mbili kutafuta utaalamu mbali mbali, utaalamu umepatikana na tenda imeshafunguliwa na mtu ameshakuwa tayari wakati wowote yoyote mashine itaweza kufika na kufungwa na kufanyakazi.

Lakini *DNA* ni jambo moja nasema bado suala la maadili ni letu sisi wenywe, kwa sababu kwenye *DNA* ukisoma *literature* yake inasema ina *ponsen and conse* hiyo *DNA* yenyewe ni mashine haijui inapelekewa nini. Kwa hiyo, kama mtu kapeleka kitu sicho mashine kitarudi kile

ambacho kimepokea. Kwa hivyo, nasema suala la maadili ni jambo la msingi sana na lazima tulisimamie kikamilifu.

Kwa hiyo, nataka niwatoe wasi wasi Waheshimiwa Wawakilishi kwamba serikali imesikia kilio chao cha wananchi kama inahitajika mashine ipatikane, itapatikana. Lakini mashine kama mashine haifanyi kazi bila ya binaadamu. Suala la binaadamu bado liko pale pale huyu binaadamu anaweza kuchukuwa damu ya mtu mwengine akapeleka pale, akachukuwa na ya mtu mwengine akaipeleka pale tumeshayakuta hayo. Suala la uaminifu na uadilifu ni suala la msingi sana. Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wanawake na Watoto: *Bismilah Rahman Rahim*. Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi kwa mwaka wa 2018/2019.

Mhe. Spika, mchango wangu mimi utalenga sana katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wawakilishi ambazo walitaka kupata ufafanuzi. Lakini kabla ya kutoa majibu Mhe. Spika, namuomba Mwenyezi Mungu anipe utulivu, anipe hekima na busara ili tuweze kuwajibu Waheshimiwa Wawakilishi na hatimae waweze kutufahamu vizuri na baadae waweze kutupitishia bajeti yetu hii ili tukaendelee na kazi zetu kama tulivyopangiwa.

Mhe. Spika, kwa kuanza naanza na Mhe. Omar Seif Abeid pamoja na Mhe. Abdalla Maulid Diwani kuhusu sheria iliyopitiwa imekuwa bakora au kandamizi kwa upande mmoja hasa pale inapotokea haki ya kutofahamiana.

Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba hakuna sheria kandamizi ila sheria imetungwa kwa ajili ya kuimarisha utawala bora wa sheria pamoja na kuondoa vitendo vya ukatili na udhalilishaji njinsia ya wanawake na watoto.

Aidha, sheria hii hamlengi mwanamme ila inalenga watu wote wa aina na lengo la kulinda haki na ustawi wa wananchi wote. Kwani misingi ya sheria ni kwamba haipingani na sheria nyengine zilizopo. Lengo la sheria hii ni kumlinda mwanamke na mtoto dhidi ya madhila na mateso ya udhalilishaji bila kujali umri alionao. Sheria imeanzimia kuondoa kero na vitendo vya udhalilishaji na bughuza kwa watoto pamoja na wanawake sambamba na kuleta heshima kwa wanawake na watoto wetu kuzingatia silka na maadili yetu ya Kizanzibari.

Mhe. Spika, kuhusu fedha za udhalilishaji kuongezeka kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hili Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Mhe. Hamza Hassan Juma na Waheshimiwa wengine Mhe. Spika, kwa sababu hatutokwenda moja kwa moja ikiwa Mheshimiwa aliingia huku basi na yeye tunamuomba aridhike na jibu hili ambalo tutalitoa.

Programu hii ya kuimarisha Mapambano hayo. Serikali imechangia Milioni Mia Mbili (200,000,000) fedha za kawaida na Milioni Mia moja na sitini na saba, Mia saba na Hamsini na saba (167,757,000) kwa ajili ya mishahara. Pia, Washirika wa Maendeleo wamechangia ikiwemo *UNFPA* Milioni Mia Mbili (200,000,000), *UNICEF* Milioni Mia Tatu (300,000,0000), *UNPD* Milioni Mia Tano Hamsini na Nane, Mia Moja Sitini na Nane (558,168,000) na *UN Women*

Milioni Mia Tatu (300,000,000). Fedha hizi zimeongezeka kutokana na kuwepo na utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano wa Kupinga Ukatili na Udhalilishaji pamoja na utekelezaji wa Programu za kumwendeleza na kumwezesha Mwanamke

Mhe. Spika, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kuhusu kuongezeka fungu la Prgramu ya uzalishaji wa mwaka 2017/18. Mhe. Spika, wizara ilitimiza kilio cha Waheshimiwa Wawakilishi kwa kuliongeza fungu la Prgramu ya udhalilishaji kutoka milioni hamsini na tano hado milioni mia moja sabini na tano kwa mwaka wa fedha 2017-18 ambapo uchanganuzi wake ni kama ifuatavyo:

Milioni hamsini na tano ni matumizi ya kawaida kutoka serikalini, milioni thamanini zimetoka Shirika la *UN FPA* na milioni arubaini kutoka *UNICEF* kama inavyojionesha katika kitabu cha Makadirio na Mapato ya Matumizi ukurasa wa Q01-21 katika fungu la SQ010202 fedha hizi zimetuka kwa uzinduzi wa mpango wa miaka mitano kuimarisha utaratibu na mapambano kuwajengea uwezo viongozi wa dini na kamati za Shehia na kufanya tathmini ya muamko wa jamii katika mapambano hayo. Naomba Waheshimiwa wafahamu mpango huo na kusimamia utekelezaji wake.

Mhe. Spika, kuhusu tofauti baina ya fedha zilizopitishwa na zilizopo katika kitabu. Mhe. Spika, fedha hizi zinaonekana kuwa ni tafauti kutokana na kuwa baadhi ya fedha zimeripotiwa katika fungu kuu Pemba kiasi cha shilingi milioni ishirini na nane laki nane thalathini ambazo ukijumlisha na Unguja unapata milioni mia moja sabini na tano na laki moja.

Vile vile, kuhusu kuendelea kukithiri kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji. Mhe. Spika, wizara inakiri kuwa vitendo vya udhalilishaji vinaendelea pamoja na juhudi za wizara ya serikali juhudi zake wizara imekuwa ikifanya kazi karibu na jamii kuanzia ngazi ya shehia wakiwemo Masheha kudhibiti hali hatarishi zinazopelekea vitendo hivi. Wizara inawapongeza Masheha wengi ambao wao pamoja na waratibu wa Shehia wanatoa mashirikiano makubwa kwa wizara.

Suala la Wilaya ya Kati kuhusu mtoto aliekufa. Wilaya ya Kati ni kawaida ya kukutana kila wiki mara moja siku ya Jumanne kujadili masuala mbali mbali yanayohusu shehia yao. Pia linapotokea tatizo la udhalilishaji tunaanzia kwa sheha wa shehia husika tunashirikiana naye kulitatua suala husika. Aidha, wizara imeshiriki kwa kutoa pole kwa wahanga wa tukio hilo kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa kila wakati, ili kuimarisha utendaji na utoaji wa huduma za jamii.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kuhusu vikundi mia moja ishirini na mbili vya wanawake vilivyofanyiwa utafiti vinaonekana vina nini. Mhe. Spika, vikundi hivi vimeunganishwa na fursa mbali mbali kama tulivyoeleza ukurasa wa 24 *bullet* ya kwanza. Kuhusu kuelimisha wanawake kujua sheria na taratibu za kuliki ardhi na haki zao nyengine. Mhe. Spika, wizara imeelimisha wanawake juu ya haki zao kupitia Vyombo vya Habari na mikutano mbali mbali ya kuelimisha vilivyopangwa. Hata hivyo, tunachukuwa ushauri wa Mheshimiwa na umuhimu wa kuwaelimisha wanawake juu ya umiliki wa ardhi.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kuhusu kuweka utaratubu wa kuwastarehesha wazee. Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba wizara imeweka utaratibu wa kuwastarehesha

wazee wanaokaa makaoni kwa kuwafanyia burdani za aina mbali mbali ikiwa ni pamoja na kwenda matembezi, kariakoo kupanda mapembea na vikundi vya burudani kama tarabu vinakwenda kuwatumbuiza hilo ni jambo la kawaida. Lakini vile vile tunamkaribisha Mhe. Mwakilishi kama kuna aina nyengine pia tuko nae tutampokea tushirikiane naye katika kuwastarehesha wazee wetu.

Mhe. Suleiman Makame Ali kuhusu omba omba wanaotoka Tanzania Bara kuweka katika makao ya wazee. Mhe. Spika, naomba kumjibu kuwa suala la omba omba wanaotoka Tanzania Bara kupelekwa nyumba ya wazee ushauri wake tumeuchukuwa na tutaifanyia kazi ingawa wizara inasisitiza kuwa wazee walelewe ndani ya familia zao ili wapate mapenzi ya watoto wao na jamii. Pia, napenda kumuarifu kwamba wengi wa omba omba hao ni watu wanajiweza, hivyo tunawashauri watafute shughuli za kufanya ili waweze kujikwamua kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuchukua mikopo kujiendeleza.

Hata hivyo, napenda kumuarifu kuwa wizara inawasaidia wale wazee ambao hawana familia hawajiwezi kabisa, ndio tunawachukua na kuwahifadhi katika makaazi ya wazee baada ya kufanyiwa tathmini maalum ya kujiridhisha kwa mujibu wa vigezo vyetu.

Mhe. Masoud Abrahaman Masoud kuhusu ongezeko kuongezeka pencheni kwa wazee. Kutathmini juhudi za serikali kupitia Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein za kuendeleza kuwasaidia wazee, ikiwemo kuwapa pencheni. Napenda niwajulishe kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar anapenda sana kuongeza pencheni ya wazee, lakini kutokana na hali ya uchumi wa nchi kwa hivi sasa hatoweza kufanya hivyo hadi uchumi wa nchi utakapoimarika. Napenda kutoa wito kwa wananchi kwa kulipa kodi inayostahiki, ili tuweze kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kufaidi matunda yake.

Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu sababu gani za kutokulipwa kwa wazee 2,060. Mhe. Spika, napenda kumjibu kwamba hawa ni wale wazee ambao hawajafika vituoni kulipwa kutokana na sababu mbali mbali, ikiwemo wazee waliofariki, waliosafiri nje ya nchi na wengine watoto wao wanachelewa kuja kuwachukulia fedha zao.

Mhe. Rashid Makame Shamsi, kuhusu kuwalipa wazee waliofariki. Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mjumbe kuwa wizara huwa inafanya ukaguzi wa mpango wa pencheni kila mwezi na iwapo inagundua kuna watu ambao wamefariki au hawakutimia umri basi inafanya uhakiki na kuwaondoa katika mpango. Pia, naomba kuwasisitiza masheha wawe wanaripoti na mapema kwetu, wale wote ambao wako katika mpango na wamefariki.

Vile vile, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe watupe taarifa za wazee waliofariki katika maeneo yao na wanaendelea kupewa pencheni ili tuweze kufuatilia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ....

Mhe. Spika: Dakika tano unazo Mhe. Naibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, kuhusu vijana wanaofanya kazi nchi za nje. Napenda kumjibu Mhe.

Mwakilishi kwamba ushauri wake wa vijana wanaofanyakazi nchi za nje umepokelewa. Aidha, mashirikiano yameboreshwa baina ya wizara na Balozi zetu nchi za Mashariki ya Kati, juu ya usimamizi wa mikakati ya kazi wanaokwenda kufanyakazi katika nchi hizo.

Mhe. Maryam Thani Juma, kuhusu kupungua kwa viwango vya mapato, kupungua kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mhe. Spika, ni kweli kuwa mapato ya wizara yamepungua, hii ni kutokana na masuala ya ugawaji wa viwango vya mapato, ni jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango, ambapo wizara inapewa kikomo na kupanga kwa mujibu wa uwezo wa chanzo husika cha ukusanyaji.

Pia, baadhi ya vyanzo vya mapato vinaondoshwa kama vile ada za mafunzo kwa wajasiriamali na ada ya ushirika imepungua, kwani lengo la serikali ni kuwainua washirika na wajasiriamali na sisi na sio kuwakomoa kwa ada. Kwa hivyo, serikali imeona mchango huo, hata hivyo ushauri wa kamati kwa wizara kuongeza vyanzo vya mapato tutaufanyia kazi.

Kamisheni ya Kazi. Mhe. Masoud Abrahman Masoud, kuhusu baadhi ya wafanyakazi wanaolipwa shilingi 150,000 badala ya shilingi 300,000, lakini wanadhalilishwa wafanyakazi wao. Mhe. Spika, tunashukuru kwa kupata taarifa hiyo, ambayo itaongeza kasi katika ufuatiliaji wa kazi zetu, ili tuweze kufuatilia kwa mujibu wa suala hili. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mwakilishi ni vyema akatusaidia sisi kwa kutupatia orodha ya taasisi hizo, ili tuweze kuzifuatilia na kuchukua hatua zinazostahiki.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, vigezo gani vimetumika kutambua udogo na ukubwa wa taasisi kuhusu ulipaji wa kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi. Mhe. Spika, napenda kumjibu kwamba kwa mujibu wa kanuni kampuni au taasisi inatambulika kuwa ni taasisi ndogo ikiwa inamilikiwa na mzawa au mtu sio mwekezaji wa kigeni. Pia kampuni au taasisi hiyo isiwe na zaidi ya mfanyakazi mmoja anayelipwa shilingi milioni moja au zaidi kwa mwezi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi, kuhusu suala la Kampuni ya Upendo. Suala hili tunalikubali kuwa kampuni hiyo inawalipa wafanyakazi wake shilingi 180,000. Watendaji wangu wameligundua hilo na kuitaka taasisi hiyo ilipe kima cha shilingi 300,000. Hata hivyo, mwajiri wa taasisi hiyo amewasilisha ombi rasmi kwa Kamishna wa Kazi anaomba kutambua kuwa taasisi ni ndogo ili aweze kulipa shilingi 180,000 kwa mwezi.

Kuhusu UMAWA, kampuni hiyo imekidhi vigezo vya kuwa taasisi, hivyo inatakiwa kulipa kiwango cha mshahara cha shilingi 180,000.

Kuhusu wafanyakazi wa Kampuni ya Jendele maafisa kazi kutoka Kamisheni ya Kazi wamefatilia kwa kina suala hilo tayari na hivi sasa kampuni hiyo tayari imeshaanza kulipa kima cha shilingi 180,000/= kampuni hiyo ni ya kizalendo.

Mhe. Omar Seif Abeid, kuhusu maradi wa mboga mboga, Mhe. Spika napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba wizara imefanikiwa kupata fedha za mboga mboga kutoka shirika la misaada la Marekani baada yakuandika mradi wa kuwasaidia wakulima wa mboga mboga kiasi cha shilingi milioni 330 kwa ajili ya kuwapitia mikopo wakulima hao. Mfuko wa Uwezeshaji unasimamia utoaji wa mikopo hiyo kwa kushirikana na Wizara ya Kilimo na Jumuiya ya

Wakulima Tanzania, pia mradi huo unasimamiwa na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Mgeni Hassan Juma nafasi za wanawake, kuhusu kuongezeka kwa viwango vya mikopo Mhe. Spika waombaji wa mikopo hawawepi kiwango cha mikopo isipokuwa viwango vya mikopo vinavyotolewa na mfuko hutegemea mahitaji wa miradi wanayoomba. Mhe. Spika naomba hili kidogo nitolee ufafanuzi, waheshimiwa wengi wamekuwa wananalamika kwamba watu wanapoomba mikopo tunawapa pesa kidogo.

Mhe. Spika, pesa tunazozitoa ni kutokana na kwamba yule mkopaji ameomba kitu gani. Kwa mfano, wakati mwengine mtu anakuja pengine anaomba shamba, lakini shamba lake pengine shida yake ni maji pengine hana *pipe* au *motor* tunasema kwa hivyo, sisi tunapiga tathmini ya ile *motor* nikiasi gani tunampa ile pesa ya *motor* kwenda kununua, lakini sio kama Waheshimiwa wengi walivyodai kwamba watu wanapoomba mikopo wanapewa kima kidogo, itagemea na yeye mwenyewe ameomba kiasi gani kutokana na mradi wake anaofanya.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, muda wako umemalizika naomba uunge mkono hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, naomba kuunga mkono haja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto aje ahitimishe hoja yake. Mhe. Waziri, unayo saa nzima ya kuhitimisha.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. kwa heshima na taadhima Mhe. Spika, kwanza nimefarajika kwamba upo hasa sasa hivi na nawashukuru wale wote waliosadia kufanya shughuli hizi tangu asubuhi. Lakini pia nipende kuendelea kuwapongeza kwamba suala zima la kuendelea na mwezi wa Ramadhani Mwenyezi Mungu aendelee kuwatia nguvu na kuwaendeleza sala nyingi sana, ili katika maombi yenu yatakayokuwa ni maombi, mambo mengine kwenye wizara yetu hayafunguki pasipo maombi ya watu wengi kwa jumla. (*Makofi*)

Kwa hivyo, nawasihi sana mtakapokuwa naomba katika sala zenu ongezeni na suala la wanawake na watoto na udhalilishaji na masuala mengine ambayo yamekuwepo, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyaeleza. Kwa niaba ya Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto napenda kukushuru wewe mwenyewe Mhe. wa Baraza lako tukufu waliochangia hotuba ya bajeti ya wizara moja kwa moja au kwa maandishi.

Jumla ya wajumbe 17 walichangia moja kwa moja na wajumbe 12 walichangia kwa maandishi. Pia napenda kumshukuru Mjumbe wa Kamati ya Habari, Utalii na Maendele na Wanawake aliyesoma hotuba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Ali Suleiman Ali kwa kuipongeza wizara kwa kutupa ushauri busara na maelekezo katika kuimarisha ufanisi wa kazi zetu.

Tunamuahidi kuwa ushauri na maelekezo waliyotupa tutayafanyia kazi kwa ajili ya kuleta maendelea ya nchi yetu kwa uaminifu na uadilifu. *(Makofi)*

Aidha nawashukuru Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kipindi chote hichi cha kutupa ushauri na maelekezo katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa ufanisi mkubwa. Ushari tunaupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia hotuba ya bajeti ya wizara yangu ni kama wafuatao:-

Kama watatokea wengine sijawataja mnaweza kunilitea kwa sababu wengine wemeleta dakika ya mwisho. Mhe. Waliochangia moja kwa moja ni

1. Mhe. Maryam Thani Juma (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.
2. Mhe. Suleima Makame Ali
3. Mhe. Hussen Ibrahim Makungu
4. Mhe. Omar Seif Abeid
5. Mhe. Massoud Abraman Massoud
6. Mhe. Mwanasha Khamis Juma
7. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
8. Mhe. Suleiman Sarahan Said
9. Mhe. Panya Ali Abdalla
10. Mhe. Amina Iddi Mbarouk
11. Mhe. Hamza Hassan Juma
12. Mhe. Abdala Maulid Diwani
13. Mhe. Simai Mohammed Said
14. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
15. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma
16. Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf
17. Mhe Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
18. Mhe. Waziri wa Afya.

Waliochangia kwa maandishi, nasema kama kuna mmoja tumemshau naomba nilitewe kwa ajili ya kuweka *hansard* sawa sawa kwa kuwa wengine wameleta mwishoni.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Rashid Makame Shamisi
3. Mhe. Mussa Ali Mussa
4. Mhe. Harusi Said Suleiman
5. Mhe. Tatu Moh'd Ussi
6. Mhe. Shaib Said Ali
7. Mhe. Panya Ali Abdalla
8. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
9. Mhe. Salama Mussa Bilal
10. Mhe. Muhammed Mgaza Jecha
11. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame

Mhe. Majibu mengi naibu ameweza kujibu, naomba niendelee na Mhe. Panya Ali Abdalla, yeye alitaka kuhusu elimu kwa wakopaji Mfuko wa Uwezeshaji una utaratibu wa kuwapa elimu waombaji wote kabla ya kupatiwa mkopo yao, pia huwa inafuatilia mwenendo wa biashara na mtu aliyepewa mkopo na kumpa ushauri wa namna ya kuimarisha biashara zake.

Wajasirimali wanaopatiwa mafunzo huongeza ufanisi katika kuendesha biashara zao pamoja na kukuza ubora wa bidhaa wanazozalishwa hali hii huongeza vipato vyao na kuweza kurudisha mikopo kwa wakati pia huimarisha na kipato cha wajasirilia mali waliopewa tu kinachangia katika ukuwaji wa uchumi katika nchi na pia kukidhi mahitaji katika familia zao.

Mhe. Rashid Makame Shamsi, kuhusu kwa nini kila mwaka fedha za mikopo ni shilingi milioni 600 kwa wakopaji 600. Mhe. Spika, shilingi milioni 600 ni fedha zilizochangwa tokea kuanzishwa kwa mfuko huu ambazo ziko benki na zinatumika kutoa mikopo kwa wananchi wanapoomba, wananchi wanatakiwa kuzirejesha fedha hizo kwa wakati, ili waweze kupewa wakopaji wengine ili kuziongeza fedha hizo mfuko unatikiwa kutafuta vianzio vyengine vya mapato kama hiki cha mradi wa mboga mboga.

Kutokana na uwepo wa mradi wa mboga mboga na matunda mfuko umepata kiasi cha shilingi milioni 300 ambazo fedha hizi zitakuza mfuko hadi kufikia shilingi milioni 900 na hatimae viwango vya mikopo vitapanda. Mhe. Spika shilingi milioni 238, 027,500 zilizoneshwa kwenye kitabu ni ruzuku kwa ajili ya kulipia mishahara ya watendaji na gharama za uendeshaji wa mfuko kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mfuko umeanza kujitegemea na una *vote* yake na unamuuongozo na uendeshaji wa na utoaji mikopo sera inakamilishwa na Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani suala zima la mipango kuhusu kuweka yaliyomo katika kitabu cha bajeti, ushauri wako tunauchukua na tutaufanyia kazi kwa kuweka yaliyomo katika kitabu tutaufanyia kazi.

Ushirika, Mhe. Suleiman Makame Ali, kuhusu wizara ina mpango katika kuimarisha usajili, usimamizi na uendeshaji wa *SACCOS*. Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba wizara ina mikakati maalum unawajumuisha watendaji wa wizara na vyama vikuu kwa kuendesha vikao kwa mashauriano na usimamizi wa vyama ushirika kiwilaya. Mkakati huu unasaidia katika kuimirisha utekelezaji wa sheria na kuongeza kasi utendaji wa viongozi kwenye vyama vya ushirika na *SACCOS*.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Suleiman Sarahan Said, wao wameuliza kuhusu juhudi za wizara kuviunganisha vikundi kwenye mabenki ya biashara. Mhe. Spika, napenda kumjibu kwamba wizara imekuwa na mpango wa kuviunganisha vyama vya ushirika na vikundi vya ujasiriamali, ili kupata mikopo kutoka kwenye mabenki mbali mbali lakini tumejifunza kwamba baadhi ya vikundi vinavyounganisha haviwezi kumudu masharti ya mikopo hiyo na matokea yake vinadhoofika.

Masuala ya uwezeshaji Mhe. Mwanaasha Khamis Juma wamepelekwa *SIDO* badala ya kupelekwa Kizimbani. Mhe. Spika, naomba utambue kwamba wajasiriamali waliopo *SIDO* ni

wajasiriamali ambao ni wavumbuzi ambao tayari wanaujuzi wa kutengeneza mashine mbali mbali kama mashine ya kutengezea sabani, matufali, miwa, kukandia unga, hivyo wamepelekwa *SIDO* kuongeza ujuzi zaidi. Ushauri uliotupa wasindikaji wa chakula kupelekwa Kizimbani kupatiwa mafunzo tutaufanyia kazi.

Sehemu ya ustawi Mhe. Hamza Hassan Juma, kuhusu fungu la utaratibu wa huduma za uhiufadhi wa jamii kupungua mwaka jana na kuzidi mwaka huu. Mhe. Spika, napenda kumjibu fedha za fungu kwa programu hii mwaka jana lilikuwa ni shilingi bilioni 8,800,749, 097 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 fedha zilizoidhinishwa ni shilingi Bilioni 5.79 kwa Unguja, na Bilioni 2.67 kwa Pemba. Kwa mwaka 2018/2019 fungu la programu hii halijabaguliwa naomba uangalie kitabu cha makadirio na mapato uk.Q01/2 kifungu no.PQ0103.

Idara ya Ajira, Mhe. Shaib Said Ali ushauri wake kuhusu baadhi ya vijana kupatiwa mafunzo wapatiwe nyenzo. Wizara yangu kupitia Idara ya Ajira imeshaanza utaratibu huo kwenye mpango kazi wake kwa kuanzia Pemba katika Wilaya ya Micheweni na Mkoani, kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Mei 2018. Vijana 10,026, wanaume 341 na wanawake 685 wako nje ya nchi ambapo Wilaya ya Mjini vijana 3,708, Magharibi 475, Kusini 42, Kati 29, Kaskazini A 20, Kaskazini B 38, Mkoani 9, Wete 9, Chake Chake 5, Micheweni 2 na Tanzania Bara 17.

Kati ya hao wanaume mmoja yupo Bahrain, mmoja yupo Madrid, Omar 160, wanaume na wanawake 585 Qatar, wanaume 98 na wanawake 2 Saudi Arabia, wanaume 23 na mwanamke mmoja Dubai, wanaume 58 na wanawake 97.

Mhe. Spika, wajumbe waliochangia kwa maandishi. Napenda kumshukuru Mhe. Harous Said Suleiman kwa kupongeza juhudi za wizara yetu katika utekelezaji wa shughuli zake. Aidha, tunamuhakikishia kwamba tutaendelea kufuatilia utekelezaji wa operesheni maalum ambao unapelekea kesi kumalizika kwa muda mfupi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kusaidia gharama za kesi kwa wananchi wasiokuwa na uwezo hasa usafiri. Napenda kumjibu kuwa wazo hili tutalifanyia kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, mtoto hakuokotwa mama yake yuko Hospitali ya Wagonjwa wa Akili kaletwa na watu wa Wizara ya Afya, mtoto jina lake halijulikani. Hivyo, watendaji pale wakatania aitwe mama Maudline Castico na wala sio Castico Cyrus Castico. Kama wanavyotoa majina mengine kwa watoto wanaokwenda wakiwa hawajulikani majina yao ni yepi, na hili sikuwashawishi wala sijui wewe ni wa kwanza kuniambia itabidi nimfuatilie mama yake hata kama ni mgonjwa huko hospitali. Kwanza nitake kujua je, anamjua mtoto wake jina lake ili aweze kusema.

Pia, suala zima la kuniunganishia na masuala yaliyopita ambayo yameshachukuliwa na yamefanyiwa hukumu, utakuwa unanionea na hunitendei haki. Kwa sababu kazi yangu niliapa hapa hapa mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa Mhe. Spika, akaniapisha na nyinyi mlikuwa mashuhuda na Mhe. Rais aliniapisha na niliapishwa mara ya pili, kwa kuwa ninataka kuhakikisha kuwa nasimamia haki zote na sitaogopa. Nitafanyakazi kwa mujibu wa sheria na utaratibu ulivyo na suala zima la kuona labda kuna hisia za ubaguzi litoweke, mimi kwa asili yangu sina ubaguzi. Nimemnyonyesha mtoto wa Kiislamu amekua na nina wajukuu watano

kwake yeye na sijambadilisha jina hata siku moja na sasa hivi anaishi Canada. Kwa hivyo, suala zima la kuchanganya na masuala mengine ya hisia likome. *(Makofi)*

Mhe. Spika, majibu ya moja kwa moja wizara kusimamia maendeleo ya vyama vya ushirika na kutoa mafunzo ushauri usimamizi wa sheria.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Naam, Mhe. Jaku Hashim.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nilisimamia kanuni ya 59(8) sijui utaniruhusu au. Nisome au haina haja. Mhe. Waziri kataja moja kwa moja jina langu na nimehisi kama kanikusudia mimi. Mimi sijambagua mtu, wala sijamkusudia yeye kuwa anafanya mambo kwa ubaguzi, katika mchango wangu sikusema hivyo. Kwa hivyo, nimuombe tu waziri afute kauli yeke, sikumtaja mimi kuwa anafanya vitendo vya ubaguzi. Kasema likome, sasa nikome mimi au likome vipi, kwa hivyo afute kauli yake.

Mhe. Waziriwa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Kama sio wewe basi kuna mjumbe mwengine alitaja ndio maana nimeunganisha. Samahani sana, na ninashukuru sana kwamba una taratibu nzuri sana za kufuatilia pale pahala, ninakupongeza. Kama sio wewe uliyenitaja basi kuna mjumbe kanitaja kwa jina.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Hapana. Mhe. Waziri nadhani tatizo ni ile lugha iliyotumika hapa haikuwa nzuri sana. Sio lugha ya Kibunge, kwa sababu inaudhi, yaani huwezi kumwambia mjumbe akome. Sasa ningeomba Mhe. Waziri ufute hiyo kauli ya kukoma tu halafu uendelee. *(Makofi)*

Mhe. Waziriwa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nimelipokea hilo suala sio kauli ya Kibunge, ninaomba radhi na nisingependa liendelee. Kwa unyenyekevu na kwa heshima zote na nitaendelea kutunza heshima hiyo kuna wakati wa ubinaadamu mtu anasema lolote. Ninafuta kwa maandishi na katika kumbukumbu zenu zote.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Naomba uendelee Mhe. Waziri.

Mhe. Waziriwa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, moja ya jukumu la wizara ni kusimamia maendeleo ya vyama vya ushirika na kutoa mafunzo, ushauri na usimamizi wa sheria katika vyama vya ushirika. Matokeo ya huduma hizo yameongeza ufanisi katika kuimarisha mahitaji ya *SACCOS* hadi kufikia bilioni 11.7 na kutoa mikopo kwa wanachama wao iliyofikia shilingi milioni 19 hadi mwezi Machi 2018 ...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane, naomba tumsikilize Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: na kurejesha kwa kupewa hadi kufikia bilioni 19.

Mhe. Spika, ushirika umesaidia kuimarisha uwezo wa viongozi, hasa wanawake na kuweza kugombea kama Mhe. Salma Mussa Bilal alikuwa mwanaushirika wa vyama. Wanachama wa vyama vya ushirika sasa wameelewa haki na wajibu wao katika vyama vyao. Wana uwezo wa kuhoji maslahi yao katika vyama vyao. Baadhi ya vyama vya ushirika vya kilimo mfano, Mtule AMKOS wametoa huduma za pembejeo za kilimo hivyo kuwapunguzia wanachama wao.

Mhe. Spika, kuhusu mtandao wa vikundi vya fedha. Wizara itaendelea kuwaelimisha na kuwaunganisha kwenye *SACCOS* kubwa ili kuimarisha usalama wa fedha zao na kupata huduma za kifedha zilizobora zaidi.

Idara ya Ajira. Mhe. Amina Iddi Mbarouk, swali lake ni wizara inachukua hatua gani kuwasaidia vijana wenye ujuzi maalum. Mhe. Spika, kwa mwaka 2017/2018 wizara kwa kupitia Idara ya Mfuko wa Ushirika na Idara ya Uwezeshaji, iliandaa mafunzo maalum mbali mbali ya kuwawezesha vijana wenye ujuzi maalum kuweza kujiajiri wenyewe na kuajibika katika shughuli mbali mbali za uzalishaji na huduma. Kwa sasa wizara ina mpango wa kuanzisha kituo maalum cha machinjio na kituo cha utengenezaji wa vifunganishio vya bidhaa. Vile vile, wizara mkakati wake mkubwa ni kuwaunganisha vijana na fursa mbali mbali za ajira ndani na nje ya nchi.

Idara ya Mikopo. Mhe. Suleiman Sarahan Said alitaka kujua utaratibu unaotumika, kufuatilia mikopo iliyotolewa ili irudi. Mhe. Spika, mfuko wa wafanyakazi unaofanyakazi kwa ushirikiano mkubwa na Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha wa Shehia zote. Wakati wa kufuatilia mikopo maafisa wetu ambao wapo kila wilaya wanashirikiana na Mashehe na Shehia husika. Aidha, maombi yote ya mikopo yanapokelewa kupitia kwa masheha jambo ambalo hupelekea kurahisisha suala zima la ufuatiliaji.

Mhe. Spika, ripoti ya mikopo za kila mwezi hutayarishwa na maeneo ambayo yana matatizo ya urudishwaji, huwahi kuchukuliwa hatua mapema kabisa.

Idara ya Wanawake na Watoto. Mhe. Amina Iddi Mabrouk suala lake linahusu mafanikio yaliyopatikana katika mapambano ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Mhe. Spika, naomba Mhe. Amina Iddi Mbarouk kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika wizara kwenye kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto kama ifuatavyo. Uelewa wa wananchi umeongezaje juu ya kuwepo tatizo hili. Samahani Mhe. Spika, naomba nirudie swali.

Uelewa wa wananchi umeongezaje juu ya kuwepo tatizo hili, sababu hatarishi zinazochangia vitendo hivi na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kutokomeza. Hali hii imechangia kuelewa kuwa kesi nyingi zinazoripotiwa usuluhishi umepungua na wananchi mbali mbali katika ngazi ya shehia kubaini sababu hatarishi za kuyafanyia kazi katika maeneo wanayoishi.

Kwa mfano, wananchi wamechangia kufungwa kwa baa kufuatia kuziripoti kuwa zinachangia uendeshwaji vitendo vya udhalilishaji, ushiriki wa ushirikiano kwa taasisi zinazoshughulikia matukio ya udhalilishaji na utekelezaji na kama vile utekelezaji operesheni maalum ambapo kesi zinatolewa huduma kwa muda maalum.

Mhe. Spika, naona katika haya ambayo nimeletewa nimeweza kujibu. Lakini kuna yale ambayo yameongezeka mbele hapa. Kuhusu suala la udhalilishaji wa mama aliyechomwa moto. Suala hili tunalifuatilia na kwa kuwa liko mahakamani itabidi tutafute utaratibu tu wa kutaka kuangalia limefikia katika hatua gani. Kama mnavyojua kwamba mambo yakifika mahakamani, masuala ya kufuatilia mengine yanachukua hata miaka minne na mingine mitano inategemea na hali halisi ya kupata mashahidi.

Mhe. Spika, naomba pia kusema kwamba masuala ya udhalilishaji ya kuzungumza kwamba wengine wametiwa kwenye vyombo vya sheria, wengine wanatajwa na wengine hawatajwi. Ni masuala pia ya kuendelea kutafuta haki za watu na kuhakikisha kwamba wanafuatiliwa ipasavyo, kupata ushahidi wa kutosha.

Mhe. Spika, fedha za mazingira zinazokatwa hazijakatwa bali wamelipwa na sasa hivi wanalipwa shilingi 70,000 ambapo hawa ni wale wanaofanyakazi katika mazingira magumu, ukiangalia ni wale wanaofanya Welezo na maeneo ya Sebleni na kulea wazee katika hali ngumu.

Pia kuna suala la waziri anafanyakazi vizuri Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nawanyanyasa wafanyakazi na kuna vyama vya wafanyakazi ambavyo vinafuatilia masuala ya unyanyasaji, hasa wale wanaopewa vitisho vya kijinsia. Kwa hiyo, wasipokuja kujieleza Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf tunakuwa hatujui tuwapate vipi na kwa bahati nzuri kwenye maeneo wanayokaa kuna vyama vya wafanyakazi ambavyo viko sehemu ile, wanapotoa taarifa wakija ofisini kwetu tunapaswa tuwafuatilie na shughuli zinaendelea.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) amepongeza na kushauri namna ya kuweza kuendelea kuchangia.

Mhe. Spika, naomba niseme la mwisho kabla sijamaliza ni suala zima linalozungumzia kwamba wafanyakazi wa Mazizini wa nyumba ya wazee wote. Suala hili nimeshalijibu, samahani. Kuna suala la mwisho ambalo nimesema kwamba linahusiana na kesi ambayo nadhani ameuliza Mhe. Abdalla Maulid Diwani, suala la mzazi anayeitwa Salum Shehe.

Mhe. Spika, naomba niseme hivi kwamba Salum Shehe ni baba na ni Shehe ni mtu ustadhi, ni mtu ambaye tunamtegemea sana katika michango ya kijamii. Amekuja mara nyingi sana ofisini kwangu kutaka hata ushauri namna gani ya kuweza kuhakikisha kwamba masuala yote yaliyofanyika ya udhalilishaji wa watoto, katika sehemu inayotolewa mafunzo ya kidini waweze kuanzisha utaratibu utakaoweza kusimamia, kwa kuwa wao watakuwa ni huru zaidi katika kueleza na kuwafahamisha watu vizuri.

Mhe. Spika, suala lililojitokeza hapa sina undani nalo sana, kama anavyosema mtu yeyote kwamba ikitokezea kesi atanipigia simu kwamba mheshimiwa kuna tatizo hili. Akisharipoti polisi suala la *summons* sio la mama Castico, sio la waziri ni suala polisi na taratibu zinachukuliwa kwenda kufatilia polisi.

Mhe. Spika, suala la kusema kwamba huyu mtu ananihusu kwa damu ama kwa namna yeyote ile, atasema hivyo ananihusu kwa sababu labda ni wifi yangu, ambaye yeye ni Muislamu, baba wa mtoto ni Muislamu, mke mama watoto ni Muislamu suala la ubadilishaji jina hilo silijui, nasikia

mnaniambia mimi hapa japokuwa nilisema kwamba suala hili mama tuliwahi kumuita akasema kwamba yeye alibadilisha kwa sababu ya dharura alizokuwa anaonesha baba mtu alikuwa anataka kumchukua mtoto, kwa sababu alikuwa amemuacha muda mrefu hakumuhudumia. Utaratibu aliofanya ni kumteka mtoto kwenye basi anapotoka skuli, masuala yote haya yalikuwa yanashughulikiwa na polisi. Hatua zilizofuatia baadae kama lipo mahakamani au lipo kwa Kadhi sijapata taarifa hizo. Mimi siwezi kufuatilia masuala ambayo yako katika vyombo vya kidini kwa mujibu wa imani ya Kiislamu, kwamba hatua zimepelekwa kule siwezi kwenda pale nikafuatilia wala nikaingilia na sina *interest* juu ya mtoto huyu, ni sawa sawa na mtoto mwengine yeyote ambaye kesi nikiletewa lazima niisimamie.

Mhe. Spika, narudia tena, mtu yeyote akiwa na kesi ya aina yoyote ambayo inahusu mtoto kwa mujibu wa sheria na makubaliano ya kimataifa juu ya kulinda haki za mtoto duniani, basi atatetewa mpaka dakika ya mwisho na hatutoona hofu wala aibu ya kumfuatilia. Lakini kama kuna suala hili la kusema lina *interest*, sina *interest* nalo na ninaomba msiunganishe na mambo mengine ambayo yamepita. Suala la mtoto Ibrahim ilimaliza kesi na yalifuatiliwa kwa mujibu kama huu. Sasa huyu anabadilishwa wakati yuko hapa hapa, Unguja baba na mama wapo hapa hapa Unguja.

Mhe. Spika, mimi kama kiongozi na Waziri wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, basi halitoweza kuvumilika mpaka lichukuliwe na ifuatwe taratibu. Kama ni hasira tunawashauri, tunawaita na tunawapoza wakumbuke jinsi walivyopendana siku za kwanza na hakuna mtu aliyekuwa anampenda mkewe kama Shehe Salum kokote aliko anisikie, alikuwa anampenda mno. Sasa kama wamekosana pahala ni masuala ambayo yanaweza kwisha ni kesi za familia ambazo zinapaswa zifuatiliwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, labda kwa nyongeza tu ni kwamba mimi sasa hivi ni mjane, naitwa Maudline Castico kwa heshima kwa kuwa jina langu ni la mume wangu na linajulikana hilo, lakini kwa taratibu ya Kikristo ningeweza kubadilisha nikaitwa jina jengine. Kwa maana hiyo, siko kwenye kufungamana na familia iliyoniowa, ndio maana tunasema kwamba hatuachani mpaka kifo kitutenganishe. Nikifiwa mimi naruhusiwa kuposwa na hata yeyote anayenitaka hapa, anayetaka aje asubiri suala la jibu la ndio au hapana. Lakini ili usihangaike sana sina haja ya kuolewa sasa hivi nina wajukuu ninawalea na watoto. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, naomba tuendelee na mshikamano na upendo uliopo kwenye wizara yangu, mnanichangia sana. Kabla sijasahau Mhe. Suleiman Sarahan Said alizungumza akasema kwamba kuna wakati mwengine wanaume wananyanyaswa. Ni kweli wanaume wananyanyaswa, kuna wakati wengine hawasemi kwa kuona aibu. *(Makofi)*

Lakini niseme tu Mhe. Spika, mwanamme yeyote kati yenu kama ananyanyaswa basi nileteeni hao wanawake wanaonyanyasa niwashughulikie. Wanawake msikie msiwanyanyase waume zenu, imeandikwa kwamba wanaume ndio vichwa vya familia, wakikosea kuna utaratibu wa kushauriana, kama vile kuna viongozi wa dini, kuna Masheha na kila pahala ili tuendeleze familia. Kwa kweli, zikiharibika familia inakuwa mzigo wa serikali na hapo ndipo inaposhindwa kufanyakazi na tunavunja heshima na masuala yote yanakuja ya udhalilishaji kwa sababsu familia hazikai pamoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niwaombee sana Mwenyezi Mungu aendelee kuwatunza na kuwabariki muendelee kupendana, tuendelee kutunza taifa letu na tumpongeze sana Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kutunza amani na uhuru wa wananchi wa kwenda wanakokwenda pasipo ubaguzi, hakuna kujali mtu huyu wa Bara huyu wa Kisiwani au mtu wa wapi, kwa rangi, kwa dini wala kabila. Naomba kuwatoa wasiwasi watu wote wasiwe na hofu kwamba Zanzibar kuna ubaguzi hakuna, hizo ni hisia chache chache za kawaida ambazo zitafika siku moja zitakwisha. Kwa hivyo, ninaendelea kuwaombe tena Ramadhan Kareem na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, samahani naomba utoe hoja.

Mhe. Waziriwa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Vicheko/Makofi)*

$$$

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Naomba kuipongeza wizara kwa uwasilishaji wenu huu wa bajeti ya mwaka 2018/2019. Naomba kuchangia maeneo mawili ya bajeti hii nayo ni;

Fungu No. Q010202 Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhalilishaji.
Ukurasa wa 28 Aya ya 31. Kuna ongezeko kubwa la pesa la 1,775,924,760 kwenye programu hii ukilinganisha na mwaka jana, programu hii 150,000 ilipangiwa kiasi ambacho tulopigania sana kuongeza fungu hili leo limeshapitishwa na viashiria vyake ni vile vile. Nataka kujua kumeongezeka nini.

ENEO LA PILI

AYA YA 24 BULETI YA MWISHO

Kuna takwimu zenye kuleta utata akipiga hesabu yake akilinganisha na eneo la kiambatanisho chako no. 10, kuna wazee karibu 638 hawana maelezo na wako kwenye fungu la waliokuwa hawajalipwa. Hapa nataka maelezo yake kuwa wamekwama kulipwa kuna tatizo gani?

Mwisho wa Mchango wangu. Nataka pia maelezo ya nyumba ya kulelewa watoto inamilikiwa na nani?

Kama serikali inamiliki tunataka kuona hati ya umiliki wa nyumba hii. Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 65 na zilizobaki nipate maelezo ya hoja zangu. Ahsante.

Mhe. Mohamed Mgaza Jecha: Mhe. Waziri, kwanza napenda kuungana na Wizara yako ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Naipongeza sana wizara hii kwa kuchukua hatua mbali mbali kuongoza wizara hii. Naomba uendelee na kazi hii ya wananchi wa Zanzibar. Naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Kuhusu mchango wa maandishi hotuba ya bajeti mwaka 2018/2019. Pongezi kwako na watendaji wote wa wizara.

1 **Kukosekana kwa kurasa za yaliyomo**

Kurasa za yaliyomo ni muhimu, yaliyomo humrahisishia msomaji kujua maudhui yaliyomo ndani, yapo wapi na yana upana gani?

Ushauri. Kwa kuwa inaonekana kama ndio *style* za hotuba za wizara yako, kwani hata hotuba ya mwaka 2017/2018 haina mashauri 2019/2020 yaingizwe.

2 **Kampuni ya Ulinzi wa Minara ya Simu inayoitwa Jendele**

- Wafanyakazi wanaofanyakazi katika kampuni hii wana malalamiko ya siku nyingi katika idara yako inayoshughulikia migogoro ya kazi.

- Wanadai kulipwa mishahara midogo shilingi 106,000/- isiyoendana na agizo la wizara shilingi 300,000.

- Wanadai kutokuwa na mikataba ya kazi, kufukuzwa ovyo, kupewa lugha mbaya na kadhalika.

Hoja: Shauri hili limefikia wapi? Kama bado halijapata ufumbuzi, unawaahidi nini wafanyakazi wa kampuni hiyo?

3 **Fungu; Q010201- Utaratibu wa Huduma za Uhifadhi Jamii**

Hoja: Fungu hili ambalo liliitwa Q010301 bajeti ya mwaka 2017/2018 lilikuwa na makadirio ya shilingi bilioni 5.79, lakini katika bajeti hii lina bilioni 8.44.

Ni mambo gani yameongezeka hadi kupanda kwa fungu hili kwa wastani wa asilimia hiyo? Naomba ufafanuzi wa kina.

4 **Fungu Q010202 - Maendeleo ya Wanawake na Kupinga Udhalilishaji**

i) Kwenye kitabu ukurasa 61 kiambatanisho no. 12. Fungu lina namba Q010201. Naomba lifanyiwe marekebisho na lisomeke Q010202.

ii) Fungu hili mwaka jana lilikuwa na wastani wa shilingi milioni 150 na baadae tukaliongezea kidogo. Mwaka huu limeongezewa jumla ya shilingi bilioni 1.77.

Je, ni shughuli gani kubwa zimepangwa kutekelezwa? Naomba ufafanuzi na mchanganuo kulingana na shughuli zilizopangwa.

5 **Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto**

i) Pongezi kwa mafanikio katika utoaji na urejeshaji wa mikopo ya uwezeshwaji.
ii) Je, ni lini mfuko wa uwezeshaji utajitegemea wenyewe na kutoingiziwa fedha kutoka serikalini?
iii) Imeelezwa katika kitabu kuwa mfuko umewekeza shilingi 550 milioni. Je, mfuko unayo sera ya mikopo ambayo imetoa muongozo wa uwekezaji?
iv) Kuna sababu gani za kutolipwa kwa wazee 2,060 - Pensheni - (Ukurasa 59 kiambatanisho namba 10)
v) Naomba ufafanuzi;

Kiambatanisho namba 4 ukurasa wa 53 na 54 kuhusu waliopata mikopo
- Naelewa kuwa mikopo inatolewa kuendeleza miradi ya uzalishaji, lakini ukiangalia shughuli zilizotajwa kwa makundi namba 5,12,15,19,24,27 kama sio shughuli za udhalilishaji. Je, watalipaje mikopo hiyo kwa ununuzi wa vitu?

6 **Mpango wa Pensheni**
Takwimu iliyotolewa ukurasa wa 22 *bullet* ya 3 ina utata. Naomba ufafanuzi.

Mwisho;

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja iwapo nitapata majibu yenye kukidhi hoja zangu. Ahsante. Kazi nje, pole kwa majukumu.

Mhe. Shaib Said Ali: Nianze kwa shukrani kwa wizara, waziri, katibu na watendaji wote wa wizara hii.

Ukurasa wa 18 kifungu 24. Uratibu wa Huduma za Jamii, suala zima la fidia. Kwanza nimshukuru sana waziri kwa kufuatilia hatua hii na kuwalipa fidia wale wote wanaostahiki. Lakini nimuombe waziri wale 7 waliobaki basi wapatiwe stahiki yao kwani wengine ni wapiga kura wetu

Ukatili wa watoto. Naomba wizara kuzidi kufanya utafiti na ufuatiliaji kwani bado kuna wzee wa kiume na wakike bado wanawanyanyasa na kuwatendea ukatili watoto hasa wale wanaoachwa na baba yao au mama yao kwa kulelewa na mama au baba wa kambo.

Ukatili na udhalilishaji wa wanawake. Bado vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji wa wanawake unaendelea.
a) Katika mirathi- hawashirikishwi.
b) Wanapodai talaka baada ya kupata mateso au udhia kwa wanaume zao.

Hapa vyombo vya sheria hasa kadhi, hapa kidogo panahitaji wizara yako kulifuatilia. Mtu hutoa talaka kinyume na kile alichopewa maharusi. Kwa mfano, mtu kamuowa mwanamke kwa mahari ya shilingi laki mbili, lakini awataka watowe shilingi laki 7 au laki 8 ndio atowe talaka, hii sio haki hata kidini.

Upatikanaji wa ajira za stahiki ukurasa 30. Mimi nashauri baada ya mafunzo basi wapatiwe nyenzo na sehemu za kufanyia kazi. Kwani vijana wengi hupata mafunzo, lakini hatunao huishia ndani
Mimi nimuombe waziri, kuna utaratibu gani wa vijana hawa kwani bado wanakwenda na manyanyaso ya ukatili yanaendelea kufanyika. Nimuombe tu waziri ni vijana wangapi walioajiriwa nje ya nchi na wako vipi. Ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Napongeza sana juhudi za serikali kusimamia utekelezaji wa wizara hii ya Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto na kupelekea walengwa wa wizara hii wakiwemo wanawake na watoto kuweza kupata na kujua haki zao.

Nampongeza Mhe. Waziri kwa kuwasilisha vyema hotuba ya bajeti, hotuba iliyotimiza mahitaji yote ya wizara hii.

Nashauri wizara isimamie na ihakikishe kesi za udhalilishaji wanawake na watoto zinapatiwa uamuzi wa haraka sana, ili kuepuka kupotezwa kwa ushahidi kwa makusudi. Pia kusaidia gharama za kesi kwa wale ambao wanaonekana kutoweza kugharamia, ikiwemo gharama za usafiri kwa wahusika.

Naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

Kwanza naungana na wajumbe wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Ulimwengu, aliyetuwezesha kufika hapa tukawa katika hali ya uzima na tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe kuumaliza mwezi mtukufu wa Ramadhani. Amina.

Naomba kuchangia katika ukurasa wa 14 orodha ndogo ya maendeleo ya wanawake kupinga udhalilishaji.

Mheshimiwa, programu hii ina dhamira ya kupinga udhalilishaji, lakini wizara hii bado ina kazi kubwa kwa suala la udhalilishaji, hasa ukizingatia udhalilishaji una maana nyingi na bado kuna baadhi ya wananchi suala hili hawalichukulii kuwa ni suala la udhalilishaji katika nchi yetu.

Ushauri wangu.
- Serikali ibuni mbinu za kutafiti kwa karibu sana kuwa na wananchi bega kwa bega ili tulitokomeze suala hili.
- Vyombo vya dola vifanye doria katika maeneo yetu yaliyokuwa tishio kwa suala hili.
- Takwimu zetu ziwe za uhakika.

Kifungu cha 2b mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto.
Mhe. Waziri, umetueleza lengo la kukuza muitiko na uratibu mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji nchini.

Vile vile umefanya uzinduzi wa mpango kazi, pia umeongeza wajumbe wa kamati.

suala langu lipo hapa. Je, Mhe. Waziri tangu tufanye shughuli hizo za uzinduzi na uingizaji wa wajumbe tumepata mafanikio gani? na uzinduzi huo umefanyika mkoa gani?

Mwisho. Nawapongeza wafanyakazi wote wa wizara yako kwa kutekeleza majukumu yao kwa umahiri.

Baada ya mchango huu kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mheshimiwa, naipongeza wizara hii ya uwezeshaji pamoja na Naibu Waziri na watendaji wako wote.

Mheshimiwa, naunga mkono hoja kwa asilimia 80 hadi nipate jawabu ya wakopaji binafsi na mahali walipo na kila mmoja kafaidika kupata mkopo wa kiasi gani? Uwezeshaji watu kiuchumi, mikopo ya watu binafsi imekua kwa idadi kubwa. Nataka kujua watu hawa binafsi wapo katika wilaya gani na jimbo gani, ili tuone hatua zao za maendeleo, kwani vikundi tunaelewa ukivihitaji viko wapi, lakini hawa binafsi hatujui wako wapi?

Lakini pia katika mchanganuo wa mikopo unaonesha kuwa watu wamepewa fedha za mkopo kutafuta vifaa vya elimu, au utoaji wa mafunzo. Mhe. Waziri naomba ufafanuzi hawa waliopewa

fedha hizi wao watalipa vipi hizi fedha ambazo zimetolewa katika kuendeleza biashara mbali mbali.

Pia kumeelezewa fedha zilizotolewa kwa wafugaji, lakini kwa nini ufugaji haukuainishwa ni ufugaji wa samaki, kuku, ng'ombe, mbuzi na kadhalika ambapo ungeainisha ukubwa wa mradi na fedha walizopewa.

Ustawi wa jamii nawapongeza kwa juhudi za kujali wazee, lakini kama kuna uwezo wa kuwasadia wazee wetu basi tuwapeleke Hija na sio kuwapeleka Forodhani na kusikiliza mziki wazee wetu, wanahitaji sana kuleta istighfar na kumuelekea muumba wao.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Waziri niweke kwenye orodha ya waliochangia kwa maandishi hotuba ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa wizara hii.

Mheshimiwa, naipongeza sana wizara yako kwa utendaji wenu wa kazi. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Waziri na Naibu Waziri, naomba kuchangia kwa maandishi. Naunga mkono bajeti yenu kwa asilimia 100. Lakini mwaka huu naomba shehia zangu sita naomba kupatiwa mikopo, kila shehia angalau kikundi kimoja majina nitakuletea, tayari wamejisajili muda mrefu lakini mikopo hawajapata, tena wote ni kinamama. Ahsante sana.

$$$

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Watendaji wake kidogo wakamsaidia.

Mhe. Mwenyekiti: Watendaji wa Mhe. Waziri wanaruhusiwa kuja kumsaidia kuwa karibu.

FUNGU Q01 - WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu Q0107	Idara ya Maendeleo ya Ushirika	60,000,000
Kifungu Q0108	Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii	20,000,000
Kifungu Q0110	Idara ya Ajira	50,000,000
Kifungu Q0111	Kamisheni ya Kazi	600,000,000
Kifungu Q0112	Idara ya Usalama na Afya kazini	64,613,000
	Jumla Kuu	**794,613,000**

FUNGU Q01 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu PQ0101 Programu ya Uwezeshaji Kiuchumi

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nitaanza na Suleiman Makame Ali, atafuatia Mhe. Abdalla Maulid Diwani, alafu atamalizia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutaka ufafanuzi. Jana nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la utoaji wa mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tukarudi kwenye viashiria kwenye ukurasa wa Q1013.

Mhe. Mwenyekiti, wametwambia kwamba wametoa mikopo yenye thamani ya shilingi 600,000,000 lakini kwenye viashiria kwenye kitabu kikubwa hichi mwaka 2017/2018 kuna shilingi 300,000,000, lakini mara pia vile vile mara hii wamesema watatoa mikopo 600. Lakini kwenye kitabu hichi kikubwa kuna shilingi 500,000,000. Kwa hivyo, naomba kujua kitaka mie nijue shilingi 100,000,000 tukisha idhinishia 600 itakwenda wapi kwa sababu huku haiko, hii shilingi 100,000,000 ya mikopo 100 itakwenda wapi, mfukoni kwa nani. Vile vile, kwenye hichi kitabu walitwambia kwamba wametoa mikopo 600 lakini kitabu cha bajeti hichi hapa wameweka mikopo 200 kwa Unguja na Pemba wameweka mikopo 279.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kujua ukweli uko wapi kwenye kitabu kikubwa kuna 300 kwenye kitabu kidogo kuna 279 na lengo wamelifikia wamefikia shilingi 660,471,000. Kwa hivyo, nikitaka nijuwe vizuri hapa mikopo 21 kwenye ile 300 walioiweka kwenye kikubwa imekwenda wapi, na ile mikopo 100 itakwenda wapi, kwa sababu huku hakuna. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, yalioko humu na naomba nikukumbushe kwamba hii mikopo ni masuala ya ruzuku ni michango iliyochangishwa na Mhe. Rais kama nilivyo kwisha jibu kwenye masuala yaliyokuwa yametokea hapa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, jibu halijapatikana, nasema vipi kwamba mikopo aliyoandika kwenye kwenye kitabu waliotuomba mwaka 2016/2018 hii bajeti tunayokwenda nayo waliseme wanataka kutoa mikopo 600, tukawaidhinishia shs. 238,000,000 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mikopo lakini kwenye kitabu kikubwa kwenye viashiria wametwambia mikopo ni 300, lakini huku kwenye kitabu hichi kidogo wametoa mikopo 279, hapo haijapatikana mikopo 21 nataka nijue imekwenda wapi. Lakini vile vile mara hii wametuomba tena kwamba wanataka kutoa mikopo 600 lakini kwenye kitabu kikubwa hichi kwenye viashiria wameandika 500, hasa huku kwenye kitabu kidogo 600 sawa, huku mikopo 100 itakwenda wapi wakati iko huku kwenye buku kubwa hakuna. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. hajaweza kuona vizuri, kwa sababu tunapokuwa tunasema tuna makadirio, tumekadiria 600 na hali halisi inapokuwa inazungumzwa haifanani na ile tuliyokuwa tumekadiria. Naomba lizingatie hilo naangalie na kwamba mikopo hii inayotoka ni *revolving fund* watu wakishakopeshwa warudishe pesa ili ziweze kufanyakazi. Hatuchukui pesa nyengine mpya mahali pengine.

Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, hii ni mara 3 mimi nataka ufafanuzi anifahamishe hata kama mikopo 600 kwa sababu mara iliyopita hii bajeti tunayokwenda nayo wanaseme wanatoa mikopo 600 lakini wametoa mikopo 200 haina tatizo lakini tatizo liko wapi wametoa 300 kwenye kitabu kikubwa huku kwenye kitabu kidogo kuna 279 hapa hatuja fahamiana. Lakini, sasa kulikuwa na jengine ni kwenye suala hili hili la mikopo hapa, sasa mimi nikitaka nifahamishwe hii mikopo 100 kwenye 600 alau angeweka ile ile 600 hata kama aje toa 100 lakini ilikuwa aweke ile ile 600 ndio bageti kwa sababu kwenye bajeti hawezi kupunguza, wakasema kwamba tutaweka hii wakati hawajui kama tutaipata wangeweka ile ile 600 hapo tungefahamia. Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nishakuelewa Mhe. Mjumbe. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, sijui kama unaweza kulisaidia kidogo hili.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, najaribu kumfahamu sana Mhe. Suleiman Makame Ali, lakini kwenye utoaji wa mikopo wakati mwengine unachokipanga hakitoendana na kama hivyo anavyosema yeye, kwa sababu ni *revolving fund*. Ukitoa pesa unatarajia kwamba zikirudishwa unaweza kukopesha wengi zaidi, sasa inawezekana ikawa hiyo ndio sababu ya *misplace* baina ya fedha na idadi ya wanaokopa. Kwa kweli, *revolving fund* wakirudisha unaweza kukopesha wengi zaidi. Sasa kama hivyo ndivyo nilivyomfahamu hilo ndio jibu lake. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, muongozo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hana nafasi tena. Mhe. Hamza Hassan Juma muongozo.

MUONGOZO

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, hapa tunapitisha bajeti na kuna vitu viwili ambavyo vinavyojitokeza naomba kidogo utoe muongozo wako. Hotuba ya Waziri ni Kitabu, lakini sisi tunapitisha kitabu kikubwa cha bajeti. Kwa hiyo, kama kuna makoseo kwenye hotuba ya waziri inamana irekebishwe kwenye kitabu kikubwa, kwa sababu hapa tunapitisha kikubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, nadhani inaliweka sawa hata hilo tatizo ambalo Mhe. Mjumbe analo. Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, mimi nilivyochangia niliulizia hili suala zima la mikopo hapa na nikasema kwamba 2017 tuliwapo mikopo watu jumla ya shilingi 660,000,000 na kidogo, lakini hii 2018/2019 tumetenga au tunakisia shilingi milioni 600,000,000 kwa kigezo gani, tunacheza hapa hapa kwenye 600 tu, Mhe. Waziri hajatoa ufafanuzi wa kutosha kwenye suala kama hili. Je, wamepungua wale watu kwamba mahitaji yamepungua ndio maana nacheza hapa au kuna njia nyengine. Naomba muongozo wake kwanza.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimejibu hapa, kuhusu kwa nini kila mwaka pesa za mikopo ni shilingi milioni 600,000,000 kwa wakopaji 600. Nilipokuwa naeleza hapa Mhe. Mwenyekiti nikijibu hoja hii, nilimjibu kama ifuatavyo, kwamba shilingi milioni 600,000,000 ni fedha zilizochangwa tokea kuanzishwa kwa mfuko huu ambazo ziko benki na zinatumika kwa kutoa mikopo kwa wananchi wanaoomba, wananchi wanatakiwa kuzirejesha fedha hizi kwa wakati, ili weweze kupewa wakopaji wengine ili kuziongeza fedha hizo mfuko unatakiwa kutafuta vyenzio vyengine vya mapato kama hiki cha mradi wa mboga mboga, kutokana na uwepo mradi wa mboga mboga na matunda, mfuko umeta kiasi cha shilingi 300,000,000 ambapo fedha hizo zinakuza mfuko kufikia shs. 900,000,000.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, nadhani ungejibu kwa ufupi tu hakuna haja ya kurejea tena hotuba nzima. Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, Ahsante namshukuru sana Mhe. Waziri kaniweka wazi. Sasa kwa nini basi hapa kwa sababu kasema kwamba kaongeza katika Mfuko wa mboga mboga imekuwa 300 kwa nini hapa asiweke mikopo na juu ya kutolewa ni ya shilingi milioni 900,000,000 nafikiri ingelikuwa hakuna tatizo. Lakini hapa kasema aah! Mikopo ya shilingi milioni 600,000,000. Kwa hiyo, naona tuendelee.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilimuuliza maswali hajanijibu, wananchi wangu wa Jimbo la Chaani katika kuwezeshwa katika masuala ya vikundi hawawoni wizara haijawasaidi hasa upande wa Pwani Mchangani, Kandwe, sehemu nyenginezo ndani ya jimbo langu, nilisema Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho wanieleze wamenisaidia vipi katika jimbo kwenye kuwawezesha wananchi wangu kwenye masuala yao ya vikundi ushirika, lakini jibu hilo sijalipata.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, siko *comfortable* sana maana yake naona au nafikiri sasa tunapitisha kifungu, kwa sababu nikiruhusu hali hii kila mwenye jimbo lake naye ataka kitu ndani ya jimbo lake kielezewe katika sehemu hii. Naomba nimruhusu Naibu Waziri kama anaweza kutusaidia. Mheshimwa Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alipochangia alitaka kujua japo unimesema kila mmoja alitaka kusema kwenye jimbo lake. Lakini Mhe. Mjumbe katika jimbo lake wizara imewawezesha wananchi wa Jimbo la Chaani kama ifuatavyo:-

Mhe, Mwenyekiti, imehamasisha na kuanzisha *SACCOS* ya Jimbo la Chaani, imehamasisha na kuanzisha *ANCOS* ya Chaani inaitwa Faraja, imewasaidia vyama 5 vya kilimo, ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, kuku wa mayai, kiwanda cha kukoboa mpunga ambayo ni Chururu Si Ndondondo pamoja na *NGOs* nyengine inaitwa Tupendane Group tumewapa hawa mboga mboga.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo jimbo lake Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf tumeweza kulisaidi na kupewa mafunzo pamoja na mkopo wenye thamani ya shilingi 12,000,000.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani umeridhika Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mh. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, naam sijaridhika pesa kidogo. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee, Mhe. Panya Ali Abdalla buti la lako jepesi sijalisikia.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nilipokuwa nikichangia katika hotuba hii kuhusu hawa waliokopeshwa mtu mmoja mmoja, mikopo ya wale watu binafsi wale nilitaka kujua hawa waliokopeshwa watu 199 wapo katika wilaya gani na majimbo gani, ili tuweze kujua tuweze kufuatilia maendeleo yao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia katika uchanganuzi huu wa mikopo kuna vikundi vinaonekana vimepewa vifaa kama vifaa vya elimu, vifaa vya umeme, au utoaji wa mafunzo, tulitaka kujua hii ihusiani na mikopo watarudisha vipi. Hapa inaonekana kuna mikopo, mafunzo wataweza kulipa fedha hizi kwamba wamepewa mafunzo. Nilitaka kujua ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, lakini la kwanza la kwamba utajiwe kila jimbo ambao wamepewa nafikiri itatupoteza muda mwingi. Mhe. Waziri, sijui kama una majibu.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba bahati mbaya wameleta dakika za mwisho, kwa hivyo halikuweza kujibiwa. Lakini nataka ni mwambie tu wale wanaopewa kwenye mtu binafsi ni pale wanapokwenda vikundi vinakuwa kwa jumla kikundi kwa jina moja halafu baadae wao wenyewe kwa ndani wanapewa wanagawana. Kwa mfano, wanaweza kukopa kiasi fulani halafu baadae wakagawa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye wilaya yake ni kwenye *page 52* ambapo nimekuwa nimezungumza hapa kwenye kitabu changu, ni wale ambao kwa mujibu wanavyohitaji msaada, wale wengine walio na kazi wanaweza akapewa na akakatwa kwenye mshahara. Wengine wanapewa kwa mujibu wa kile kitu ambacho wanaweza kupewa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, lakini hii ni mikopo, sasa sijajua kama hii msaada, maana msaada mbali na mkopo mbali kama ni mkopo fedha za serikali zinahitaji kurejesha na wengine waweze kufaidika na mikopo hiyo. Lakini sasa kama ni hawa waliopewa ni msaada tusije tukalalamika kama fedha za mikopo hazirejeshwi kumbe watu wamepewa fedha kwa njia nyengine. Vile vile, hawa watu ambao wanapewa mmoja mmoja halafu ikawa hatuwajui wako wapi. Hili pia ni tatizo inawezekana fedha za serikali nyingi zikaweza kupotea bila ya kuwajua watu hawa wako wapi. Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimepokea nataka nimtowe wasi wasi kwamba utaratibu tunaofanya uko wazi na kila kitu kinatunzwa kwenye kumbukumbu zake. Kwa mfano, kuna wale wanaokuwa kwenye hali ngumu wanaweza wakapewa na bado wakafuatiliwa. Lakini yeye kila mkopo upewe urudishe, hakuna anaepewa bure, ndio mana tunatunza mfuko huu tangu Dkt. Ali Mohammed Shein ameingia madarakani hautujaupoteza. Miradi ya huko nyuma ya "AK" na "JK" iliyayuka kwa sababu hatukujifunza namna ya kufuatilia. Kwa hiyo, naomba amini ofisi yangu kwamba tunafanyakazi kwa uaminifu sana. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye lakini huu utaratibu ungewekwa mkopo ni mkopo, ili tukaweza kujua na kama kuna fedha tumewapa watu kwa ajili ya mafunzo au kwa kazi nyengine zingetengwa mbali tukajua, kwa sababu fedha ya mkopo maana yake irejeshwe wengine waweze kufaidika. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

FUNGU Q01 WIZARA YA KAZI, UWEZESHAJI, WAZEE WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu PQ0101	Programu ya Uwezeshaji Kiuchumi	1,187,594,000
Kifungu PQ0103	Programu ya Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto	

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, naona watu wawili, Mhe. Adalla Maulid Diwani na Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Adalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, wakati nilipochangia nilimuuliza swali Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto wana shamba pale Muungoni. Je, hili shamba wanalitambua na wana mkakati gani kwa wao, ili kutumia kama shamba darasa kwa wale watu ambao watawasaidia fedha zile za mikopo kuwaonesha namna gani wanaweza kujikimu katika suala zima la kilimo. Niliuliza hilo swali sijalipata. Kwa hivyo naomba jibu lake.

Mhe.Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimelipokea hilo swali na nitalifuatili kwa karibu na kuhakikisha kwamba linatumika kama alivyoshauri.

Mhe. Maulidi Abdalla Diwani: Vipi kwani wanapokabidhiwa hakuna *asset register* ndani ya wizara wakajua kwamba wizara hii ina moja, mbili, tatu kwa sababu hili shamba lina muda mrefu sasa kuniambia atalifatilia sifahamu tu miye.

Mhe. Mwenyekiti: Maana yake hana habari nalo Mhe. Waziri, lakini atafuatilia kupitia wizara. Mhe. Waziri labda umjibu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, *to be realistic* huwezi ukawa na kumbukumbu za wizara kubwa kama Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kichwani kama *computer*, naomba uniamini kabisa kwamba nitalifatilia na umenishitua, inawezekana kuna wengine wanaficha makusudi, ili tusipate kuyaona. Lakini kwa kuwa umelifatilia kwa umakini wako nakushuru kwamba nitalifatilia na mengine kama yapo unayajua mimi siyajui nisaidie ili niyafatilie. *(Makofi)*

Mhe. Maulidi Abdalla Diwani: Ahsante. Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, nafikiri wizara zote zinazo *asset registers* mali zisizohamishika ziwekwe katika buku kubwa, ili ziwe ithbati kwamba zisichukuliwe na wajanja wajanja. Kwa hivyo, watakapokabidhiana hizo wizara wende kuangalia mali za wizara isingelikuwa tatizo kulijua hili suala. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nafikiri Mhe. Waziri analo jawabu la kutosha sasa hivi sijui kama niendelee mimi tena au atakuja kutoa jawabu Mhe. Waziri kwanza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ameshamaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja zangu mbili hapa kwanza nimfahamishe tu Mhe. Waziri kwamba Mhe. Rais wetu wa Zanzibar tokea anapotoka hana ubaguzi wa kidini kabisa katika Baraza hili hata kidogo, Baraza la mwanzo alikuwemo Mkristo wa mwanzo humu na la pili ni yeye kwa hivyo hana ubaguzi kabisa wa kidini Mhe. Rais wetu wa Zanzibar. Hoja yangu ya mtoto, kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha sheria ya mtoto namba 6 ya mwaka 2011. Kimeweka utaratibu wa mtoto kupewa jina kama watendaji wameruhusika waziri achukuliwe hatua za kisheria Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba unisaidie. Sasa hoja yangu nataka hatua zichukuliwe za kisheria. Hilo la kwanza nimalize hili au nimalize yote mawili kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti: Fafanua hatua za kisheria zipi zichukuliwe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hili jambo lisije likatokea tena likome kama nilivyokomeshwa mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nilimlazimisha Mhe. Waziri alipotumia hilo neno nikamlazimisha alifute.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Lisije likatokea tena Mhe. Mwenyekiti liwe ni fundisho jengine lisije likatokea. *(Vicheko)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Nashukuru Mhe. Jaku Hashim Ayoub unapenda kuchangamsha Baraza, na mimi nashukuru kwa kunichangamsha kwa sababu una-*charge* betri ya akili yangu ifanye kazi vizuri. *(Vicheko/Makofi)*

Nataka kusema tu kwamba utaratibu uliopo anapookotwa mtoto hajulikani jina lake nani akiwa mtoto ana kadi yake, tunawashukuru sana wazazi hata wale wanaotupa watoto akituwekea kadi au akaandikwa kwenye mkono mtoto huyu aitwe jina fulani anaitwa. Sasa katika hili la mtoto kuitwa jina kwa kweli sina taarifa wala sijashauriwa nimepita tu nikasikia kuna mtoto na nikafatilia nikasema msimpe mtoto jina mnasema mama yake ni mgonjwa wa akili nitakwenda kumfata. Maadam kamlea mtoto mpaka kafika miezi mitatu anaweza kuwa na kumbukumbu na bahati mbaya mtoto mwenyewe wanadhani ana asili ya Arusha inawezekana wafanyakazi wa pale pahala wakaona wafanye hivyo kwa sababu anatoka nje ya Zanzibar sijui. Kwa hiyo, mimi sijashauriwa wala siyo utaratibu kumpa mtoto majina ovyo mtoto kwa sababu hatutaki kumpoteza na mahali ambapo anapaswa atoke. *(Makofi)*

Tunashajihisha kabisa kwamba mtoto yeyote kama kuna asili ya kuweza kum-*tress* kama yuko kwenye kituo cha watoto anaruhusiwa a-*tress* anaruhusiwa kwa sababu lengo na madhumuni ni kulea watoto wenye familia siyo kuwatenga na kuwatenganisha katika jamii yao.

Mhe. Spika, suala la ubaguzi najua halipo niliyosema ni kwa sababu tu kaitwa jina la Maudline angepewa jina jengine je lisingelisemwa, na ninaloshukuru kwamba amenikomesha lakini kaomba msamaha. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tunatunga sheria na haya si maneno yangu kifungu cha 7 cha sheria ya mtoto namba 6 ya mwaka 2011 mtoto akishakuokotwa apewe jina. Kwa hivyo, hajapewa jina na wizara kwa sababu gani.

Mhe. Mwenyekiti: Mtoto kaitwa Maudline jina kapewa, jina la Mhe. Waziri au vipi, hebu liweke vizuri Mhe. Jaku liweke vizuri hilo jambo lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mtoto akishaokotwa kwa mujibu wa sheria yule mtoto anatakiwa apewe jina siyo baadae apelekewe yeye ndo atoe jina na mtoto kapokelewa muda mrefu, mtoto kaokotwa muda mrefu na sheria namba 7 ya 2011 namba 6.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mweyekiti, nimtoe wasi wasi mtoto anapewa jina kwa sababu ni alama asipokuwa na jina tutamtambuaje, atalishwaje maziwa wakati wa kunyweshwa pasipokuwa na jina atapelekwaje hospitali asipokuwa na jina hili limetolewa kwa muda tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hoja ya Mhe. Mjumbe ni kwamba jina limechelewa kutolewa jina kwamba watu walikuwa wanasubiri mpaka Mhe. Waziri aseme.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mweyekiti, hakuna aliyesema mimi sijashauriwa katika hili wamelipenda tu jina langu, Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama unataka kuzaa mtoto mpe jina langu zuri Maudline halina tatizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, atwambie jina lake nani huyo mtoto, ili tuendelee tuje na hoja nyingine.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, mtoto anaitwa nani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Sijui jina lake mtoto naambiwa kama anavyosema kapewa jina Maudline lina tatizo, wametoa wale watu wa mle ndani wapate alama sasa kama ana jina zuri apeleke.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nije na hoja yangu ya pili huyo mtoto anaweza akawa Mkristo au Muislam sijui tena huko. Hoja yangu ya pili kwenye fungu Maendeleo ya Wanawake ya Kupinga Udhalilishaji SQ010303 nishawasha mjomba hiyo kuna bilioni 1,775,000,000 pesa nyingi sana walizopewa hizo maana baada ya kupungua haya matatizo ya kesi ndiyo kwanza yanazidi. Kuna Ofisi ya *DPP* na nilimwambia hapa Mwenyekiti wa Kamati Bajeti Mhe. Mohammed Said Mohammed hizi pesa ikiwezekana zipunguzwe wapelekewe *DPP* hasa Pemba wanapelekewa 3,000,000 tu mafuta hayatoshi hizi pesa nyingi sana na haya matatizo hayapungui yanazidi bilioni 1.7 ni pesa nyingi mno. Mimi ni Mjumbe wa kamati lakini kwa bahati mbaya siku hiyo nilikuwa sipo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti namuomba Waziri wa Fedha na Mipango anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba hicho kiasi cha fedha ni kikubwa sana na alikuwa anapendekeza kipelekwe kwa *DPP*. Tumsikilize Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kuweka vifungu hivi ni kwamba baada ya kupewa fungu lao *ceiling* wizara inakaa kwa mujibu wa mazingatio ya shughuli wanazotaka kuzifanya kwa mwaka ule. Kamati yao pia imekaa imepitisha nasikia na Mhe. Jaku Hashim Ayoub pia Mjumbe kwa hivyo wamekaa wamepitisha vifungu hivi na vipo kwa mujibu wa shughuli zinazokusudiwa kupangwa wala huwa hawaingiliwi kiutaratibu wao.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwanza unatoa funzo kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba wawe wanahudhuria vikao vya kamati, kwa sababu kumbe wewe ni Mjumbe wa kamati hii lakini siku ya shughuli hii wewe hukuwepo. Tunafahamu dharura zako Mhe. Mjumbe ulikuwa Bungeni na zinakubalika kwa sababu tulikuchagua wende ukatuwakilishe. Sasa itabidi tuache tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zinaturuhusu hizi kupunguza fungu. Nimesema kwamba nilikuwa sipo katika mchango wangu nilikiri wala sitaki kubishana, tunataka kuokoa pesa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ngojea akusaidie Mwenyekiti wako wa kamati, siyo utaratibu lakini nitampa azungumze.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa rasmi tulipokaa katika kamati Mhe. Jaku Hashim Ayoub taarifa anayo, na baada ya kuwa nayo mara baada ya kurudi nikampa taarifa yote tumefanya moja, mbili tatu na kitabu anacho hakutoa hoja wakati huo. Na tunamshukuru sana Mwenyekiti wa bajeti baada ya maelezo mazuri ya wenzetu wa wizara tulishirikiana vyema

kwamba fungu hili lipite pamoja na yeye kuona fedha nyingi lakini hivi vitendo vinaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Mhe. Mjumbe naomba ukae inatosha. Tunaendelea Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Jaku Hashim Ayoub tumemaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kitu cha mwanzo walichotufundisha wazee kumuheshimu mkubwa na mdogo. Sasa kushindana na Mhe. Mwenyekiti wangu itakuwa sijamfanyia haki, tuendelee.

Kifungu	PQ0103	Jumla ya Progrmu Kuu ya Hifadhi ya Jamii na Maendeleo ya Wanawake na Watoto	10,220,545,000
Kifungu	PQ0104	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uraribu wa Wizara ya Kazi Uwezeshaji wa Wazee Wanawake na Watoto	

Mhe. Mwenyekiti: Tutaanza na Mhe. Suleiman Sarahan Said atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Abdalla Maulid Diwani.
Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe.Mwenyekiti, sina shida sana ya kuzuia kifungu lakini nilikuwa nasema kwamba katika kifungu FQ010403 Uratibu wa Utekelezaji wa shughuli za wizara Pemba nilikuwa namwambia Mhe. Waziri kwamba kwa niaba yake wizara yake iliyoko Pemba ni kwamba katika jimbo langu naomba mkopo au taarifa yoyoye za fedha katika jimbo langu anitaarifu nikiwepo na nisipokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hilo ni ombi tu kutoka kwa Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimelipokea kwa heshima zote.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nilipokwa nikichangia niliweka nia ya kuzuia vifungu pamoja na kuunda kamati ya teule, kutumia Kanuni ya 111 kwa sababu wizara hii kuna mambo zaidi ya kesi tano, sita, saba zipo na kama tatu nazifahamu nikasema kwamba kuna haja ya kuunda kamati teule. Nimesimama hapa kuwekea mkazo hoja yangu ya kwamba kuna mambo yamekiukwa katiba na sheria hasa kuangalia hata kuingiliana na mihimili mingine. Sasa hoja yangu ipo hapo mimi niliweka nia hiyo na nilisema kabisa na nilitoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe Waziri, nafikiri utakuwa umeshaifahamu hiyo hoja yenyewe inayozungumziwa. Mwambie hiyo hoja yenyewe ili aweze kuitolea ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, huko kuna *echo* sisikii vizuri *unless* anasema taratibu sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mwambie hiyo hoja yenyewe ili aweze kuitolea ufafanuzi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Kwa kamati teule kiasi asisikie, kwa sababu keshajua kamati teule nimezungumza wizara husika kupitia yeye mwenyewe waziri pamoja na wajumbe baadhi yao wa ustawi wa jamii wanafanya mambo kuingilia mihimili pamoja na kukiuka katiba na sheria za nchi kupitia wizara yao. Sasa ni vyema kwamba tunataka tuunde Kamati Teule na nilipendekeza wakati nikichangia nilitoa hoja kwamba tuunde Kamati Teule, ili tukafanye uchunguzi zaidi wa masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kamati ikakague wizara hoja yako hasa nini yaani iundwe ikachunguze jambo gani.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Hoja yangu ya wale watoto zile kesi ambazo tumezizungumza zipo katika kuchangia nilitoa mifano na maelezo yangu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hebu kama unaweza kuna kesi ya watoto anasema.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwekezaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba aweke wazi kila kitu ni vizuri akatusaidia, ili tujue tunafanya nini.

Mhe. Nadir Abdul - latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, hoja niliyoizungumza mwanzo kwamba Mhe. Waziri kuna kesi ya mwanzo iliyofanyika ya kutoroshwa mtoto alihusika, lakini sasa hivi kuna kesi nyingine hiyo aliyozungumza huyo huyo shekh Salim ambayo vile vile kwa njia moja au mbili pia kahusika na ushahidi tunao. Na ukiacha kuna rikodi nyingine ambazo zipo zinahusu wizara yake kupitia na ustawi wa jamii ndiyo maana nikatoa maelezo ya kuunda kamati teule tukafanye uchunguzi hapa hatutaki kutoa maelezo yote mkiniambia nitoe maelezo nataka dakika ishirini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani hiyo kamati teule hebu iangalie vizuri hiyo kanuni, hatuwezi kuunda kamati teule kuchunguza mambo yote, yaani *almost* kama wizara tukaichunguze ungelikuwa na *issue specific*, mtoto yule aliyetoroshwa labda ndo tu-*deal* na hilo suala moja tu.

Mhe. Nadir Abdul - latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti ndiyo hiyo ya pili ile ya mwanzo naachana nayo, hii iliyotokea sasa hivi *currently* ipo hii kesi ambayo nimeitolea maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa, inabidi tuipe serikali muda ituridhishe ikishindwa kuturidhisha serikali ndio hapo tunapoweza kufikia maamuzi tena baadae ya kusema kwamba tunaunda kamati na hatuiundi hapa. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nimemfahamu vizuri Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf anazungumzia suala la kesi iliyoko kwa kashfa inayomhusu baba na mama mtoto walioachana, ambao kuna shauri sasa liko mahkamani kwenye Mahkama ya Kadhi kati ya mume na mke ili kuchukuliwa *fatuwa* kwa mujibu wa kazi zitazotoka ndipo tupate majibu.

Kwa kuwa hilo shauri lenyewe lipo mahakamani na lipo kwa kadhi inabidi Mahakama ya Kadhi itoe *fatuwa* hatuwezi sisi hapa Barazani tukatoa hukumu ya watu wawili kwa ridhaa zao

walikubaliana kwanza kuona na baadae kwa mujibu wa sheria zetu wanaachana na wamepata watoto sasa watoto kila mmoja anavutia watoto wake. Sasa kwa sababu Mahkama ya Kadhi ina utaratibu ina utaratibu kwa mujibu wa sheria zetu na pia na sheria za kidini Mahkama ya Kadhi itatoa *fatuwa* hiyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akavuta subira akangojea majibu hayo. Serikali haiwezi kuingilia suala ambalo lipo katika Mahkama ya Kadhi au lipo Mahkama. Ahsante Mhe, Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ni mzoefu na anaweza akamtoa nyoka pangoni mimi *concern* yangu iko hapa, Mhe. Waziri lakini matokeo yake wizara yake ikatumia njia nyingine za kwenda kudanganya Mahakama ya Mhe. Hakimu pale mjini akenda akafungua jalada jengine la kesi ya watoto kusema kwamba mahakama ile haifai wakafungua wakadanganya ikafunguliwa kesi juu ya kesi. Sasa *concern* yangu iko hapo kwamba kesi wanafahamu wizara kama kesi ipo huku na sisi tuna mahakama yetu iwe mahakama ya mambo ya kidini sisi hatuitaki tunakwenda kufungua huko kaenda kudanganya kule Mahkama ya mjini ya Watoto, hiyo ndio *issue* ambayo inafahamika si kama mimi sikatai namuheshimu sana mzee wangu lakini kwa suala hili kidogo anisamehe *concern* iko hapo watu wanafahamu vizuri kwamba kesi lakini wamekwenda ku-*cheat* huko.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kuna kesi kwenye chombo chochote, iwe hiyo mahkama nyengine ya kawaida au Mahkama ya Kadhi kama kesi ipo, hili shauri inabidi tuliondoshe tu kama hakuna ndio tunaweza tukazungumza. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, anavyoeleza Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ni kweli, kwenye masuala kwamba huyo mama mwenye watoto alifungua tena shauri kwenye Mahkama ya Wilaya na Mahakama ya Wilaya ilipoelewa kuna shauri katika Mahkama ya Kadhi imerudisha suala hilo tena kwenye Mahkama ya Kadhi. Kwa hivyo, suala hilo bado lipo kwenye Mahkama ya Kadhi na ndiyo itakayotoa *fatuwa* ya hukumu nini kifanyike. Kwa hivyo, bado hata kama mama muhusika wa mwana alikwenda kwenye Mahkama ya Wilaya kufungua shauri jengine wakati akijua kwenye Mahkama ya Kadhi lipo shauri baada ya Hakimu wa Wilaya kuelewa kwamba shauri lipo Mahkama ya Kadhi, Hakimu wa Wilaya alirudisha hilo shauri liendelee katika Mahkama ya Kadhi. Kwa maana hiyo, sasa inayongojewa ni *fatuwa* ya Mahkama ya Kadhi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima ya Chama cha Mapinduzi na Ramadhani hii ndiyo hili suala naliwacha lakini hili suala ni zito na imepita dharau kubwa hasa kwa Hakimu wetu wa kwenye masuala yetu ya dini imedharaulika vibaya. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kwa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nashukuru, kwa sababu hilo suala limerejeshwa kwenye Mahkama ya Kadhi, nadhani tusubiri Kadhi atakaloamua halafu sote tutafaidika na hilo. Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante, sana Mhe. Mwenyekiti, naomba mimi kidogo niweke sawa kwa sababu nyaraka mimi ninazo ya hili suala, hilo hilo mlikuwa mnavutana tu hapa kuna maamuzi ya Mahkama ya Mkoa naomba nikupe karatasi hizi zikusaidie Mhe. Mwenyekiti

yametoka tarehe 30/04 lakini kesi imefunguliwa Mahkama ya Kadhi tarehe 27/04 kwa hivyo imekwenda kupandishiwa, hii *summons* ya kufungua kesi. Kesi hiyo ya mtoto ambayo inamuhusu bwana Salum Mohammed Hassan na bibi Zainab. Hiyo ni hukumu au maamuzi ya Mahkama ya Mkoa kesi ya Mahkama ya Watoto hii ni ufunguzi wa kesi Mahkama ya Kadhi, kwa hivyo huyu kenda mwanzo kuliko huyo sijui tuko sawa, lakini huyu katakiwa haraka tu atoe maamuzi ili kumkandamiza huyu Kadhi**. N**dipo panapo changamoto katika suala hilo naomba na hii nikukabidhi, ili utumie hekima zako tuone hili jambo sio rahisi kiasi hichi zinavyochukuliwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yamekaa vizuri sana.

Wajumbe: Aaaaaa!

Mhe. Mwenyekiti: Subirini niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alisema ni kweli kulikuwa kuna shauri liko Mahkama ya Kadhi lakini likatoka shauri jengine ambalo ndio hili ambalo anasema la Mahkama ya Mkoa, huyu wa Mkoa baada ya kujua kamba kulikuwa kuna shauri Mahkama ya Kadhi, ameamua kwamba aaa shauri hili hatuwezi kuendelea nalo wala haya maamuzi ambayo nimeyatoa lazima lirudi kule kwa Kadhi.

Kwa hivyo, alichosema Mhe. Waziri kwamba shauri hili lipo lakini lipo kwa Kadhi sasa hivi halipo tena huku serikalini yaani kwa Mahakama ile ya Mkoa sijui Wilaya.

MUONGOZO

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba usubiri kwanza msubiri Waziri atoe ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri Mahakama ya kadhi na Mahakama ya Wilaya zote ziko chini ya Mamlaka ya Wizara yangu, kwa hivyo mimi naahidi kwamba nitalifuatilia na jawabu nitaleta hapa inshaallah.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, muongozo.

Mhe. Mwenyekit: Mhe. Mwenyekiti, nadhani ungemuacha mwenye shauri akamaliza ndio halafu tukakusikiliza wewe. Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko hivi ilipofunguliwa kesi hii kwenye Mahkama ya Kadhi ndio wenyewe wenye kuhusika na ndoa, talaka na mambo mengine imekwenda vizuri hii kesi. Ndio maana katika mchango wangu

nikasema Idara yake ya Ustawi wa Jamii inaingilia kesi za Mahakamani nina ushahidi tosha, kupitia Waziri mwenyewe kwa sababu ana uhusiano alizungumza pale kwamba ni wifi yake huyu bibi, anawaambia ata kama hawa wamekwenda kuruka huku sie twende huku, sijui unafahamu kesi yangu. Huku Mahkama ya Kadhi haijasikiliza kesi ndio kwanza inafunguliwa kesi huyu inapangwa tarehe ya kusikilizwa huku yanatoka maamuzi uharaka gani.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kesi zaidi ya miezi mitano miezi sita mpaka miaka miwili zipo hii kuna uharaka gani uliopelekea hata kwamba iwe haraka huyo Jaji Naila katoa maamuzi moja kwa moja kuwafedha hawa huku na kutumia nguvu, alitoa mpaka *summons* watoto kwenda kuchukuliwa ndani ya nyumba wakati kesi ile iko mahakamani. Je, hapa si kuingilia muhimili. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili: Mhe. Mwenyekiti, kama niliviyosema awali jaji mwanzo alipotoa hiyo *summons* ya mwanzo alikuwa hajaeleza kama kuna kesi iko Mahkama ya Kadhi, wakati hakimu alipotoa hukumu alikuwa hajaelewa kama kuna kesi iko Mahakama ya Kadhi, baada ya kwisha kueleweshwa kwamba kuna shauri linaendelea kwenye Mahkama ya Kadhi hakimu akafuta uamuzi akairudisha hii kesi iendelee kwenye Mahkama ya Kadhi, hii kesi sasa ipo kwenye Mahkama ya Kadhi hivi tunavyoijadili hapa itafika mahala tuidondoshe Mahakama yetu ambayo ina iwezo wa kufanya maamuzi na tutaanza ku-*influence* kupata maamuzi ya wajumbe.

Ni vizuri jambo lilioko kwenye shauri katika mahkama hatulizungumzia hapa tuiachie mahkama itoe uamuzi, kama kuna jambo lolote limefanyika kinyume na utaratibu wa kisheria kwa mujibu wa sheria unatakiwa uende tena kufuata taratibu za kisheria kurudisha hilo, chombo hichi hatuwezi kuingilia mambo yaliyokuwepo mahakamani Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nafikiri hilo liko wazi Waheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, muongozo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hebu subiri kwanza una haraka sana. Mhe. Abdalla Maulid Diwani, nadhani utakuwa umeridhika na haya maelezo sasa ya Mhe. Waziri na suala hili liko mahakamani kwa maana ya Mahkama ya Kadhi sio ya Mkoa, kwa sababu wale waliokwenda kule wametoa kimakosa wamelirejesha tena kwa kadhi ndio *point* ya Mhe. Waziri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante, Mhe. Mwwenyekiti nimekufahamu na nimeelewa yote kwa hisani yangu na nafikiri Waziri mwenye kushughulika na masuala ya Katiba na Sheria kazungumza, lakini hapa tupo katika kupitisha bajeti na kila siku kesi kama hizi kigezo kwamba ziko mahakamani hatuzizungumzi zinafichwa, kila siku kesi kama hizi tunaambiwa ziko mahakamani tunanyamazishwa tusiseme.

Je, Mhe. Waziri anaji-*commit* vipi kwamba lini tutaweza kujua mustakbali au mwenendo mzima wa ile kesi kule mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani hili keshalibeba Mhe. Waziri ambae anahusika na hizi mahakama zote, nadhani tumuachie afanye shughuli yake.

Naam sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa una muongozo.

MUONGOZO

Mhe. Miraji Khamis Kwaza: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba muongozo kwa sababu kiti chako serikali, Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwenye jambo hili kwa sababu tuko kwenye chombo kimoja kikubwa kauli zinapishana, Mhe. Abdalla Maulid Diwani katoa ushahidi kama hawa watu wamehukumu kesi, lakini serikali wanasema imehamishwa kesi maana kama kafuta lile shauri limerejeshwa kwenye chombo kilichopo zamani, busara ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani ile barua kakupa ile ya Mahakama ya Mkoa kuhusu watoto kiti chako kitusomee ni hukumu, kama ni hukumu tutajua inasemaje maelezo ya Waziri kama imehamishwa tutajua. Lakini kama haikuhamishwa imetolewa hukumu tutajua ikisha kiti chao kitoa muongozo wa hili, tusilifanye kuwa jepesi tukakosa utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nadhani hakuna haja hata ya kukusomea kwa sababu tayari maelezo yameshatoka hata kama ilihukumiwa lakini alifahamishwa kwamba kulikuwa kuna shauri liko chini lilikuwa lishaanza na ameshalirudisha, anayezungumza hapo ni mtu lakini ni serikali. Serikali imeshasema hata kama pana karatasi hapa lakini wenyewe wameshasema serikali kwamba hili shauri lisharudishwa kwa Mahkama ya Kadhi. Sasa sijui tunavutana nini, mimi nafikiri tulikwisha kuelewana Waheshimiwa Wajumbe naomba tusipoteze muda, naomba ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, uzoefu na tuko katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani pana kesi na sitakiwi kuzungumza kwa kanuni mtoto Ibrahim Mzee kesi iko mahakamani na mtoto kaondoshwa, kwa hivyo hii wizara ina matatizo huu hapa ushahidi nakala zote, Mtoto Ibrahim Mzee serikali hii hii ndani katuahidi serikali hii haijabadilika tutaletewa taratibu humu ndani na *hansard* zipo hatujajibiwa mpaka leo, kwamba Waheshimiwa Mawaziri mnatusokota. Ndio yale mnakaa maofisini uzoefu wizara ina mambo ambayo si mazuri hii hapa….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba ukae

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri hili jambo limeshakaa vizuri tusilikoroge tuendeleeni tu. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, naomba ukae. Mhe. Mwanasheria Mkuu, naomba unyanyuke kama unacho chochote cha kusema.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na *ofcourse* mengi yamesemwa lakini kwanza lazima tukumbuke….

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tusikilizane naomba tumsikilize Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Kwanza lazima tukumbe kwanza na turudi kwenye Kanuni ya 37(3)(ix) kama kuna jambo ambalo lipo kwenye Mahakama maana yake kanuni yetu inatukataza kulijadili jambo ambalo liko kwenye Mahakama.

Lakini pia turudi kwenye misingi ya katiba yetu ambayo inasema kuna *separation of power* na kila mtu anasimamia eneo lake, nafahamu Waheshimiwa Wajumbe wana hamu ya kujua mambo ambayo yanaendelea ndani ya mahakama. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mahakama ina utaratibu wake, kama kuna mazonge ambayo yametokea bado kuna utaratibu wa kukata rufaa, huo ndio utaratibu wa mahakama ambao upo na hizi kesi zote zimeanza kwenye Mahkama ya Mwanzo au chini.

Lakini, mahkama iliiyopewa mamlaka ya kusikiliza mashauri yote ni Mahkama Kuu hii ndio ina *unlimited jurisdiction* ya kusikiliza mashauri haya yote. Sasa kama kuna mazonge ambayo yametokea huko chini bado mahakama ina nafasi ya kutoa maelekezo Mahakama Kuu ya namna gani shauri hili lisikilizwe. Sisi kama alivyosema Mhe. Waziri tunalichukua tutalifuatilia na lifuate misingi ya sheria ya kusikiliza hiyo kesi mpaka kutolewa hukumu yake.

Kwa sasa hatutoweza kuanza kujadili ilikuwa mahakama ipi imetoka wapi imekwenda wapi, kwa sababu na hizo kumbu kumbu nyengine hatuna. Mhe. Abdalla Maulid Diwani kaja na zake ukimwambia Mheshimiwa Mjumbe mwengine atakuja na zake, wajibu wetu ni kufuatilia na kushauri pande zote mbili zinazohusika kufuata utaratibu wa kisheria nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu tunaongozwa na kanuni Mhe. *AG* kazungumza lakini tuna kanuni 147 kutenga kanuni kando, lakini hata vile vile kataja Katiba ya Zanzibar lakini Katiba ya Zanzibar 88 Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya katiba hii vitafanya kazi kwa mambo yafuatayo.

a) Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unapohitajika kuwepo
b) Kujadili shughuli za kila Wizara wakati wa kikao cha mwaka wa bajeti ya Baraza la Wawakilishi.

c) Kuuliza masuala mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi.
d) Kuidhinisha na kusimamia mipango ya Maendeleo ya Serikali katika njia ile ambayo bajeti ya mwaka imeidhinishwa hii ni kazi yetu.

Kwa kweli, hili lakini uzoefu wa wizara mtoto mahakama imezuia kuna Ofisi ya Mufti imezuia, Mkuu wa Mkoa, Polisi tunafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, bado unarudi kule kule ilikuwa tumeshalimaliza shauri kwanza umeongea bila ya ruhusa yangu umeingilia kati tu naomba tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti nilikuwa na hoja mbili pale..

Mhe. Mwenyekiti: Nilikusahau endelea sasa Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ya pili wakati nachangia niliuliza mustakbali mzima wa Nyumba ya Kulelea Watoto ya Mazizini, mimi na mwenzangu mmoja tulizuia lakini mimi nilimpita nini mustakbali wake, tukataka kujua ile nyumba tupate tamko ya serikali, ya kampuni au taasisi ama mtu na kama kampuni imeweza vipi kufunga baadhi ya vyumba ambavyo watoto wale wasivitumie jibu lile sijapata, naomba jibu langu tafadhali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri anavyoendelea kujibu vizuri masuala yanayohusu wizara hii, pia nimshukuru Mhe. Abdalla Diwani Maulid kwa swali lake.

Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa kwamba kiwanja kile cha Nyumba ya Kulelea Watoto awali kiliombwa na *ZAYEDESA* na hati ilitoka ya *ZAYEDESA*, kukawa na mkataba maalum kati ya *ZAYEDESA* na wizara husika kwa msingi kwamba jengo lile litashughulikiwa na wizara yetu hii, ili watoto waweze kulelewa vizuri. Kwa msingi huu *ZAYEDESA* walikabidhi serikali ili itumike jengo lile kwa shughuli ya kulelea watoto.

Katika mkataba ule kuna vyumba viwili viliombwa hapo awali kwa mujibu wa mkataba vitumike kwa ajili ya kuweka vifaa vya *ZAYEDESA*, kinachofanyika sasa ni kwamba wizara husika kuendelea kuzungumza na *ZAYEDESA*, ili hata hivyo vyumba viwili kwanza viweze kutumika kwa shughuli za kulelea watoto, huko mbele taratibu nyengine zitakwenda ili tuzungumze na *ZAYEDESA* kwa msingi kwamba jengo lile liwe na umiliki wa asilimia mia moja kwa serikali ili litumike kwa malengo ambayo Wajumbe wa Baraza lako tukufu wanapenda litumike ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimefarijika kumsikia Mhe. Waziri kuweka wazi kwamba ile nyumba ni ya *ZAYEDESA*, lakini watoto wale walikuwa katika Nyumba ya Kulelea Watoto Forodhani ambayo ni ya serikali, yaani watoto wa serikali, sasa vipi watolewe kwenye nyumba ya serikali, watoto wa serikali waje kuletwa kwenye nyumba ya *ZAYEDESA* nyumba ya taasisi fulani, hapa mimi sifahamu naomba maelezo niwekwe sawa.

Kwa kweli, sababu gani iliyopelekea kuwatoa watoto Forodhani kwenye nyumba ya serikali na watoto wa serikali, kuletwa kwenye nyumba ya *ZAYEDESA* kwenye nyumba ya taasisi kwa namna gani naomba muongozo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nina hakika Mhe. Abdalla Maulid Diwani anajua kwa nini maamuzi yale yalitokea wakati wa awamu ya sita, kwa sababu serikali ni endelevu hatuwezi kulaumu maamuzi ambayo yalifanyika, inabidi kama serikali tuheshimu maamuzi yaliyopita. Lakini sababu zilizojitokeza wakati ule jengo lile lilikuwa haliko hali nzuri na wakati huo *ZAYEDESA* walijishughulisha sana na kutoa huduma mbali mbali kwa watoto.

Kwa hivyo, serikali kwa wakati huo iliona busara kuwapa *ZAYEDESA* wajenge nyumba ya watoto na kutokana na mazingira yaliyojitokeza katika jengo lile kwa wakati huo, ilibidi watoto wale wahamishwe kupelekwa kule, lakini serikali ikawa inasimamia kuwalea watoto wale.

Kwa sasa, serikali inaona ni vizuri tuendelee kuzungumza na wenzetu wa *ZAYEDESA*, ili jengo hili liwe chini ya milki ya serikali na watoto wale waweze kukaa kwa vizuri zaidi chini ya usimamizi wa serikali. Lakini tukubali kwamba mwanzo walipewa *ZAYEDESA* na kwa kiasi fulani *ZAYEDESA* sio tu kwamba walitoa fedha za kujengea lile jengo, lakini taasisi mbali mbali za serikali zilitoa mchango mkubwa katika kujenga jengo lile na wahisani na wafadhili mbali mbali ikiwemo na serikali yenyewe ilisaidia kujengwa katika eneo lile. Msingi wake lilijengwa kwa dhamira kwamba watalelewa watoto, kwa hivyo kila aliyetoa hiyo fedha walitoa fedha kwamba eneo lile litumike kwa kulelea watoto na *ZAYEDESA* wenyewe wanajua kwamba jengo lile kwa ajili ya kulelea watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo naamini haitokuwa shida tutakapozungumza na wenzetu wa *ZAYEDESA* katika kuliweka jambo hili katika misingi mizuri zaidi bila ya kuleta malumbano, sote tunaelewa kwamba *ZAYEDESA* wamefanya kazi kubwa na nzuri. Kwa hivyo, tuwapongeze wenzetu wamefanya kazi hiyo tunataka tuwaambie Waheshimiwa Wajumbe waipe nafasi wizara iendelee na mazungumzo yake, ili hilo lengo lao ndio lengo la wizara ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wanasema akisimama Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pale palipokuwa pagumu panalainika sijui ana uchawi gani anaotumia. Lakini, bado nasimamia hoja yangu pale pale ni

kwamba watoto wamehamisha Forodhani kwenye Nyumba ya Kulelea Watoto ya Serikali, inavyosadikika kwamba ile nyumba baadhi ya hao watu waliojenga huko *ZAYEDESA* wametengeneza *restaurant* kule kuna mabaa na ile nyumba kwa historia ilikuwa maktaba ya kiislam. Sasa je kauli anayotwambia Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ile Nyumba yetu ya Forodhani iko kwenye mikono ya nani nikishapata hilo jibu basi mimi nitatoa ruhusa tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, jengo au nyumba ya Forodhani lipo kwenye mikono ya serikali na ni mali ya serikali na itaendelea kuwa mali ya milki ya serikali, wote waliokuwepo pale walipangishwa kwa mujibu wa taratibu za kiserikali. Lakini sasa dhamira kubwa ni kulifanya jengo lile kuwa kumbu kumbu ya kihistoria katika nchi yetu, limo katika mpango wa kukarabatiwa vizuri sana ili litumike kwa ajili ya historia ya nchi yetu.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako kwa sababu suala hili Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii katika kujibu maswali ya hapa ya Barazani ya Waheshimiwa Wawakilishi katamka bayana fawahisha kwamba nyumba ile ni nyumba ya serikali, leo Mhe. Waziri……

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, subiri ipi hiyo.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Nyumba hii ya *ZAYEDESA* iliyowekwa watoto Mazizini, Mhe. Naibu Waziri katika kujibu kajibu *live* kwamba ni nyumba ya serikali, leo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais anatwambia hiyo nyumba ya *ZAYEDESA*. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri mmoja wapo leo afute kauli yake. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sisi ni binaadam kawaida ya binadamu wakati mwengine unaweza kupitikiwa na hasa ukitizama namna ambavyo lile jengo linavyoendeshwa, kwa sababu huo mkataba ni wa zamani na jengo lile namna linavyoendeshwa mtu yoyote atakuwa na dhana kama dhana aliyokuwa nayo Mhe. Naibu Waziri kwa sababu linasimamiwa na serikali, watoto wale wanahudumiwa na serikali, wafanyakazi wa pale wanalipwa na serikali, kila jambo linafanywa na serikali.

Kwa hivyo, kwa tafsiri ya haraka haraka mtu anaweza akaona kabisa kabisa kama binaadamu kwamba lile jengo la kiserikali, lakini ukweli ni kwamba jengo lile liko chini ya jina la *ZAYADESA* na sasa kwa sababu madhumuni makubwa ni kulelea watoto tutazungumza na wenzetu wa *ZAYADESA*, ili hili lengo ambalo Waheshimiwa Wajumbe, wanalitaka naamini *ZAYADESA* tutakubaliana nao. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan Said, Waheshimiwa wajumbe hukuonesha nia

Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf: Na mimi hoja yangu hiyo hiyo nimechangia.,

Mhe. Mwenyekiti: Hapana hukuonesha nia kwa sababu wamenyanyuka watu watatu, nikawataja Mheshimiwa. Nilimtaja Mhe. Abdalla Maulid Diwani,

Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf: Na mimi nimo nimechangia na nimeinuka.

Mhe. Mwenyekiti: Haya subiri, Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naondoka kwenye eneo hilo nakuja kwenye SQ010503 Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja kazini. Kusimamia Utekelezaji wa Sheria za Kazi na Mkataba wa Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, Waheshimiwa naomba tusikilizane, endelea Mhe. Mjumbe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nasimamia fungu hilo, wakati nachangia hoja niliwahi kumwambia Mhe. Waziri aje anielekeze kwamba sisi ni kisiwa na tumetafuta ajira sana katika mataifa ya nje ili vijana wetu waende huko kwenda kufanya ajira.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti, viwango vya kazi hiyo au vipi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, viwango vya kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Hatujafika huko.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Fungu ndio hili hili Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana ukurasa wa pili hebu angalia ukurasa wa mwisho.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Hakuna fungu ndio hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, lipo fungu nitakupa hiyo nafasi. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf

Mhe. Nadir Abdul latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, sisi sote *Alhamdulilah* tunashukuru Mwenye ezi Mungu.,

Mhe. Mwenyekiti: Jaribu kuwa-*brief* kidogo Mhe. Mjumbe kwa sababu ya wakati.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Naam

Mhe. Mwenyekiti: Jaribu kuwa-*brief* kidogo kwa sababu ya wakati.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, basi bora tupanguwe wakati kwa sababu ah!

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, endelea.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti sisi sote *Alhamdulilahi* tuko vizuri na wale tunaowatetea ni watoto yatima ambao wengi wao hawana baba na mama, wizara au serikali kwa ujumla tumemsikia Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais, anasema kwamba jengo lile la mwanzo nipo kwenye taratibu na ukarabati wa siku za mbele kufanya sehemu ya historia. Kwa hivyo, anatuhakikishia vipi kwamba jengo lile hata kwa siku za mbele halitokuja kubadilika na kurudi kwenye mikono ya watu hao waliofanya *plan* ya kutaka kuchukua jengo lile kuja kufanya hoteli au *investment* ya mambo haya ya utalii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa anataka kuhakikishiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe. Nadir Abdul latif kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, lile jengo la Forodhani kama nilivyosema awali ni milki ya serikali itaendelea kuwa milki ya serikali, na serikali ina mipango ya kulikarabati, liwe katika hali nzuri na moja katika matumizi yake kutakuwa ni mambo ya kumbukumbu ya kihistoria. Kwa kweli, lile jengo lina historia ndefu, kilikuwa ni Chuo cha Kiislamu hapo awali kwa hivyo katika mambo yake ya historia pia yatakuwemo na mambo yenye maelezo ya kiislamu. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe waiamini serikali kwamba dhamira yake ni kulitengeneza na kuimarisha, na kuliendeleza kwa kumbukumbu za historia yetu. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul latif nadhani utakuwa usharidhika.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar tunaiamini asilimia zote na tunakuwaminini mawaziri sana, wachache tu tunakuwa hatuwamini kwa sababu wanakuwa wanageuka geuka. Ninachotaka kusema kwamba kwa nini tokea siku hizo zaidi ya miaka mitano hamjaanza kulitengeneza, kwa sababu sisi tushapekura sana lile eneo, au lile jengo kuna watu wametaka kulirithi kufanya masuala ya hoteli au masuala mengine *investment* kwenye masuala ya utalii.

Lakini, leo tunasikia jengo lile serikali inatwambia ni masuala ya kihistoria yatakuja kufanyika na makumbusho. Hivyo, naomba tuhakikishiwe Mhe. Waziri lini labda mna taratibu wa kuanza haya matengenezo na kweli kwamba yatakuwa maonesho ya historia na sio mtu tena aje apewe asema kakabidhiwa afanye yeye.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf bado uko kwenye jengo, lakini hoja yako ya mwanzo ilikuwa uhakikishiwe kwamba halitoenda kwenye mikono binafsi. Sasa unataka uhakikishiwe tena, Mheshimiwa unatuzungusha hapo kwa hapo naomba tuendelee Waheshimiwa naomba tuendelee.

Kifungu PQ 0104	Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kazi Uwezeshaji Wazee na Wanawake na Watoto.	3,016,361,000
Kifungu PQ0105	Usimamizi wa Sheria Kazi, Ukaguzi Kazi	

Na Kazi Staha kwa wote

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Jaku nimekuona.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi nasimama kwenye SQ010503 Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini, Kusimamia Utekelezaji wa sheria za Kazi na Mikataba ya Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa ni Kisiwa na sisi hapa ni kwamba utaratibu wetu sana, tumefanya kwa kutafuta kila hali kwa vijana wetu kupata ajira nchi za nje, lakini sasa hivi nimemuona katika kitabu cha Mhe. Waziri hapa kuna utaratibu mwingi wa watu wetu ambao ni vijana ambao wanafanya kazi katika nchi za nje. Lakini pia katika majadiliano bado serikali kuna tatizo la uzuiaji wa hizi mambo kwenda kufanya shughuli nje, hivi sasa waziri anipe maelekezo ya vijana wetu ambao wanafanya kazi nje wamezuiliwa, wanaendelea au inakuwaje.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nataka kumwambia Mhe. Suleiman Sarahan, kwamba sisi kwa upande wa Zanzibar hatujazuia na ndio maana wanaendelea ndio maana juzi umeona watoto wameondoka. Na wanaendelea hivyo kwa sababu hakujawa na utaratibu wowote unaohusiana na kuwazuiya kwa upande wa Zanzibar, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zuio kwa upande wa Zanzibar halipo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti lakini kidogo kuna pande mbili, kuna pande ambazo zinasimama kwa mambo ya wanawake na watoto mambo ya kwenda kufanya kazi kama mambo ya majumbani, lakini kuna na kama vyuo vyetu vya *Danaos* ambavyo vinatumia sana mambo ya meli na kila kitu hii anaisemeyaje.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hii ni tofauti *Danaos* ni mambo ya ubaharia, sijui Mhe. Waziri,

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Sijamsikia vizuri nimemsikia meli tu mwishoni.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Waziri amejibu ni sawa kuna baadhi ya vijana wameondoka juzi ambao wanafanya kazi za majumbani nchi za nje, lakini kuna vijana wetu ambao hapa wanafanya kazi katika mambo kama ya meli kama hawa *Danaos* ambao tume *proposal* kwamba wao wanakwenda kufanya kazi nje lakini kwa kupitia mikondo ya meli, waziri anasemaje kuhusu hili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kuhusu mabahari *Danaos* wanasimia masuala ya ubaharia wafanyakazi wanaokwenda kufanya kazi za ubaharia nje.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mpaka sasa hivi kwenye wizara yetu hatujashughulikia baharia hata mmoja, lakini kama watapatikana

kutaka kuwashughulikia tunaweza tukatafuta utaratibu kwa sababu ni suala la kuwatafutia kazi, mahapa watakapoweza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan Said samahani, Mhe. Waziri anatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi suala hili ambalo anazungumzia Mhe. Mjumbe suala la utumishi na usimamizi ya masuala ifara ya ubaharia ni masuala yanayosimamiwa na Sheria *ZMA* kwa imani yangu, kwamba taratibu za *International Maritime Organization (IMO)* na nyenginezo za ifara zote yanasimamiwa na na sheria zile za husika kwa imani kwamba utaratibu mzuri utakuweko chini ya muongozo wa sheria husika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, sitaki kubishana nao lakini nataka nizungumze tu kwamba Mhe. Waziri niikuwa naridhika zaidi, suala la Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwamba atalifuatilia zaidi kwa sababu kwamba sisi neno hasa vijana kwenda kufanya kazi nje au ajira sio hasa kushindana kisheria na *ZMA*. Nia na serikali ni moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimpe pole kwanza Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, kufanya mazoezi katika mwezi huu wa Mtukufu wa Ramadhan kusimama na kukaa kwa kumsaidia Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, pole sasa Mhe. Mohammed Aboud. *(Makofi)*

Na matarajio yako utayapata kwa Mwenye ezi Mungu na kunako mabadiliko mie ningekuomba hii wizara ukakae nayo tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja tuna upungufu wa muda.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu wala sina nia ya kuzuiya kifungu, sina nia kabisa niliwatetea sana wafanyakazi wasimamizi katika Idara ya Usalama Afya Kazini, vitetea kazi hawana hata vespa, hawana hata baskeli hawana. Watafanya kazi vipi kitu cha kichekesho hawana *raincoat* wala *rainboot* hata kwenda kwenye soko la Mombasa wanashindwa kwenda. Kwa hivyo, anambie tu atawapatia vespa tano Unguja na Pemba angalau tatu kule mbili hili ni ombi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ombi wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, fedha zikiruhusu tunataka kila mfanyakazi apate mahitaji ya kutendea kazi sehemu za kazi, kwa hiyo tutakapo pata tutafanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, hawa ambao anaowazungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sio wa serikali wote hao tu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ofisini kwangu Afya na Usalama Kazini, wameshanunuliwa tayari vifaa, wameshanunuliwa gari, na wataendelea kupewa uwezo wa kufanya kazi kwa uhakika ili waweze kufikia maeneo yao.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, gari ngapi zilizonunulia, au iko njiani maana yake hivi sasa nawaona mimi katika mazingira hayo, kununuliwa zishanunuliwa hiyo gari moja itafanya sehemu zote. Hiyo gari ipo lakini, isijekuwa ishanunuliwa tu.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimenunua mwaka jana bado inaendelea na kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Imenunuliwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Imekuwa wanaenda maeneo tofauti watu hawa, hawaendi pahala pamoja kwa wakati wote kwa pamoja kwa hiyo wanatafautiana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku tunaendelea.

Kifungu PQ0105	Usimamizi wa Sheria Kazi, Ukaguzi Kazi Na Kazi Staha kwa wote	1,166,100,000

Mhe. Nadir Abdul latif: Tunasema siku zote Wawakilishi wote hawajui kazi zao ndio haya, wanasema ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu Q01	**Jumla Kuu**	**<u>15,590,600,000</u>**

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa tukae. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa kwa heshima na taadhima ...

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane kidogo. Endelea Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Kwa heshima kwa taadhima Mheshimiwa napenda nilishukuru Baraza lako bado lina nguvu ya kutosha. Sasa nasema kama ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo. Ahsante na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa niwahoji wale wote wanakubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapo ndio tumefikia mwisho wa shughuli za leo, lakini nitoe shukurani zangu kwa Mhe. Waziri na changamoto lakini bado kuna mambo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi, muende mukayasimamie kama ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wamependekeza, na hatimae tukifika tukirudi tena mwakani hapa hali iwe shuwari.

Waheshimiwa Wajumbe, walipokuwa wanamalizia, alipokuwa anamalizia Mhe. Waziri kuhitimisha hoja yake, naona mmekuwa mmefurahi sana kwa yale ambayo ameyapendekeza. Kwa kweli, ni bahati mbaya sana, Mhe. Suleiman Sarahan Said alikuwa nje, lakini tunalifikiria lile ambalo amelipendekeza Mhe. Waziri halafu tutaona namna gani tutaweza kulisaidia.*(Makofi)*

Baada ya hapo, Waheshimiwa Wajumbe kwa muda tulionao hoja inayofuatwa ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, haiwahi lakini tutakuja kuanza kesho, pamoja na kwamba mwenyewe nimemuona Mhe. Waziri amefika. Kwa hivyo, nichukuwe nafasi hii kukushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe na niseme kwamba naakhirisha shughuli za Baraza mpaka kesho saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 8:50 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe
24/05/2018 saa 3:00 asubuhi)